ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi

8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa

		Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe

31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 07 Disemba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, katika Baraza la Tisa Mkutano wa Saba, kikao cha 11 cha tarehe 11 Oktoba, 2017, Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa mjumbe huyo Ahsante. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi Mhe. Waziri namuona pale ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, wakati ninajibu swali Nam. 11niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyetaka kujua ni hatua gani zilizochukuliwa kuwahifadhi ndege waliokuwa hawajapoteza muelekeo wa kuhama Zanzibar.

Mhe. Spika, jibu ni kama ifuatavyo. Wizara yangu inafahamu kwamba wapo ndege wengi wa asili katika visiwa vya Unguja na Pemba wanaopatikana katika maeneo ya majini na nchi kavu. Aidha bado hakuna tafiti za kutosha za kutambua idadi na aina

zote za ndege wanaopatikana hapa Zanzibar. Hatahivyo, inakisiwa kwamba zipo aina mia moja za ndege wa asili hapa visiwani.

Mhe. Spika, ndege ni miongoni mwa viumbe wanaotembea masafa marefu kutafuta chakula, makaazi na mahitaji yao mengine, hata hivyo ndege wengi wanakuwa na maeneo maalum ambayo wanayatumika katika kukaa kwa muda mrefu kuendesha maisha yao. Hivyo, basi kuharibiwa kwa maeneo yao ya makaazi na malisho kunapelekea kupungua au kutoweka kabisa kwa aina fulani za ndege hao.

Mhe. Spika, ili kupunguza ongezeko la kupotea kwa aina ya ndege wa asili wizara yangu inafanya juhudi za makusudi za kuhifadhi makaazi ya ndege waliopo Zanzibar mkakati inayotumika katika kuwahifadhi ndege hao ni kama ifuatavyo.

Kutenga maeneo ya misitu ya hifadhi ya serikali ambayo yanatoa fursa na makaazi na maeneo ya kuzalia kwa aina mbali mbali za ndege, hifadhi hizi zinajumuisha zile za kitaifa kama vile Hifadhi ya Taifa ya Jozani, Ghuba ya Chwaka kwa Unguja, Msitu wa Hifadhi wa Maumbile wa Ngezi, Vunawimbi, Msitu Mkuu na kadhalika kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, wizara yangu inawashajihisha wanajamii kuanzisha maeneo yao ya hifadhi wa misitu ya jamii katika vijiji vyao, ili kuhifadhi misitu, wanyamapori na ndege waliomo humo. Vilevile, wizara yangu inawashajihisha wanajamii kuanzisha kamati zao za kuhifadhi za vijiji na shehia na kusimamia masuala ya uhifadhi wa maliasili na mazingira katika maeneo yao. Kutoa elimu kwa jamii kupitia kamati zao za uhifadhi wa vikundi vya uwindaji, ili kufahamisha umuhimu wa kutunza misitu wa maeneo yanayotumiwa na ndege na wanyama wengine, uhifadhi huu pia unajumuisha udhibiti wa uvunaji wa miti mikubwa ambayo hutumiwa kama makaazi ya ndege pamoja na kudhibiti uundaji

haramu wa ndege hao. Kuzuia usafirishaji wa ndege hai kwenda nje ya nchi.

Mhe. Spika, pia wizara yangu inawahamasisha wanajamii kuwafuga ndege kwenye mazizi, ili kuweza kupata mbegu iwapo aina fulani ya ndege watapungua au wako hatarini kutoweka, kuondoa au kuwaua ndege ambao ni wavamizi kwa ndege wengine pindi ikigundulikana ndege wa aina hiyo ni hatari kwa ndege wa asili.

Mhe. Spika, kwa mfano uangamizaji wa kunguru weusi, ambao wameonekana kuta tishio kwa ndege wa asili wa Zanzibar kama vile Manna, Zuwarde na kadhalika. Vilevile, wizara yangu inadhibiti uingizaji wa ndege wa kigeni ambao hawana asili ya Zanzibar, ili kuepusha kuongezeka kwa ndege wavamizi na hivyo kupunguza uwezekano wa uwepo wa maadui wa ndege wa asili, udhibiti huu unasaidia kupunguza kuingia kwa maradhi ya ndege hapa nchini.

Mhe. Spika, kwa vile wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwepo kwa ndege wa aina mbali mbali kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kijamii na kimazingira……..

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, jawabu lako ni refu mno linatosha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, namalizia.

Mhe. Spika: Basi panatosha hapo ni refu sana. Nafikiri lilikuwa lisharidhisha pale pale mwanzo tu, unatakiwa ujibu kwa ufupi sana. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar Pamoja na Kuwezesha Ushajiishaji na Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo): Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar Pamoja na Kuwezesha Ushajiishaji na Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 49

Mpango wa Kuvisaidia Vikundi vya Sanaa

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa kazi za sanaa za Kizanzibari ni kivutio kimoja kikubwa kwa wageni, kazi ambazo pia hufaywa na vikundi mbalimbali vya watu wasioona kwa ajili ya kupata kipato cha kuwawezesha kumudu maisha yao.

(a) Je, kuna mpango gani ambao umekusudiwa kuvisaidia vikundi vya ujasiriamali na sanaa kwa watu wasioona ambao wanavipaji katika fani mbalimbali.

(b) Je, kuna mpango gani wa kukitembelea kikundi cha watu wasioona kilichopo Mtambile, Mkoa wa Kusini Pemba ambacho ni maarufu kwa kazi za kusuka mazulia ya magunia ambayo yana bei kubwa, ili kusaidia kuzitangaza bidhaa zao ndani na nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa sasa itavipatia ruzuku vikundi 10 vya wajasiriamali na sanaa vya Watu wenye Ulemavu kwa lengo la kukuza vipaji vyao. Aidha Idara imo katika kutekeleza mpango kazi wake wa mwaka 2017/2018 wa "Uwezeshaji wa Watu wenye Ulemavu".

Mhe. Spika**,** Baraza la Sanaa Zanzibar, linautaratibu wa kuvitembelea vikundi mbalimbali vya sanaa vilivyosajiliwa, kwa lengo la kuvijengea uwezo na kuviwezesha, ili kukuza sanaa na kuendeleza biashara wanazozifanya.

Mhe. Spika**,** Kikundi cha Watu Wasioona kilichopo Mtambile, Mkoa wa kusini Pemba bado hakijajisajili katika Baraza la sanaa la Zanzibar. Hivyo, Idara ya Watu wenye Ulemavu inaendelea na utaratibu wa kuvipatia mafunzo na kuvihamasisha vikundi mbalimbali vya sanaa, ili viweze kujisajili na kufaidika na mpango wa Baraza la sanaa la Zanzibar.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suali dogo la nyongeza.

Kile Kikundi cha Watu Wasioona kilichopo pale Mtambile tulikitembelea na kikapeleka malalamiko makubwa kama kimeshahangaika sana kupatiwa usajili, jambo ambalo limekuwa ni gumu ukitilia maanani kwamba wao wenyewe ni walemavu.

Je, idara hiyo inayoshughulikia mambo kama hayo, ina mpango gani wa kuvisaidia vikundi vyenye mwelekeo mkubwa kama kile cha pale Mtambile, kuweza kuvisaidia kupata usajili na hatimae kufaidika kama vinavyofaidika hivyo vyenginevyo ahsante sana Mheshimiwa.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwalikishi swali lale la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ili tutambue kwamba kweli zipo changamoto zinazovikuta baadhi ya vikundi vya watu wenye ulemavu katika maeneo tofauti hasa katika wakati wa usajili. Kwakweli, jambo kubwa ambalo idara imekuwa ikifanya baada ya kuvitambua na kuvihamu, idara imekuwa ikivisaidia vikundi vile, ili kuweza kupelekea kuweza kujisajili, tunapowaachia wao wenyewe kunakuwa kuna tatizo kuweza kufikia maeneo yote kuweza kupata usajili. Sasa jukumu kubwa la idara baada ya kuvitambua na kuviona na kuthamini kazi wanayoifanya tunakuwa tunahangaika sasa kuweza kuvipatia usajili katika maeneo husika.

Changamoto nyengine, mara nyingi katika baadhi ya vikundi hivi wengi wanakuwa hawana ule uelewa wa kutosha namna gani vikundi vinahitajika kusajiliwa. Idara imekuwa ikijitahidi sana katika kutoa elimu ya kutosha na kutoa mwelekeo na muongozo

kwa vikundi vile, ili kuweza kupata usajili wa kudumu katika maeneo tofauti.

Mhe. Suleiman Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweka *Hansard* sawa naitwa Suleiman Makame Ali. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri ulisema kwamba watu wenye ulemavu wanawathamini na kuna Idara ya Watu wenye Ulemavu katika Wizara yao, lakini watu wenye ulemavu hususan walioko vijijini wenye ulemavu wa kuona yaani, niseme vipofu mara nyingi husahaulika katika jamii, hususan walioko mule vijijini.

Je, wizara yake kupitia Idara hii ya Watu Wasioona ina mpango gani kuhakikisha kwamba makusudi kuwasajili watu hawa wote, ili kupata huduma zile za jamii na za lazima kutoka kwenye wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba tutambue kwamba Waheshimiwa Wajumbe kuwa idara yetu ni Idara ya Uratibu katika Mahusiano na Watu Wenye Ulemavu, tunavyokifanya sisi hatuwezi kwenda kuwabagua wenzetu na unapowazungumzia watu wenye ulemavu unazungumzia watu wenye ulemavu wa aina tofauti. Sasa wote hawa kwetu sisi wanakuwa *categorise* katika kundi moja, tunachokifanya sisi ni kuwaasisi mpaka sasa hatujabahatika kuweza kusahau kundi lolote miongoni mwa watu wenye ulemavu ndani ya Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana ukifika idarani kwetu tutakupa aina tofauti na sehemu walipo watu hao wenye ulemavu wapo ambao wana ulemavu wa viungo tofauti, lakini hawa wanye ulemavu wasioona, pia nao sisi tuseme tu idara pamoja na serikali hatujawasahau tunawatambua, tunawathamini. Vilevile, Mhe. Mjumbe akifika idarani kwetu tutamuelekeza tutamfahamisha hawa tunaowataka wapo sehemu hii na wengine wapo sehemu hii, ilimradi kila mkoa takwimu zao tunazo kwa wale ambao tayari wameshakuwa na jumuia na kuwa na utaratibu unaotambuliwa. Nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 90

Kutoendelea Kwa Mafunzo ya Vijana wa JKU

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) linastahili pongezi kwa kutoa mafunzo ya vijana katika Kambi za Unguja na Pemba. Katika kuadhimisha sherehe za kutimiza mwaka mmoja wa vijana hao, tumeshuhudia vijana wakiwa wamehitimu mafunzo vizuri, katika vitendo na kadhalika. Kwakuwa Mhe. Waziri wa wizara hiyo alifurahishwa na mafunzo hayo na kuwataka Makamanda wazidi kutoa mafunzo hayo.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea tokea mwaka 1999 hadi sasa mwaka 2017 mafunzo mazuri kama hayo hayakuwepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 90 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kutoa mafunzo kwa vijana ni miongoni mwa majukumu ya msingi kwa JKU katika fani za kilimo, mifugo, kazi za ufundi pamoja na mafunzo ya msingi ya uaskari, ulinzi, ujasiriamali na ukakamavu. Hatahivyo, kwa kipindi kirefu mafunzo ya namna hii yalikuwa yakikosekana kuendeshwa kwa ukamilifu kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kwenye makambi ya JKU hakukuwa na vijana wa kutosha kwa kuendesha mafunzo hayo. Hii inatokana na kuwa mafunzo ya namna hii hupatiwa sehemu tu ya vijana ambao hutegemewa kuwa viongozi kwa vijana wenzao iwapo watakuwa wengi makambini.

(ii) Upungufu wa vijana kujiunga na JKU ulikuwa mkubwa kutokana na uwezo mdogo wa serikali katika kuwahudumia vijana wa JKU, hivyo ilipelekea kukosekana haja ya kuendesha mafunzo ya namna kama ile ya uongozi wa vijana *(Volunteer Leaders).*

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwakuwa mafunzo haya yaliyotolewa, tumeshuhudia yakifanyika katika makambi ya Unguja na kwa kuwa kule Pemba vilevile ziko kambi za JKU na kambi la Mafunzo na nyenginezo kama ambavyo vipo kwa upande wa Unguja. Je, mmejipanga vipi kutoa mafunzo haya kwa vijana walioko kwenye Makambi ya Pemba, ili na wao kuweza kupata mafunzo mazuri na kuweza kuhitimu katika taaluma ambayo mnawapatia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa

ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Kwanza nimpongeze kwa kuliona hilo kuona kwamba kuna haja na kwa upande wa kisiwa cha Pemba vijana wetu kuendelea kupata fursa hii. Lakini majibu ni kwamba Mhe. Spika, katika kozi ile ya uongozi ambayo imefanyika hapa Unguja ilikuwa na mchanganyiko wa baadhi ya vijana ambao walitoka katika kambi za kisiwa cha Pemba.

Jengine ambalo tunaangalia ni mpango gani. Mhe. Spika, kwa kadri ambavyo tutaendelea kupata hawa vijana tutazingatia sana kuona kwamba kwa kipindi kinachokuja tuongeze wigo mpana zaidi kuona kwamba, kozi kama ile hata kama tulikuwa na mchanganyiko wa vijana kutoka Pemba. Lakini tuifanye pia na kule Pemba kuonekane nako tuweze kufanya ile kodi kule kisiwani Pemba. Vilevile jibu ni kwamba nimwambie Mhe. Mwakilishi mchanganyiko ulikuwepo pia na vijana kutoka Pemba.

Nam. 1

Msamaha wa Vyakula kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan

Mhe. Machano Othman Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein inastahili pongezi kwa kusimamia vyema ukusanyaji mapato katika mwaka 2016/2017, hatua ambayo imeiwezesha kutoa fedha za matumizi *(OC)* kwa zaidi ya 90% kwa wizara nyingi. Pamoja na hatua hiyo nzuri, bado wapo wakwepa kodi ambao wanapunguza kasi ya maendeleo.

Hivi serikali inajua kwamba msamaha wake wa kodi za vyakula muhimu wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani hauwanufaishi wananchi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza namuunga mkono katika kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein katika kusimamia ukusanyaji wa mapato katika mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la msamaha wa kodi za vyakula muhimu wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Serikali katika kuwajali wananchi wake imeweka utaratibu huu wa kutoa misamaha ya kodi ya bidhaa muhimu, kama vile mchele, unga wa ngano na sukari, ili kuwawezesha wafanyabiashara kuweza kuuza bidhaa hizi kwa bei nafuu ambayo mwananchi wa kawaida ataimudu. Imekuwa ikifanya hivyo si kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani tu, lakini ni kwa kipindi cha miezi yote, ambapo kodi ambazo zinalipwa kwa bidhaa hizo ziko chini ya kiwango cha kodi cha Afrika Mashariki ambacho ni asilimia 75. Badala yake bidhaa hizo zinalipiwa kodi kati ya asilimia 10 na 12.5, na punguzo hilo kwa kiasi kikubwa limeweza kupunguza bei za bidhaa hizo katika masoko ya Zanzibar ukilinganisha na masoko ya Tanzania Bara.

Mhe. Spika, kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani punguzo hili la kodi huendelea kupunguzwa kwa bidhaa hizi muhimu pamoja na tende, ambayo huliwa kwa wingi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, ambapo tende hupunguzwa kutoka kiwango cha asilimia 25 mpaka asilimia 10.

Faida au manufaa ambayo serikali inayokusudia kumfikia mwananchi wa kawaida ni mbili:
Kwanza kutoadimika kwa vyakula hivi,
Pili kuwepo kwa unafuu wa bei.

Mhe. Spika, kwa upande wa tende, faida zote mbili zimekuwa zikionekana. Tende huwa kwa wingi katika mwezi mtukufu na bei pia hushuka mfano katika mwezi wa Ramadhani uliopita tende iliuzwa kwa shilingi elfu 2,000 mpaka elfu 4,000 kwa kilo. Ukilinganisha kabla ya na baada ya Ramadhani bei zilikuwa 3,000 mpaka 5,000 kwa kilo hutegemea na aina ya tende.

Mhe. Spika, kweli katika upande wa vyakula vyengine, mchele, unga wa ngano na sukari, napenda kukubaliana na Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kuwa bei huwa hazibadiliki sana ingawa msamaha wa kodi umetolewa. Ingawa mtakubaliana na mimi kuwa vyakula hivyo vinakuwepo kwa wingi katika miezi hii.

Mhe. Spika, uwepo wa vyakula na msamaha wa kodi kwa vyakula muhimu katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani umekuwa ukiwanufaisha wananchi kwa kuwa na uhakika wa kupatikana kwa vyakula na kwa unafuu wa bei. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na wafanyabiashara tutaendelea kuzifanyia kazi changamoto zinazojitokeza, ili kujua jinsi na wakati gani muafaka kwa msamaha wa kodi wa vyakula gani muhimu kwa ajili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani utolewe, ili wananchi wazidi kufaidika kwa msamaha huo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake yenye ufasaha. Lakini pamoja na majibu yake hayo naomba niulize swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ametueleza Mhe. Waziri kwamba kwa Afrika Mashariki sukari, mchele na unga ni 75%, lakini Zanzibar kwa kuwaelewa hali ya wananchi wake na mahitaji halisi tunatoa mpaka 25% na bei ndiyo tunakuwa tunatumia kwa mwaka mzima. Lakini wakati wa Ramadhani serikali inakwenda mpaka 0% kwa mchele sukari na unga, lakini haionekani tofauti ya bei ya kati ya Mfungo 9 na Ramadhani, bei inakuwa ni ile ile.

a. Je, hapa serikali haionekani kama inapiga changa la macho na wafanyabiashara.

b. Tende mwezi wa Ramadhani inatolewa msamaha wa kodi, lakini wafanyabiashara wengi wanaleta tende siku za mwisho wa Ramadhani na baadaye mzigo uke unauzwa katika mwezi wa kula mchana na bei ya tende inakuwa kubwa. Nalo hilo halioni kama linakosesha serikali mapato.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni lazima tuelewe utaratibu wa uagiziaji wa vyakula, lakini pia kiasi gani inachukua kuagiza vyakula kutoka nje mpaka kufika Zanzibar. Kwa upande wa mwezi wa Ramadhani mara nyingi wafanyabiashara wanapokuwa wanaagiza vyakula wanakuwa wanaagiza vyakula kwa muda mrefu. Kipindi kile tulipokuwa tunafanya utafiti tunakuta kama vyakula kwa mfano mchele, unga wa ngano na sukari inakuwa vimeshaagizwa na vipo nchini. Kwasababu moja kubwa tunataka kuona uhakika wa vyakula ndani ya nchi, sasa kama kutakuwa na upungufu wa vyakula kati kati na ndani ya maghala hakuna vyakula ndio mnaona ghafla moja bei huwa zinapanda.

Kwahivyo, wafanyabiashara wengi mara nyingi wanakuwa wanaagiza vyakula vyao kwa muda wa miezi mitatu au miezi miwili au miezi minne. Mara nyingi huwa inatokezea kwamba ule wakati wa Ramadhani kwa mfano kama mchele na unga wa ngano, sukari sio aghalabu, unakuta kwamba ndani ya maghala kunakuwa tayari kuna vyakula vya nyuma. Kwahiyo, inapokuwa vinaagizwa vyakula vya Ramadhani wakati vyakula tayari vimo ndani na bei inakuwa bado wakati ule haijaingia bei ya Ramadhani.

Mhe. Spika, natoa mfano wa mwaka jana. Mwaka jana vyakula vya Ramadhani vilivyoingia vikachelewa kutolewa kwasababu kuna matatizo ya bandarini, kwahivyo vyakula vikawa vinaendelea na bei ya nyuma wakati bei mpya ilivyokuja Ramadhani ikawa tuko mwishoni mwa Ramadhani. Haya inakuwa siyo sana kwamba ni makosa au ukwepaji wa kodi, utaratibu unakuwa vilevile unamazonge kwasababu vyakula vinakuja mapema, lakini vya Ramadhani vinachelewa kushushwa kwasababu ya utaratibu na wakati mwengine bandarini au meli zinakwama Bara au zinakwama hapa kutolewa.

Lakini la pili kuhusu suala la tende. Mhe. Spika, pia niseme hivyo hivyo. Natoa mfano wa mwaka jana tende zilikuja mapema lakini kulikuwa na msururu mrefu wa meli bandarini. Kwahiyo, tayari ilivyokuwa zikitolewa tende zikawa zimetolewa kati kati ya Ramadhani, matokeo yake ilicheleweshwa na bei ikawa tofauti na baadaye ilipotolewa ikabidi iendelee pia baada ya Ramadhani.

Lakini nilisema katika jibu mama kwamba tutakaa Wizara ya Fedha, wizara yetu pamoja na wafanyabiashara, ili kuona utaratibu gani mzuri tutakaoufanya kwa ajili ya kuweza bidhaa za Ramadhani zifike kwa wakati na kwa siku za Ramadhani. Lakini hii pia itabidi tukae na watu wa mawasiliano kwasababu wao ndiyo wanaushughulikia masuala ya meli kuingia na kupakuwa

vyakula. Mhe. Spika, nadhani Waheshimiwa Wajumbe wenyewe waliona mwaka jana tulivyokuwa tunapata tabu meli zipo bandarini, lakini zilishindwa kushusha mizigo kwasababu ya *line* ilikuwa ndefu sana ya meli ambazo zilikuwa na vyakula vya Ramadhani.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada yake kubwa ya kuhakikisha kwamba Zanzibar chakula kinapatikana kwa wingi katika nchi yetu. Lakini hata katika bei za kila leo sasa hivi bei imeshuka kutokana na wingi wa chakula na mambo mengineyo ambayo tunapata kwa wananchi wetu.

Swali langu liko hapa. Mhe, Spika, kwa kuwa serikali yetu ina imani sana na wananchi wake, na zaidi na zaidi hasa watu wanyonge ndiyo maana ikapunguza kiwango kikubwa cha kodi, kwa ajili ya wananchi wetu wapate manufaa hususan zaidi mwezi wa Ramadhani. Je, kwakuwa mchezo huo upo unafanyika kwa baadhi ya wafanyabiashara katika nchi yetu, na wanaonekana na wanajulikana. Wizara inachukua hatua gani dhidi ya wale ambao wanakwenda kinyume na utaratibu uliowekwa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwanza lazima niseme kwamba serikali yoyote iliyokuwa makini itakuwa inaangalia hali za wananchi wake zinavyokwenda. Lakini pia naomba mkumbuke kwamba kuna tafauti kubwa sana katika Afirika ya Mashariki nzima kati ya wananchi wa Zanzibar na wananchi wa nchi nyengine kwa mfano hata wananchi wa Tanzania wanaokaa Bara. Zanzibar mfumko wa bei unakuwa kidogo tafauti kwasababu gharama za maisha zinakuwa ni ghali zaidi hasa vyakula, kwasababu vyakula vingi tunategemea kutoka

nje ya Zanzibar. Ndiyo maana serikali hapo nyuma, na mjue utaratibu sasa hivi wa kutoa *exemption* lazima uwende ukazungumzwe Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilituma *delegation* tukashiriki katika Kikao cha Afrika Mashariki kuomba kwamba Zanzibar katika masuala ya kodi zinazotoka nje kwa sababu kuna kodi ya pamoja *external tariff* kwa vitu vinavyoingia nchini tukaomba maalum kwa Zanzibar yaani, tusilipe kodi viwango hivi vinavyotakiwa vikubwa, ndio maana tukakubaliwa kwamba tulipe viwango hivi ambavyo vitakuwa vinawasaidia wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, lakini la pili suala la bei ya vyakula sio suala la kodi peke yake, hapa kuna viwili vinachangia. Kwanza kinachochangia bei ya vyakula ni bei ya vyakula vyenyewe huko tunakonunua. Kwa mfano, kipindi cha nyuma bei ya mchele ilipanda ghafla na kipindi chengine bei ya sukari ikapanda, sasa hivi vyakula hivi bei zake zimeshuka chini. Moja hii inasaidia kushusha bei ya vyakula.

Pili, sisi kama Zanzibar hatuna mkono wa kupanga bei ya dola yaani, *foreign exchange*, hii inapangwa kwa mujibu wa uchumi unavyokwenda na inayosimamia ni Benki ya Tanzania, ambayo Makao Makuu yake ni Dar-es-Salaam sisi tunaona nini tunafaidika.

Kwahiyo, vitu hivi viwili ambavyo havipo ndani ya mikono yetu vinasababisha bei kupanda na pia bei kushuka. Niseme kwamba wizara yetu tunakaa na wafanyabiashara na tunaangalia vitu vyote hivi vinavyotokea, tunaangalia bei ya vyakula kule nje, tunaangalia bei ya dola inavyokuwa, tunaangalia vile vile hali halisi ya wananchi pamoja na faida ya mfanyabiashara. Pindipo tunapoona wafanyabiashara katika bei elekezi ambazo tumewapa na tonatoa bei elekezi mara kwa mara, ili kuona bei zisiwaumize

wananchi pamoja na msamaha huwo wa kodi. Tunapoona kwamba bei elekezi imepindukia na bei imepandishwa bila ya msingi, tunachukua hatua ya kuwaita wafanyabiashara wale na kuwaambia kwamba warudishe na waweke bei serikali ambayo inaamini kwamba ndiyo elekezi.

Mhe. Spika, huwo ndiyo utaratibu tunaoufanya, lakini mpaka sasa hivi tumeona hali inakwenda vizuri kwasababu wafanyabiashara wengi tuliokwenda nao tunaona hawajakiuka kiwango kikubwa kinachotia hofu nakuwaumiza wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, nashukuru sana na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, swali linasema hivi serikali inajua kwamba msamaha wake wa kodi za vyakula muhimu wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani hauwanufaishi wananchi. Kwanza napenda kuipongeza serikali kwamba serikali inaijua umuhimu wa Ramadhani na huwa inatoa msamaha wa kodi kwa wafanyabiashara, ili chakula kiwe rahisi katika mwezi Mkutufu wa Ramadhani. Lakini kinachofanyika katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kwamba wafanyabiashara huwa hawapunguzi kodi, nitatoa mfano.

Mhe. Spika, Ramadhani iliyopita tende kabla ya Ramadhani ilikuwa inauzwa 27,000 ndani ya Ramadhani ikafika 92,000 kwa boksi, hii inatokana na ukosefu wa Tume ya Bei *strong*.

Mhe. Spika: Uliza swali Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Naomba kumuuliza Mhe. Waziri, lini wizara yake itaweka Tume ya Bei, ili iwe inafanya *monitoring* ya bei ya kununua na bei ya kuuzia wananchi kwasababu bado

wananchi wanapata shida, wafanyabiashara nilisema hawana dini, dini yao ni faida na wanawasumbua wananchi.

Mhe. Spika: Ahsante inatosha Mheshimiwa, lini mtaweka Tume ya Bei, Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimeshajibu pale mwanzo lakini nitajibu hili jengine ambalo amelizungumza Mheshimiwa la mwisho.

Mhe. Spika kama nilivyosema kwamba tuna *monitor* kila siku masuala ya bei zinazokwenda na zinazobadilika za nje na za ndani. Lakini kama nilivyosema suala la tende za mwaka huu tukumbuke kwamba meli ilipokuja ilikaa nje ya bandari kwa muda wa wiki tatu, *by the time* tunaingilia kati tende ilivyotolewa tayari Ramadhani imeshakwenda. Kwahivyo, tende tuliyokuwa tukitumia mwaka huu ni tende ambayo ilikuwemo tayari ilikuja siyo hii ya Ramadhani.

Mhe. Spika, kuhusu Tume ya Bei, sisi kama wizara tumeona kuna tofauti au matatizo kwasababu tunataka kufanya biashara Zanzibar iwe biashara ambayo inasimamiwa siyo biashara holela. Kwanini nikasema hivyo? Kwakweli, hapo nyuma tulikuwa sisi tuna Sheria ya Ushindani Halali ya Kumlinda Mlaji. Sheria hii mpaka leo ipo, lakini vyombo vyake ambavyo vilivyotakiwa visimamie sheria hii kama kuwe kuna chombo cha ushindani halali lakini pia na *tribunal,* vile vile ya kusimamia mabishano na mambo mengine yanayohusu kama hayo ya bei.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kipindi hichi cha Baraza letu tutawasilisha Sheria kwa mara ya kwanza ambayo itazungumzia masuala ya kuanzisha Sheria mpya ya Ushindani Halali na Sheria mpya vile vile ya Kumlinda Mlaji. Tunavyozungumzia kumlinda mtumiaji au mlaji maana yake nini,

moja ya jambo tunalopendekezwa mle kuwa na Kitengo maalum cha Kusimamia Masuala ya Bei na kusimamia masuala mengine yanayohusu hayo.

Mhe. Spika, kwakweli Mhe. Hassan Khamis Hafidh, haya ndiyo maoni yake siku zote. Kwahiyo, awe na moyo, asubiri kikao cha January kinachokuja au pengine cha mwezi March sheria hii itazungumzwa na moja ya kitengo kinachotakiwa kuanzishwa ni kuhusu kitengo cha kusimamia bei, ili bei ziweze kujulikana na ziweze kumilikiwa na wanafanyabiashara wasiwezi kuwa na upenyo wa kuwaathiri wananchi. Asante Mhe. Spika.

Nam. 34

Athari za Kuondolewa Chuo cha Nkurumah

Mhe. Miraji Khamis Mussa - Aliuliza:

Serikali ilikiondoa Chuo cha Uwalimu cha Nkurumah na kukiunganisha na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kwa matumaini ya kuimarisha zaidi taaluma ya walimu katika ufundishaji kabla ya kuunganishwa *SUZA*. Chuo cha Nkrumah kilikuwa kinatoa mafunzo ya Uwalimu ya Daraja *"A" (Grade "A"),* ambapo mafunzo hayo kwa sasa hayapatikani kwenye Chuo Kikuu cha *SUZA*.

(a) Je, ni utafiti gani wa wizara uliofanywa na kupelekea kuondoa Chuo cha Uwalimu Nkrumah na kukiunganisha na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) na kusababisha kuondoa mafunzo ya Uwalimu ya Daraja "A".

(b) Je, kuna kipimo chochote cha mafanikio kilichoonesha matokeo mazuri toka Chuo hiki kiunganishwe na *SUZA*, kama yapo naomba kuyafahamu kwa faida ya wakwezi na wakulima.

(c) Hatua gani, zilizochukuliwa za kitaaluma katika *"content and methodology"* baada ya kukiunganisha Chuo cha Nkurumah kwenda *SUZA*, ili kuendeleza yale mema yaliyokuwa yakipatikana kwenye Chuo cha Nkrumah.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye vipengele (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikiunganisha Chuo cha Uwalimu cha Nkrumah na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa madhumuni ya kuimarisha taaluma ya uwalimu. Kabla ya kuunganishwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo cha Uwalimu Nkrumah, kilikuwa kinatoa mafunzo ya ualimu cheti daraja la A, mafunzo ya Stashahada ya Uwalimu Sekondari na mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu. Baadhi ya wakufunzi waliokuwa katika Chuo cha Uwalimu Nkrumah, walihamishiwa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na baadhi katika Chuo cha Kiislamu kuendeleza kutoa mafunzo ya Uwalimu. Mafunzo ya Uwalimu Cheti Daraja "A" hayatolewi na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar bali yanaendeshwa kwa njia ya elimu masafa kwa walimu walioko kazini ambao hawajasomea uwalimu.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Kabla ya kuuganishwa kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliiomba Shirika la Kimataifa la *UNESCO* kutoa ushauri kuhusu uanzishaji wa Chuo Kikuu hapa Zanzibar. Shirika hilo lilifanya utafiti mwaka 2000 na ripoti yake ilipendekeza Chuo Kikuu kianzishwe kwa

kuviunganisha vyuo mbali mbali kuwa chini ya *SUZA*. Vyuo vilivyopendekezwa ni Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni na Chuo cha Sayansi ya Afya na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah.

Pia, Sera ya Elimu ya mwaka 2006 imeagiza kuwa mafunzo yote ya uwalimu katika vyuo vya walimu vya serikali visimamiwe na Chuo Kikuu cha Taifa. Hivyo, kuunganishwa kwa mafunzo ya uwalimu yaliokuwa chini ya Chuo cha Ualimu Nkrumah na Chuo Kikuu cha Taifa ni sehemu ya utekelezaji wa ripoti hiyo ya *UNESCO* na Sera ya Elimu ya mwaka 2006.

Kuondelewa kwa Mafunzo ya Uwalimu ya Cheti ya daraja la "A" hakukutokana na ripoti hiyo bali ni maamuzi ya wizara yaliyopitishwa kwa madhumuni ya kuinua hadhi na taaluma ya uwalimu hasa kwa walimu wa Daraja la Tatu "A", ambapo wanapojiendeleza wanalazimika kufanya masomo ya Stashahada ya Elimu ya Sekondari. Hivyo, kufutwa kwa mafunzo ya Cheti cha Uwalimu Daraja la "A" na kuanzishwa kwa mafunzo ya Stahahada ya Uwalimu wa Msingi kumeinua hadhi na uwezo wa walimu wa skuli za msingi.

(b) Kuunganishwa kwa Chuo cha Nkurumah na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kumeleta mafanikio makubwa kitaaluma na kimaslahi kwa walimu na wizara kama hivi ifuatavyo:-

Kumekuwa na ongezeko la idadi ya walimu wanaosomea mafunzo ya ualimu katika ngazi mbali mbali. Kwa mfano, katika mwaka 2006, Chuo cha Uwalimu cha Nkrumah kilikuwa na jumla ya wanafunzi 1,620 wanaohudhuria mafunzo ya uwalimu, wakiwemo 929 wa Ualimu Cheti Daraja la III A, 223 Stashahada ya Ualimu wa msingi, 449 Stashahada ya Uwalimu wa Sekondari ukilinganisha na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuanzia mwaka 2006 hadi 2015/2016, jumla ya walimu 4,043,

wamehitimu mafunzo ya uwalimu wakiwemo wahitimu 1,967 wa stashahada za mafunzo mbalimbali ya uwalimu na 2,076 wa shahada ya uwalimu katika fani mbalimbali.

Kuongezeka kwa ubora wa walimu wanaohitimu kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, kutokana na usimamizi na udhibiti wa sifa za kujiunga na ubora wa mitihani yake.

Wahitimu wa Stashahada na Shahada za Uwalimu kukubaliwa kujiunga na masomo ya juu katika vyuo vikuu vya ndani na nje, kutokana na kukubalika kwa vyeti vinavyotolewa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

(c) Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kilifanya mapitio ya mitaala ya mafunzo ya ualimu na mitaala mengine mipya iliandaliwa, kulingana na ubora wa elimu inayotolewa kwa mujibu wa vigezo vya vyuo vikuu. Mapitio hayo yalihakikisha kuwa walimu wanaoandaliwa wanakuwa wamebobea katika fani wanazofundisha na wana uelewa wa mbinu za kisasa za kufundishia. Walimu hao kabla ya kumaliza mafunzo yao wanafanya mazoezi ya kufundisha chini ya uangalizi wa wahadhiri wao. Asante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

Mhe. Waziri, nampongeza sana kwa majibu yako marefu lakini ukiyapitia majibu yake yenyewe yanapishana hayapo katika mtiririko mzuri, ambalo hili jibu unalonipa limekwenda kama vile ambavyo wananchi wanatarajia yamepishana. Naomba nikariri Mhe. Spika kidogo tuu katika tafiti zilizofanywa na Shirika la Kimataifa wamesema kuna vyuo na akavikariri kuna Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni kuwa uinganishwe katika Chuo

Kikuu cha Taifa *SUZA*, Chuo cha Uwalimu Nkrumah na Taasisi ya Sayansi ya Afya.

Lakini pia katika Sera ya Elimu ya 2006 imeagiza vyuo vyote vinavyotoa taaluma ya elimu maana yake viunganishwe chini ya *SUZA*.

Sasa swali langu liko hapa kwanini hadi leo Chuo cha Kiislamu kinatoa mafunzo ya uwalimu wakati sera ya elimu ya 2006 iliagiza vyuo vyote vinavyotoa taaluma ya uwalimu viweko chini ya *SUZA*.

Wizara huku iliafanya maamuzi ya kuiondoa Daraja "A" ni maamuzi ya wizara. Sasa swali langu linakuja Wizara ya Elimu ilifanya maamuzi kuondoa mafunzo ya uwalimu Daraja A kwa vigezo gani bila ya kufanya utafiti. Mhe. Spika nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako naapenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifutavyo:

Ni kwamba suala la uhamishaji wa vyuo kutoka sehemu moja kwenda nyengine ni suala la mchakato ingawa maagizo ya sera yanaagiza hivyo. Lakini tunakwenda hatua kwa hatua hatuwendi kwa pahali pamoja na hiyo Mhe. Mwakiliswhi analifahamu vizuri sana tunakwenda hatua kwa hatua. Hata ripoti nyengine ya kuunganisha vyuo tunakwenda hatua kwa hatua, hatua ya mwanzo vimeunganishwa ambavyo hivi viko sasa, lakini kuna hatua ya pili na tatu *SUZA* yenyewe ina mpango huo na Mhe. Mjumbe analijua hilo tunakwenda hatua kwa hatua.

Wizara iliamua kwa kutumia kigezo cha ubora wa taaluma. Kigezo cha ubora na taaluma maana yake kwamba taaluma iliyo

juu zaidi ni bora zaidi, kwa maneno mengine tulifikia wakati tukaona cheti *content* ya cheti, *methodology* ya cheti iko chini, kwa hivyo walimu hawa ili kuwapatia maarifa zaidi tunakamua sasa hebu tuweke katika kiwango cha stashahada, na kweli walimu wengi wamejiendeleza wamefikia katika hali hii na ubora upo pale pale. Ahsante sana.

Nam. 86

Ukosefu wa Fundi wa Dharura na Kituo cha Huduma za Umeme Micheweni

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Kumekuwa na kilio cha muda mrefu sasa kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni kwa kukosekana kituo cha kuuzia umeme na fundi wa dharura hasa kunapokuwa na hitilafu ya umeme wilayani hapo pindi ikitokezea kuharibika *transfomer*, kuanguka nguzo, kukatika waya kwa kuangukiwa na miti na kadhalika, na kwakuwa jambo hili ni muhimu kwa jamii.

(a) Je, serikali ina mpango gani kwa sasa wa kuweka kituo cha uuzaji umeme na kuachana na kutumia simu za mkononi, jambo ambalo halina uhakika na wananchi kupata usumbufu.

(b) Je, serikali haioni kutokuwepo kwa fundi wa dharura katika wilaya hiyo kunaweza kuleta maafa kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari swali lake Nam. 86 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utoaji wa huduma bora kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba ni jambo linalopewa kipaumbele na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha inajenga mazingira mazuri ya wananchi kufanya shughuli zao za kila siku za kiuchumi na kijamii.

Katika kufanikisha lengo hilo, serikali imekuwa ikibuni na kutekeleza mikakati mbalimbali, ili kuona kwamba pamoja na kupeleka huduma hizi muhimu. Lakini changamoto zinazojitokeza wakati wananchi wanapozitumia zinatatuliwa katika muda mfupi iwezekanavyo.

Mhe. Spika, Micheweni ni Wilaya pekee kwa Kisiwa cha Pemba ambayo bado haijawa na kituo cha kuuzia umeme na kutoa huduma za dharura, na hii inatokana na gharama za uwekaji miundombinu hii kuwa kubwa. Lakini katika kuhakikisha kwamba wananchi hawapati usumbufu kwenye ununuzi wa umeme, shirika liko katika hatua za mwisho za kuanza kutoa huduma hii kupitia makampuni kwa kutumia kutumia *Sim Banking* na kwa kutumia *Point of Sales* mfano wa mawakala wa kutoa na kuweka pesa.

Mhe. Spika, kwa upande wa utatuzi wa matatizo ya umeme. Shirika linashirikiana na Serikali kwenye Wilaya ya Micheweni pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wa Majimbo ya Micheweni na Tumbe, ili kuweza kupata mahali pa kuweka kituo hicho, na baada ya eneo kupatikana hatua za haraka za kuhakikisha wanakuwepo watendaji wa shirika, ili waweze kutatua matatizo yanayoripotiwa zinachukuliwa. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu yake mazuri ya Mhe. Waziri, pia naomba nimpongeze kwa kuchukuwa juhudi ya kuweza kugawa na kufanya *survey* juu

swali langu ambalo nimemuuliza. Lakini napenda nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Waziri pamoja na majibu yako mazuri huu utaratibu wa kulipia benki ni lini utaanza wakati kadhia hii kule Micheweni inaendea.

Kuna ugumu gani wa kutuwekea fundi kwa muda huu ikiwa na yeye bado fundi huyu atakuwa yupo na anasubiria hicho kituo kuweza kujengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika kwanza napokea pongezi, lakini kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo:

Ni kwamba hakuna ugumu wa kuweka mafundi na ndio nia yetu, lakini cha muhimu pia kama nilivyokuwa nimesema namna tunavyoshirikiana basi tupate pale pahala, tukishapata pahapa pa kuwekea wale mafundi basi mafundi watakuwepo pale masaa ishirini na nne.

Lini hii huduma itaanza mafundi wetu ambao watendaji wetu wiki ijao wanaenda kukamilisha hizi taratibu Afrika ya Kusini na kilichokuwa kimebakia sasa ni ukamilishaji wa utaratibu za mfumo wa kuuzia umeme yaani, *P Paid System* baada ya kukamilika hiyo, basi huduma inaanza. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri imekuwa ni kawaida sasa kwa wananchi wangu baadhi yao wa Jimbo la Wawi na baadhi ya wananchi wa Jimbo la Ole kukosa umeme kuanzia saa 12:00 jioni hadi saa 4:00 za usiku yakiwemo maeneo muhimu ya vikosi vyetu vya

upatikanaji 141 KG na 14 KG pamoja na Hospitali ya Vitongoji. *(Makofi)*

Hivi, naomba nimuulize Mhe. Waziri analijua kadhia hii na kama anaijua kadhia hii ni lini Shirika lake la *ZECO* linataondoa kadhia hii kwa wananchi hawa, ili kuondoa usumbufu hususan kwa wagonjwa wetu na baadhi ya wananchi wa maeneo hayo niliyoyataja. hsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Ni kwamba kadhia hii siijui lakini ninavyofahamu inatokezea wakati mwengine umeme unazimwa baada ya kwamba kuna hitilafu kule ambako unatoka, lakini wacha nilichukuwe na tulifuatie tujuwe ukweli wake ukoje ahsante.

Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bissimillah Rahman Rahim*. Mhe. Spika, nakushukuru sana naomba nimuulize swali lenye (a) na (b) Mhe. Waziri wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Kwakuwa mjini na mashamba wananchi washakuwa wingi ndani ya Unguja na Pemba, ni lini sasa wizara yake itafanya vituo vya kuuza umme masaa 24 mjini pamoja na maeneo ya shamba na hasa jimboni kwangu Chaani.

Kwakuwa *ZECO* ni Shirika ambalo umeme wake hauna uhakika unakatika mara kwa mara na fedha wanachukua nyingi. Je, lini wataanza kuwalipa wananchi wanao waunguzia vitu vyao kuzima umeme kila wakati, na umeme kushuka na kupanda uliokuwa hauna uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Nimesema kwamba shirika liko katika hatua za mwisho, kwa ajili ya kuwarahisishia wananchi kupata hii huduma ya umeme usiku, mchana mjini na vijijini. Sasa naomba sana arejee kwenye jibu lakini awe na stahamala apewe muda huu, kwa ajili ya hizi taratibu zikamilike hiyo huduma inawafikia wananchi wote Unguja na Pemba mjini na vijijini.

Kwanza haina utaratibu huo *ZECO* ya kwamba inawasababishiwa wananchi hasara. Lakini pengine inatokezea wakati mwengine umeme umezimwa kule ambako tunachukuwa hitilafu inaweza ikatokezea. Vilevile, pia tuangalie kwenye nyumba husika umesajili vitu vyako vyote ambavyo unatumia, kama unasema una redio lakini huko kuna vitu vyengine baadaye unakuja kulalamika kwamba kile ambacho haujakiorodhesha kimeungua inakuwa shida kidogo, tuwe waaminifu na baadaye hayo mengine yanazungumzika. Ahsante sana.

Nam. 28

Hitilafu za Umeme MV. Mapinduzi II

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa uamuzi wake wa kununua Meli ya MV. Mapinduzi II kwa ajili ya kuwapunguzia wananchi wake tatizo la usafiri. Hatahivyo, kwa bahati mbaya meli hiyo tokea ilipofika na kuanza safari zake kumekuwa kukijitokeza matatizo ya umeme mara kwa mara.

Je, Mhe. Waziri kuna sababu gani zinazopelekea kuwepo hali hiyo.

Mhe.Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake Nam. 28 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, matatizo yanayojitokeza kwenye MV. Mapinduzi II ni hitilafu za kawaida za kiufundi katika mitambo yake ambazo kwa vyombo vya baharini ni kawaida kutokea. Changamoto kubwa inayosababisha meli kusitisha huduma ni ukosefu wa vipuri vya dharura ndani ya meli, hivyo inapotokea hitilafu za kiufundi, wizara yangu kupitia Shirika la Meli hulazimika kuagiza vipuri husika ambapo kwa kawaida muda wa kuagiza na kupatikana vifaa unakuwa si chini ya wiki moja.

Katika kukabiliana na changamoto hii, shirika limeanza kuagiza vipuri hivyo kwa awamu na kuviweka melini ili kurahisisha matengenezo na kuepuka kusitisha huduma kwa meli hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa MV. Mapinduzi II imekuwa ikisitisha safari zake kwa kuharibika mara kwa mara na kwakuwa meli hii kununuliwa kwake kumekuwa ni muda mdogo tuu tokea kufanya kazi yaani, kuja kwake hapa Zanzibar. Je, meli hii ina *guarantee* ya muda gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Meli hii ilikuwa na *guarantee* ya mwaka mmoja na ndio maana ilipofika mwezi wa Septemba 2016 ilipelekwa chelezoni na wale wajenzi wa meli walichuka hatua kulipia gharama zile pamoja na sisi serikali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b). Kwakuwa, Mhe. Waziri majibu yake yamekiri wazi kuwa tumeshaanza kununua vipuri vya kutengeneza meli hii katika hitilafu zilizokuwa zinajitokeza naomba kumuuliza swali langu lenye vitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:

a. Toka kuanza hitilafu hiyo na kuagiza vipuri ni kiasi gani zilizotumika kununua vipuri hivyo toka hitilafu zilipoanza kujitokeza.

b. Ni kampuni gani tunayoitumia katika kununua vipuri hivyo pale ambapo hitilafu zinapojitokeza. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe.Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama ulivyosema meli yetu hii katika kipindi chake cha kuwepo imeharibika mara mbili mara mwanzo tulinunua *Electroil Model Card* kwa *Euro* 3,500 na matumizi ya juzi yalituharimu kidogo kwasababu iliharibika katika *engine*. Lakini

kwa hivi sasa tunanunua vifaa ambavyo kabisa kama vile *gusket* vile vile *system* ya kuharibika kwa vyoo ambavyo vimetugharimu zaidi ya shilingi milioni za tanzania 50,000,000.

Vile vile kama nilivyosema kwamba sisi huwa tunapenda kwamba meli hii isipate hitilafu. Kwahiyo, kila wakati tunachukua hatua za kuhakikisha kwamba meli hii inakuwa katika ubora wake na vile vile inafanya kazi wakati wowote pale ambao tunafanya kazi zetu za safari. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri amesema kwamba meli hii inaharibika vipuri mara kwa mara. Lakini lengo la serikali ni kuondoshea wananchi usumbufu hususani wanaotoka Pemba kuja Unguja na kutoka Unguja kwenda Pemba, lakini meli hii inaharibika mara kwa mara. Jee, haoni ni kwamba kuisababishia serikali hasara na kwamba faida hapo haipatikani kwenye meli hii.

Mhe.Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na nachukua nafasi hii tena kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali kama nilivyomjibu Mhe. Miraji.

Hii meli ni mpya na kuharibika kwa meli ni jambo la kawaida na juzi tuu kama mnavyojua *Sea Link* nayo imeharibika na hivi sasa nayo bado haijaondoka Pemba na kama tunavyosema tunapokuwa panapotokea matengenezo mafundi wetu wanaifanyia kazi, na hivi vifaa napenda kumjibu pia Mhe. Miraji tunanunua kampuni tafauti.

Matengenezo ya mwisho tuliyafanya kupitia Kampuni ya *Damlet*. Kwahiyo, mimi namwambia Mhe. Mwakilishi amini meli yetu kama ni nzima na mafundi wetu wako tayari wakati wowote ambapo panatokezea matatizo kuitengeneza ile meli.

Matatizo mengine kama hitilafu za umeme kwasababu kile chombo kinatumia mfumo wa kisasa ni mambo ya kawaida, lakini mafundi tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya mara inapotokea hitilafu, kwasababu imeonekana katika ile *system*, basi pale pale zile hitilafu zinatengenzwa, hitilafu ikiwa kubwa ndio inabidi tuagizie vipuri au wataalamu kutoka nje. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 41

Ujenzi wa Barabara ya Konde - Chake

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa Barabara ya Konde - Chake iliyojengwa na Cogefar ilikuwa nyembamba, lakini kwa wakati huo ilikuwa inatosha kutokana na vyombo vya usafiri kuwa kidogo. Kwa hivi sasa barabara hiyo imekuwa haikidhi haja kutokana na kuongezeka kwa magari mengi, hasa malori yanayobeba mchanga, mawe na kifusi kutoka Micheweni na Ndamani kwenye maeneo yanayochimbwa mchanga. Vilevile, kwakuwa zimebaki km 25 kutoka Madenjani hadi Konde.

Jee, ni lini serikali itaitanua barabara hiyo kama ambavyo imefanya kutoka Melitano hadi Madenjani.

Jee, kwa sasa kuna mpango gani wa kuzirejesha alama za barabarani ambazo zilitolewa sambamba na kuvirejeshea vikuta

ambavyo viliwekwa, kwa ajili ya kuonesha masafa ya barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid swali lake Nam. 41 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe Spika, serikali imeanza kuchukua hatua kwa kuipanua barabara ya Melitano-Konde hatua kwa hatua kadri ya fedha zinavyopatikana, na ndiyo maana Mhe. Mwakilishi ameona tayari kipande cha kilomita 13 kutoka Melitano hadi kwenye makutano ya barabara ya Kojani imeshafanyiwa marekebisho na kuipanuwa kutoka upana wa mita sita 6 za mwanzo hadi mita nane (8) zilizokuwa hivi sasa.

Aidha urejeshwaji wa vikuta vya masafa pia utazingatiwa wakati wa utanuzi wa sehemu ya barabara iliyobaki yenye urefu wa kilomita 25 kama alivyopendekeza Mhe. Mwakilishi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri yenye kutia moyo mazuri ahsante sana Mheshimiwa, bidii zimeonekana. Lakini nina swali dogo la kuongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwanza katika swali langu niliulizia swali za alama za barabarani ambazo hukuzijibu lakini kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yako hakutaja ni lini huu mpango utaanza, na lile tatizo la kutokuwepo kwa alama za barabarani ishara zile za usalama lipo na kwasababu hatujui lini tutaanza swali langu lipo hapa.

Jee, wakati tunasubiri huu utanuzi wa hiyo barabara kama ilivyofanyiwa kule uwendelee, na barabara ile haina alama za ishara ya barabarani. Hivyo, ni lini au wizara haiyoni umuhimu wa kuziweka zile barabarani wakati tunasubiri hiyo kazi ya utanuzi ya hiyo barabara ikawa na zile alama.

Jee, ni lini walifikiria wizara wataanza kazi hiyo kwa haraka, ili kuepusha ajali zinazoweza kujitokea kutokana na kukosekana na mambo haya kwa alama hizo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Omar Seif bin Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli hilio tatizo lipo na kama nilivyosema kwamba katika bajeti ya mwaka huu tumetenga milioni 152,000,000/= kwa *road sign* na vile vile kwa ajili ya *road marking*, kwa hiyo namuomba sana Mhe. Mwakilishi awe na subra na hiyo kazi tutaifanya katika kipindi hiki cha bajeti *inshaallah*.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeza Mhe. Waziri kwa ngumu aliyonayo na kubwa lakini asichoke aendelee.

Lakini napenda kumuuliza swali Mhe. Waziri katika brabara ya Mndo, Kizimbani, Miwani mpaka Kiboje ni barabara ambayo siku zote tunaipigia kelele na kuiulizia maswali, lakini hivi karibuni barabara ile imeenda kuparwa na kutiwa fusi na kuwekwa sawa lakini bado haikutiwa lami. Mhe. Spika, ila barabara hiyo hiyo hivi karibuni mvua hizi zinazoendelea tayari imesharudi kama zamani ilivyokuwa na usumbufu bado upo pale pale kwa wananchi wetu.

Jee, kuna taratibu gani Mhe. Naibu Waziri kuirekebisha barabara hii na kuimaliza kabisa kwa kiwango cha lami, ili ule usumbufu usiwepo na usiendelee kuwepo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Spika, ni kweli tunajua kwamba ile barabara ni muhimu sana kwa wakaazi wa Kizimbani mpaka Miwani kwasababu kuna mazao mengi kule ambayo wakulima wanalima akiwemo na yeye. Nataka kumwambia kwamba kwa mujibu wa bajeti yetu tunategemea ikishakujengwa barabara ya Jumbi - Koani, basi barabara inayofuata itakuwa ni barabara ile ya Miwani - Kizimbani. Kwahiyo, tunasubiri wakati ambapo tutapata fedha basi na ile barabara kwa sasa hivi tutachukua hatua ya kuirekebisha zile sehemu zilizopata athari baada ya mvua kubwa kunyesha, lakini tuna ahadi kwamba ile barabara pia tuitie lami. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 64

Kuwekwa Alama Barabara ya Ole/Kengeja

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa kazi ya ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja inaendelea vizuri na matumaini yao kwamba barabara hii itakamilika sio muda mrefu, na kwasababu baada ya kukamilika kwa barabara hiyo maeneo yote ambayo yamepitiwa na barabara hiyo kama vile Pujini, Mtangani, Kengeja na mengineo yataongezeka thamani sana na kusababisha wananchi kujenga hata kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara.

(a) Jee, wizara imejipanga vipi kuyapima na kuyawekea alama maalumu maeneo ya hifadhi ya barabara, ili kutokutoa mwanya kwa watu kuyabania na kujenga ndani ya maeneo ya hifadhi ya barabara na kusababisha kudai fidia mara nyingine pindi ikitokea kutanuliwa au kujengwa upya barabara hiyo miaka ya baadaye.

(b) Sambamba na barabara ya Ole - Kengeja, wizara ina mpango wa kupima na kuziwekea alama barabara zote za Unguja na Pemba, ili kuepuka matatizo kama hayo ambayo yamekuwa yakijitokeza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vipengele (a) na (b**)** kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara imeweka utaratibu wa kuweka viguzo kwenye mipaka ya hifadhi ya barabara kwa kila mradi wa ujenzi au matengenezo makubwa ya barabara unapofanywa, hivyo barabara hiyo nayo itawekewa viguzo hivyo.

(b) Mhe. Spika, wizara imeshaanza kuweka viguzo kwenye mipaka ya hifadhi ya barabara kwenye miradi iliyokamilika Unguja na Pemba. Aidha, kwa kazi ya uwekaji wa viguzo hivyo, wizara yangu itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti za matengenezo ya barabara kwa kila mwaka kwa ajili ya uwekaji wa viguzo hivyo kwa kila barabara inayosimamiwa na wizara yangu.

Vile vile, Mhe. Spika wizara yangu ina mpango kabambe wa kuweka alama kwenye mipaka ya hifadhi ya barabara Unguja na Pemba, ili kuwawezesha wananchi kuifahamu mipaka ya hifadhi na barabara na hivyo kuepusha uvamizi wa maeneo hayo kwa kujenga majengo na kupanda mazao ya kudumu ambayo hupelekea serikali kugharimu fedha nyingi pasipo na ulazima kwa ajili ya kulipia fidia ya majengo na vipando hivyo wakati wa upanuzi wa barabara husika.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi wanaopenda kujenga kwenye maeneo ya karibu na barabara kufuata sheria na taratibu zilizopo za Mipango Miji na Vijiji pamoja na marekebisho ya Sheria ya Barabara ya mwaka 2012. Mtu yeyote aliyejenga na anayejenga au kutaka kujenga au kupanda vipando ndani ya eneo la mipaka ya hifadhi ya barabara, na kuviondoa viguzo vya mipaka ya hifadhi ya barabara vilivyowekwa kwenye baadhi ya barabara atakuwa amekiuka sheria na atalazimika kuvunja jengo lake kwa hiari kuanzia sasa na kuchukuliwa hatua kwa yoyote atakayebainika kuondoa viguzo hivyo.

Mhe. Spika, wizara yangu imejipanga kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa pamoja na kuvunja majengo yao bila ya kufidiwa kwa yeyote atakayekaidi wito huu, ikiwa pamoja na wale wote walikaidi kuvunja majengo yao baada ya kupelekewa barua na Idara ya UUB za kutojenga lakini waliendelea na ujenzi, kwani orodha ya majina yao tunayo katika wizara yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumeshakuwa na huo mpango kama huu wa kuweka vikuta kwenye mipaka ya barabara ikiwemo barabara ile ya Ole/Kengeja ambayo ndio swali

langu la msingi, na kwasababu kuna watu ambao hajamaliziwa malipo yao ya fidiwa hadi hii leo kwenye ujenzi huo.

Jee, kabla ya kuwawekea hivyo vikuta kwenye hiyo barabara. Wizara ina mpango gani wa kumalizia kuwalipa fidia wale watu ambao hawajawamalizia kuwalipa, ili kuondoa manung'uniko kwa wananchi wetu kwamba serikali inawacheweleshea malipo yao kabla ya ujenzi au na pale ujenzi wao unapoendelea, ili wasihisi kwamba serikali yao inawacheweleshea kuwapa malipo yao. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kama nilivyosema kabla ya kuanza ujenzi wa barabara lazima kwanza tuwalipa fidia na hili ni agizo kutoka kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein. Kama unavyoona hivi sasa barabara ya Ole/Kengeja tumeanza kuwalipa fidia na ndio maana tukaendelea na ujenzi, na sehemu ambayo hatujalipa fidia basi itakuwa kuna sababu maalum ambazo hatujalipa fidia.

Hata barabara ambayo tutaanza hivi karibuni ujenzi wake, barabara hii ya Bububu/Mkokotoni basi tayari wananchi takriban wote waliostahiki kulipwa fidia tayari wameshalipwa fidia. Ni hali ambayo inatufanya sisi baadhi ya wakati kupata gharama kubwa lakini kwa vile serikali yetu inawajali wananchi tutaendelea kuwalipa wananchi fidia, wale wote ambao wamejenga majengo yao katika hifadhi zetu wakati ambapo sheria hii ya 2012 haijapita. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 70

Kutokuwepo Mfamasia wa Kudumu Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa kumekuwa na tatizo la kutokuwepo kwa Mfamasia wa kudumu Pemba jambo ambalo ni tatizo kubwa na sababu Wizara ya Afya inafahamu tatizo hilo.

(a) Jee, ni sababu gani inayopelekea kutokuwepo kwa Mfamasia Pemba.

(b) Jee, ni lini wizara itampeleka Mfamasia wa kudumu Pemba, ili kuondokana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** wizara inatambua kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi wa kada hii hapa Zanzibar. Licha ya uhaba huo wizara imeshaajiri Mfamasia na tayari ameshapangiwa kazi kisiwani Pemba. Katika kipindi chote hiki wapo mafundi sanifu dawa (*Pharmaceutical Technicians,* ngazi ya *Diploma*) ambao wanasaidiana sana kwa masuala yote yanayohusiana na dawa katika hospitali na vituo vya afya. Aidha, vijana wawili wa kada hii ya Famasia ambao wanatarajiwa kumaliza masomo yao mwaka huu wa fedha 2017/2018, pia tunatarajia kuwapanga kazi Pemba kwa umuhimu wake.

Mhe. Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona wizara tunao Wafamasia wa kutosha na wanapangwa na kufanya kazi katika hospitali zote za Unguja na Pemba. Kwa kukimbilia

kukamilisha dhamira hiyo serikali imeturuhusu na kutoa kibali cha kuajiri Wafamasia wakati wowote wanapoomba ajira.

Mhe. Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo na wa viti maalum wawahamasishe vijana wetu kujitokeza kujisomea fani hii, ili tuondokane na uhaba wa Wafamasia Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwakuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kuwa kuna upungufu wa wafanyakazi au wataalamu wa afya, na kwakuwa katika miaka ya 1990 tulikuwa tuna skuli mbalimbali tukizisomesha kama skuli ya *X-ray*, skuli ya *Pharmacy* na skuli ya *Labor* ni kwa nini sasa haturudishi skuli zile ambazo hazipo tukaanza kuwasomesha tena wanafunzi ambao wamejaa na *qualification* zipo, ili kupata wataalamu wengi na wa uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, mawazo yako tunayachukua kama ni ushauri, lakini tunao wanafunzi ambao wako katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya Tanzania kwa mfano India, China wanasomea fani hii na baada ya muda mfupi tunategemea kuwapata na kuwaajiri katika taasisi yetu ya afya.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza, lakini kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo yanatupeleka mbele katika kutatua changamoto za afya.

Lakini Mhe. Spika, inasemekana kuna kituo cha afya tulisaidiwa na wenzetu wa *Milele Foundation* katika kijiji cha Ukongoroni, na lipo tatizo la jumla la Wafamasia pamoja na madaktari. Je, wizara yake inalitambua hili, kama inalitambua kuna utaratibu gani wa kutatua changamoto hiyo, ili serikali iende sambamba na shida za wananchi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, serikali tunalitambua hilo na katika harakati za kutafuta vijana wa kuwaajiri kufanya kazi hizi za afya, basi tumepanga kukamilisha katika kituo kile ili tuone hakuna tatizo tena la wafanyakazi. Hilo ni tatizo ambalo tunalifahamu na mara nyingi tulikuwa tunajaribu kuli-*solve* kwa kupeleka mmoja mmoja, lakini mara hii tukiajiri tunategemea kukamilisha wafanyakazi pale ili tatizo hili liondokane, na sio katika kituo hicho cha Ukongoroni tuu, ni katika vituo vingi vya afya katika Zanzibar hii Unguja na Pemba. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 11

Hatma ya Wananchi Waliosaidia Kufichua Mashamba ya Mikarafuu

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Kny: Mhe. Bahati Khamis Kombo) – Aliuliza:

Serikali inastahiki pongezi kwa hatua ambazo imechukua kwa kushirikiana na wananchi kufichua mikarafuu ambayo ilikuwa haijulikani na kwa msaada wao tumeweza kufarajika na kupata mapato ambayo ni makubwa sana.

Jee, serikali imewafikiria nini wananchi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakiri kwamba mwaka huu wizara yangu imepata mashirikiano makubwa kutoka kwa wananchi ya kuyafichua mashamba 390 ya eka ambayo yalikuwa yamefichwa na kuiwezesha serikali kuyakodisha na kuipatia mapato.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kuwapongeza wananchi wote waliojitokeza kutoa taarifa na hatimaye kuyafichua mashamba hayo kwa vile kitendo walichokifanya ni cha ujasiri na cha uzalendo wa kuipenda nchi yao. Aidha, serikali imewapa kipaumbele katika kukodisha mashamba hayo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana pia swali hili lilileta manung'uniko makubwa kwa wananchi lakini namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein katika ziara zake alilitolea ufafanuzi lakini naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a. Je, kwasababu mashamba haya yalikodishwa na pesa za mashamba haya zililipwa *cash*, ni sababu zipi zilizofanya mpaka leo wale ambao wanahudumikia mashamba yale hawajalipwa kifuta jasho chao.

b. Pamoja na matatizo yaliyojitokeza, wizara imepanga mikakati gani na kutoa elimu gani kwa wale wenye

mashamba, ili tatizo hili lisijitokeze tena huko mbele tunakokwenda.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

a. Mhe. Spika, taratibu za ulipaji kwa upande wa Wizara ya Kilimo tayari tumeshaziwasilisha katika Wizara ya Fedha na Mipango, ilichobakia ni Wizara ya Fedha na Mipango kukamilisha na kuhakiki wale watu na kuwalipa fedha zao.
b. Hili tunajitahidi kutoa taaluma kwa wale wote ambao wanamiliki mashamba na wale ambao waliokuwa wanayashughulikia mashamba haya, na vilevile bado serikali haitaacha kuwapa kipaumbele wale ambao waliokuwa wanayashughulikia mashamba haya na kuwapatia ile fidia yao ya mashamba. Ahsante sana.

Nam. 24

Kituo cha Kuwaweka na Kuwakuza Samaki Wadogo Wadogo

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ilisema itaanzisha Kituo cha Kuwaweka na Kuwakuza Vifaranga vya Samaki, Kaa na Majongoo kabla ya kusambazwa kwa wafugaji kwa upande wa Pemba.

(a) Je, hatua hiyo imefikia wapi.

(b) Ni wafugaji wangapi waliopata vifaranga hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, uanzishaji wa kituo cha kupokelea na kusambaza vifaranga vya samaki huko Pemba umefikia hatua nzuri ya maandalizi. Timu ya wataalam kutoka Wizara ya Kilimo, wakishirikiana na mtaalam kutoka Shirika la Chakula Duniani (*FAO*) wamefanya uchunguzi na kuainisha eneo la Pujini na matayarisho ya gharama za ujenzi na kutafuta mkandarasi zinaendelea.

(b) Mhe. Spika, uzalishaji wa vifaranga kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi (wafugaji) bado haujaanza, ingawa majaribio ya uzalishaji wa samaki, kaa na majongoo yanaendelea vizuri huko eneo la Beit-el-Ras. Aidha, Kituo cha Uzalishaji Vifaranga cha Beit-el-Raas kiko katika hatua za mwisho za ujenzi na kinategemewa kumalizika na kukabidhiwa serikalini kabla ya mwezi wa Januari, 2018.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwakuwa adhma ya kuzalisha vifaranga ilipangwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018, na kwakuwa matayarisho yanaendelea kusuasua yakupatikana vifaranga hivyo. Jee, Mhe. Naibu Waziri azma yake hii ataitekeleza katika mwaka huu wa bajeti.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Katika jibu langu mama nimesema vifaranga tayari vinazalishwa lakini bado hatujaanza

kwasababu tunatengeneza lile eneo la Pemba. Kwahiyo, namuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba hili litawezekana kwenye bajeti hii ambayo tuko nayo sasa hivi kuweza kulikamilisha ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa vile ni swali la uvuvi na mimi nimeguswa kwani na mimi ni mvuvi. Mhe. Spika, katika jimbo langu hususan wananchi wa Ndagoni, Michungwani na Wesha wengi wanategemea uvuvi kwenye masuala ya ufugaji kaa na majongoo. Jee, ni lini watapata taaluma ili kuhakikisha kwamba mradi huu ukija waweze kufuga majongoo kama walivyokusudia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Taaluma na kila kitu tunavitoa, labda Mhe. Mjumbe nimwambie kwamba siku ambayo tunakuja na wataalamu wetu na yeye tunamuomba awepo, ili ahakikishe taaluma hiyo tunavyoitoa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Spika, na mimi pia nishukuru kwa Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali yake vizuri lakini na mimi niongezee kuulizia juu ya swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi naulizia kuhusu ufugaji wa vifaranga kwasababu wizara hii ilizungumzia ukuzaji wa vifaranga mpaka vifaranga vya pweza. Hivyo sijui wamefikia wapi katika ukuzaji huu ili na sisi tupate faida angalau tujuwe kama wizara ina mpango mkubwa huu wa ufugaji wa pweza nataka majibu ili na mimi nipate ufafanuzi kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Hili ni suala ambalo tumevishauri vijiji kufunga sio kufuga, kufunga pweza kwa

kipindi fulani. Kwa mfano, kama tuseme unafunga wale pweza huvui kwa muda wa miezi mitatu, ili tunawapa muda wale pweza kuweza kupata angalau kimo, kwasababu Sheria yetu ya Uvuvi unapomvua pweza chini ya ule umri wake basi tunaweza tukakushtaki. Kwahivyo, tulivishauri vijiji wafunge, ili tuweze kupata pweza mkubwa na vile vile katika kuwahamaisha hili tukatoa ahadi kwamba kile kijiji ambacho kitafaidika na kuvua pweza mkubwa kabisa basi tutamzawadia zawadi, ili kuweza kupata ule uzito wa pweza na kuongezeka thamani ya pweza. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Nam. 25

Uvamizi wa Ujenzi wa Maeneo ya Kihistoria

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Katika malengo ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ya mwaka 2017/2018 ni uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria. Hatahivyo, kuna baadhi ya maeneo mengi ya kihistoria yamevamiwa kwa ujenzi ikiwemo Unguja Ukuu.

(a) Jee, wizara suala hili inalifahamu.

(b) Jee, wizara itachukuwa hatua gani kwa wale waliovamia maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika ahsante sana, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kutukutanisha hapa tena katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali langu kwanza naomba nichukue fursa hii niipongeze timu ya *Zanzibar Heroes* kwa mwanzo wake mzuri, lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi tuwaombee dua na mechi ambayo wataendelea nayo leo na ndugu zao wa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake lake Nam. 25 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli wizara inafahamu suala hili la uvamizi wa maeneo ya kihistoria.

(b) Wizara ina mpango wa kuwaondosha wale wote waliovamia maeneo yetu ya kihistoria na imeshawaandikia barua baadhi yao. Ahsante.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa sehemu ya Unguja Ukuu tumeitembelea na tumeona hali mbaya ya uvamizi. Je, wizara yake ina mpango gani maalum wa kuchukua, kwasababu waliovamia ni wengi. Hivyo, ina mpango gani wa kuchukua, ili kuona wavamizi wale mara moja wanaondoshwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika ahsante sana. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika eneo la Unguja Ukuu limevamiwa sana na nakiri kwamba tumetembea na kamati, hatua ambazo tumezichukua kwa sehemu ile, kuna baadhi yao pale tulishawaandikia barua, lakini wengine kesi zao ziko mahakamani tunasubiri uwamuzi wa mahakama. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja kama ifuatavyo. Mhe. Spika, maeneo ya makumbusho ya kihistoria yako chini ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na yamekuwa yanatembelewa sana na watalii, lakini maeneo mengi kama Maruhubi, Kijichi, Mtoni na Kihinani yamevurugika kwasababu hayana usimamizi mzuri na kwa muda mrefu sasa serikali imeshindwa kuweka Mkurugenzi wa Idara hii.

a. Je, ni jambo gani linalosababisha kutokuwa na mkurugenzi kwa zaidi ya miaka miwili katika idara hii.

b. Je, huu si mpango tu kwa wizara kutaka mambo waendeshe wao kutoka wizarani badala ya wakurugenzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika ahsante sana, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba ni kweli maeneo yale ni ya kiutalii kwa upande wa kihistoria hasa ukizingatia nchi yetu ya Zanzibar ni maeneo ya kihistoria. Mhe. Spika, lakini naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, suala la kuteua mkuu wa idara ile kushughulikia mambo ya kihistoria ni jukumu la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hiyo, yeye Mhe. Rais bado hajateua na sisi hatuna uwezo wa kuteua mtu ambaye atashughulikia idara ile, pale uteuzi wa Mhe. Rais

atakapomteua ataona kwamba maeneo yale kawekwa mtu na anashughulikiwa na bado yanaleta uhalisia wake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsate kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza, lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mwanana sana. Lakini Mhe. Naibu Waziri swali la leo hasa linahusu uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria, maana yake ndio hayo makumbusho yetu. Baadhi ya makumbusho yetu katika visiwa vya Unguja na Pemba yako katika hali mbaya na ni hali ya kusikitisha kiasi kwamba tunakosa ule mvuto kwa watalii wanaotembelea. Swali langu lipo hapa.

(a) Jee, wizara yake ina mpango gani wa dharura wa kuokoa makumbusho yetu haya.

(b) Kwakuwa bajeti ya mwaka 2017/2018 tulipitisha fedha kwa ajili ya kuendeleza makumbusho, fedha hizi zimeshaanza kutumika kwa ajili ya programu ya makumbusho hayo ili katika sura ya kuyaendeleza. Kama wameshaanza kutumia ni kiasi gani ambacho kimetumika kwa sasa. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza kwa pamoja lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza nakiri kwamba ni kweli maeneo yale ya kihistoria kwa Unguja na Pemba hayaridhishi kiuhalisia wake. Lakini napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi.

(a) Wizara hivisasa imo katika mpango wa kuyaendeleza maeneo yale na kurejesha uhalisia wake, ili tuone kwamba watalii

wanapokuja wanavutika na makumbusho yetu, kwa kuwa makumbusho yale ndio yanayoingiza pato kubwa la taifa pia tutahakikisha kwamba tumelisimamia hili na uhalisia wake umerejea.

(b) Fedha ambazo zimeingizwa hivisasa tayari zimeshaanza kutumika, tumeanza kukarabati maeneo mbali mbali ya kihistoria yakiwemo Unguja Ukuu na kadhalika. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako. Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha kuna tangazo la mgeni ni mgeni wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chaani. Mgeni mwenyewe ni Ndugu Ramy Waheed Hammam ambaye tunamuona hapo juu. Huyu ni Meneja Mkuu wa *Double Tree*, Nungwi ni Raia wa Misri. *Welcome to the House of Representatives*. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo Mhe. Mohamed Said Mohamed nimekuona kama una jambo kidogo lete.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 42 kuweka hoja ya dharura kuhusiana na barabara ya Michenzani, lakini nilikuwa sitaki tuweze kuijadili au sitaki tuweze kuweka kando kanuni hiyo. Sasa jambo langu hili kuwa barabara hii ipo katikati ya mji wetu wa Zanzibar, ndio kati ya inayoleta haiba nzuri. Vilevile, inasumbua sana wananchi kwa kipindi hiki, nilitaka serikali ilichukue au kama kuna maelezo madogo ituambie ili tuone basi jinsi gani barabara hiyo inaweza kutengenezwa kwa haraka zaidi. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, suala ulilolileta ni kweli la muhimu kwa sababu sote tunapita tunapaona palivyo, lakini vizuri ni kwamba serikali imeshasikia

watalichukua hili kwa sababu waziri muhusika hapa simuoni. Aaa! Kuna majibu naona kutoka serikalini, ahsante Mhe. Waziri kwa majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimshukuru Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa hoja yake hii aliyoileta katika kiti chako Mhe. Spika. Sisi kwa upande wa serikali tumeiona kadhia ile kwa wananchi na tulianza kuifanyia kazi, lakini kutokana na hali ya mvua tukasimamisha kidogo. Msingi wetu mkubwa nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe na Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla kwamba serikali itaendelea kulifanyia kazi eneo lile, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi na iwe barabara nzuri inayopitika wakati wote bila ya kuleta usumbufu wowote. Naomba tuvute subira kwa sababu ya hali halisi ya mvua zinazoendelea, tutahakikisha tunalipokea jambo hilo na kulifanyia kazi kwa umakini wake, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti, ili aje achukue nafasi na tuweze kuendelea. Mwenyekiti karibu sana.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanzibar ya Mwaka 2017

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba niwasilishe Mswada wa Sheria ya

Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unaandika historia nyengine katika jitihada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, katika kujenga maisha ya wananchi yaendelee kuwa mazuri katika kuangalia kipato chao na maendeleo yao ya ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unaandaa sheria ya kuanzisha chombo ambacho ni wakala wenye jukumu la kushughulikia maendeleo na usimamizi wa viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umekuja na utatupelekea kuwa na wazo, serikali kuwa na wazo la uundwaji wa wakala baada ya kuangalia changamoto zilizopata Sekta ya Viwanda katika kipindi hiki ikiwemo kwanza mapungufu mbalimbali. Kwahiyo, mapendekezo ya kuondoa mapungufu yaliopo, kuongeza ukuwaji wa huduma za viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati.

Mhe. Mwenyekiti, pili kushajihisha matumizi ya teknolojia inayofaa katika uzalishaji katika viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati.

Tatu, kuwawezesha wazalishaji kuwa na mazingira bora baada ya kuona changamoto katika hilo. Kwahiyo, kuwa na mazingira bora kwa uzalishaji ikiwa kwa ajili ya upatikanaji wa bidhaa salama na zenye ubora unaokubalika. Wakala itakayoanzishwa katika kutekeleza malengo yake kwa ujumla itafaya kazi za ushauri, kuendeleza kuratibu, kushajihisha na kusaidia kwa kina kwa kila linalowezekana katika shughuli za viwanda vidogo vodogo, vidogo na vya kati hapa Zanzibar, kuanzia na uwezeshaji katika

hatua za awali za kuzirasimisha shughuli za viwanda, pia masuala ya masoko na bidhaa hadi kufikia kuwa viwanda vikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umegawika katika sehemu sita.

Sehemu ya Kwanza imejumlisha masuala ya jina fupi la sheria na njia za kutumika kwake na ufafanuzi wa maneno mbalimbali;

Sehemu ya Pili inaelezea uanzishwaji wa wakala, kazi na uwezo wa wakala;

Sehemu ya Tatu inaelezea uhusiano na uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, majukumu yake, wafanyakazi, Bodi ya Wakurugenzi, Katibu na wote watakaokuwa wanaendesha na kusimamia wakala hii. Vile vile uwezo wa kifedha, marufuku mbalimbali ambazo zimewekwa, ili ziweze kufanya kazi nzuri kwa mujibu wa sheria na taratibu za serikali;

Sehemu ya Nne inaelezea kuhusu Mfuko wa Maendeleo ambao ni kitu muhimu kilichopendekezwa juu ya kuendeleza viwanda na usimamizi wake na matumizi ya fedha na utaratibu mzima kuhusu masuala ya fedha ya Mfuko huu;

Sehemu ya Tano imejumuisha bajeti ya mwaka, masuala ya fedha ya bajeti na mambo mengine ya ziada kuhusu ukaguzi, yote yanayohusu masuala ya fedha na utaratibu wa kuweza kutumia fedha kwa mujibu wa sheria na taratibu za serikali na

Sehemu ya Sita inaelezea uwezo wa waziri katika kutoa maelekezo mbali mbali na kutoa kanuni zinazowezesha viwanda hivi kufanya kazi vizuri na adhabu na makosa mbali mbali yatakayofanywa, adhabu zake na kinga zilizotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema naomba kuwasilisha Mswada huu na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, sasa naomba nimuite Mwenyekiti aweze kuwasilisha maoni yao.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria wa kuanzisha Wakala wa maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar pamoja na kuwezesha ushajihishaji, uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* aliyetujaalia uzima na afya njema na tukaendelea na majukumu yetu katika Baraza letu hili la Wawakilishi. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie ufasaha katika uwasilishaji wa hotuba hii na atupe usikivu na uelewa, ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa makini mswada huu ulioko mbele yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Aidha, napenda kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako hili niwasilishe maoni ya Kamati yetu hii ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa nichukue fursa hii kumshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein (Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi), kwa ujasiri wake katika jukumu zima la kuongoza nchi yetu sambamba na jitihada anazozichukua katika kuendeleza sekta ya viwanda na sekta nyengine hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa shukurani za dhari kwa Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa kutarazaki na ushauri anaompatia Mhe. Rais katika mambo mbali mbali kwa ustawi wa nchi yetu na watu wake. Kadhalika tunamshukuru Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa kusimamia vyema shughuli za Baraza hili ikiwa ni kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Balozi, Amina Salum Ali na timu yake ya watalaam kwa mashirikiano yao waliyoipatia kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya mswada huu.

Kadhalika, napenda kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sikuwatendea haki iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi nzito waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada huu ulioletwa mbele yetu kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Naomba sasa niwataje Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwenyekiti

2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
5.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
6.	Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, katika uchambuzi wa mswada huu, Kamati yangu haikusita kufanya kazi bega kwa bega na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi. Naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:

1.	Ndg. Asma Ali Kassim	Katibu
2.	Ndg. Said Khamis Ramadhan	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, fasili ya (6) ya kanuni ya 83 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016 inaipa uwezo kamati yetu kuwaalika wadau mbali mbali kila inapotokea shughuli ya kujadili miswada ya sheria. Hivyo, Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo iliwaalika wadau wafuatao, ili kutoa maoni yao juu ya mswada uliopo mbele yetu.

Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Wakulima Zanzibar *(Zanzibar National Chamber of Commerce, Industries and Agriculture)*
Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu *(Zanzibar University)*
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)* pamoja na
Aids Bussiness Collisions Zanzibar (ABCZ)

Kamati inathamini sana mchango mkubwa wa wadau hao na tunawashukuru kwa maoni na ushauri mzuri uliotuwezesha kuwa na mawanda mapana ya kuufahamu mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuleta mswada huu katika wakati muafaka ambapo nchi yetu imo kwenye mageuzi makubwa ya kiuchumi kutoka uchumi wa kutegemea kilimo hadi uchumi wa viwanda. Ni matumaini yetu kwamba uanzishwaji na ushajihishaji wa viwanda vidogo vodogo, vidogo na vya kati nchini utawawezesha wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo kupiga hatua zaidi za uzalishaji na kupata masoko ya ndani na ya nje ya nchi chini ya usimamizi wa wakala utakaoanzishwa na sheria hii. Hatua hii ni muhimu sana kwani uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo ni chachu ya kuzalisha ajira kwa vijana na kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa ukuwaji wa uchumi wa nchi unategemea sana sekta ya viwanda kwa asilimia kubwa. Zanzibar hatuwezi kukwepa ukweli huu na hata Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein alisisitiza hili katika hotuba ya uzinduzi wa Baraza la Tisa la Baraza la Wawakilishi mnamo tarehe 5 April, 2016 na hapa namnukuu.

“Katika nyakati mbali mbali nilieleza juhudi na mipango yetu ya kuendeleza viwanda hasa viwanda vya kusindika samaki, mazao

ya kilimo na mifugo, viwanda vya ushoni na viwanda vyengine vidogo vidogo.” Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein ana dhamira njema ya kuirejesha Zanzibar ya viwanda kama ilivyokuwa zamani. Kuletwa kwa mswada huu mbele ya Baraza lako hili Mhe. Mwenyekiti, ni hatua ya mwanzo ya nchi yetu kuelekea kwenye uchumi wa viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unaweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wawekezaji na wajasiriamali wa ndani na nje ili kuwekeza katika sekta ya viwanda. Ni dhahiri kuwa, kupitia mswada huu kutaifanya Zanzibar kufungua milango na fursa za kuinua uchumi wetu na kupelekea Pato la Taifa *(GDP)* kuongezeka maradufu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara iwe makini zaidi ili dosari zilizojitokeza nyuma za kufubaza viwanda vyetu hapa nchini zisijirudie tena. Sambamba na hilo, wizara ijitahidi katika kuweka mazingira bora zaidi kwa bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda hivi vya ndani kwa kuweka vikwazo kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi.

Uwekaji wa vikwazo hivi *(Trade and Non Trade Barriers)* vitasaidia sana kuimarika kwa viwanda vyetu vya ndani na kupata soko kubwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha, kamati yetu inashauri Serikali zote mbili zikae pamoja ili kutatua baadhi ya changamoto za kisheria ili bidhaa zinazozalishwa Zanzibar ziweze kuingia katika soko la Tanzania Bara, soko la Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi, Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na mswada huu

pamoja na marekebisho madogo madogo tuliyoyapendekeza wakati tulipokaa na wizara kwa nia ya kujenga mswada huu. Marekebisho hayo yamegawika katika sehemu mbali mbali zikiwemo makosa ya kiuandishi, makosa katika uteuzi wa maneno na kuingiza baadhi ya vifungu vipya ili kujenga zaidi misingi ya viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati kwa ajili ya kuwainua wazalishaji wadogo wadogo na wa kati na kuongeza pato la Taifa *(GDP).*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 kifungu kidogo cha (2) kamati imependekeza kwamba kiandikwe upya, ili kiwiane na kile kilichomo katika mswada wa Kingereza na kisomeke kama ifuatavyo:

“Ukiacha wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa bodi watatumikia nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia siku ya uteuzi na wanaweza kuwa na sifa ya kuteuliwa tena”.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pia imependekeza kuongezwa kwa kifungu chengine cha 7, paragraph (q) na kisomeke kama ifuatavyo:

“Kupendekeza kwa Waziri vivutio vitakavyoshajihisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati pamoja na kupendekeza mbinu muafaka za kulinda viwanda hivyo.”

Halikadhalika, kifungu cha 9 kamati imependekeza kuongezwa paragrafu ya 9(e) inayosomeka kama ifuatavyo:

“Atakabiliana na kila tatizo ambalo linaonekana ndio kikwazo kwa maendeleo ya viwanda kwa idhini ya bodi.”

Pia kifungu cha 8(2) kamati imependekeza kifutwe na kiandikwe upya na kisomeke kama ifuatavyo:

“Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa:”

Kwa ajili ya kuainisha sifa za Mkurugenzi Mkuu kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imebaini makosa madogo madogo ya kisarufi na vile vile migongano baina ya mswada wa Kiswahili na ule wa Kingereza na marekebisho hayo tumeyaweka katika waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambao Waheshimiwa Wajumbe wamepatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nichukue fursa hii kwa kupitia sheria hii sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi tuwe wa mwanzo kuwekeza katika suala la viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati ili tuwe mfano wa kuigwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa utulivu wenu na naomba tuuchangie, tuujadili na hatimaye tuupitishe mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe tunaanza kuujadili mswada huo na mtu wa kwanza atakuwa Mhe. Ali Suleiman Ali akifuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi. Mhe. Ali Suleiman Ali karibu sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama

hapa kuweza kutoa michango yangu juu ya Mswada huu wa Sheria muhimu juu ya masuala ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na wataalam wake wote kwa kukaa na kufikiria juu ya hatima ya nchi yetu, hasa sasa hivi tukiangalia kwamba vijana wetu wengi wanategemea ajira katika sehemu mbali mbali. Tunaamini kwamba kama viwanda vyetu vitasimamiwa vyema na ushauri mzuri wakapewa watu wetu hawa ambao watakuwa na viwanda watu binafsi, basi vijana wetu wengi watabahatika kupata ajira na kuendesha maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika moja kubwa ninalotaka kulizungumza huwezi kufanya jambo lolote bila ya kujijua unatoka wapi, uko wapi na unakwenda wapi. Kwa bahati nzuri Zanzibar tulikuwa na viwanda vingi, serikali ilijitahidi baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ilirithi viwanda. Tulikuwa na viwanda vyetu vya mafuta ya nazi ambayo yalikuwa yanasafirishwa nje Tanzania Bara mpaka Kenya kama sikosei na wananchi wengi walifaidika na kuendesha maisha yao pamoja na waliokuwa wanafanya huduma hizo.

Lakini kwa wakati huo serikali ilirithi Kiwanda cha Soda potelo ambapo watoto wetu wadogo tuliowazaa hata ukiwaambia hawajui tena, kama itakuwa imewekwa katika kumbukumbu ya historia basi wanaweza kuoneshwa tu hii ndio soda ya aina ya potelo. Lakini bahati mbaya tulikwenda kutoka mwaka 1964 mpaka 1970 mambo hayo yakatoweka kabisa hapa kwetu yakawa hayapo. Kwakweli, wananchi wengi walipata ajira na walifaidika katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, mwanzo wa kufa viwanda hivi vya serikali kwanza ilikuwa uaminifu hakuna au ulikuwa mdogo, changamoto kubwa iliyoleta maafa ya viwanda hivyo ni kwasababu ulikuwa

ukiingia katika Kiwanda cha Mafuta ya Nazi ukitoka unavaa kanzu kama shekhe. Ile kanzu umeivaa kama bomu Mwenyezi Mungu atunusuru umetia chupa zako za mafuta ya nazi kama nne ndani ya kanzu unatoka hata kama ukiwa mwembamba utakuwa mnene watu wanakustaajabia. Lakini kutokuwa na uangalifu na umadhubuti, basi ilibidi unatoka mlangoni hata huulizwi sasa ile ilikuwa ni njama moja. Kwahivyo, viwanda vyetu vilikufa na kuleta athari kubwa kwa jamii yetu. Kwanza serikali ilikosa mapato, lakini pili serikali yetu ilipoteza ajira kwa wananchi wetu wengi sana wa Zanzibar Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, jengine serikali katika jitihada zake za kuendeleza viwanda ilijenga Kiwanda cha Viatu Mtoni, ikajenga Kiwanda cha Sigara Maruhubi. Pia ilithubutu kujenga viwanda vidogo vidogo vingi ambavyo mpaka leo jina hilo lipo linaendelea Viwanda Vidogo Vidogo. Mhe. Mwenyekiti, viwanda vile tulishuhudia akinamama, akinababa na vijana wengi sana wamo ndani mle wanapata ajira. Lakini bahati mbaya halikadhalika viwanda hivyo vilipoteza uhai wake kimoja baada ya kingine.

Mhe. Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo tulishuhudia kama sikosei mpaka Wairan walikuwepo pale wanauza vitu mbalimbali. Ukenda leo unaingia pale unatoka na kitu cha thamani unachotaka, lakini leo imebakia historia tu viwanda vile utasikia kuna viwanda vya kaseti sijui vya nini vilivyobakia, lakini yale madhumuni hasa hayapo. Kwahiyo, vijana wetu wamepoteza ajira tena wengi kupindukia kiwango.

Lakini, serikali kwa wito wake kuanzia viwanda vya binafsi pia ilitoa wito ikaanzisha viwanda vya *COTEX* ambavyo vilikuwa vinazalisha vitambaa, Kiwanda cha Magodoro *Banco* vyote Maruhubi kwa Mhe. Machano Othman Said wakati huo. Viwanda vyote hivyo vilikufa kimoja baada ya chengine.

Mhe. Mwenyekiti, watu walikuwa wanashuhudia kiwanda kinazalisha humu ndani unakuta magodoro yanafika juu huku lakini watu wanajipanga utafikiri kama wanacheza sarakasi, wanachukua godoro moja baada ya jengine wanarusha kwa nyuma ili kuiba. Pia vitambaa vilikuwa vinaibiwa kupindukia kiwango. Viwanda hivyo vyote vilikufa. Bahati nzuri tumebakiwa na viwanda vyetu viwili ambavyo serikali naiomba sana tuviangalie na tuvishike kweli kweli Kiwanda cha Sukari Mahonda japo kimo katika mikono ya ubia, lakini na Kiwanda cha Makonyo Wawi Pemba. Viwanda vyetu hivi bado tunasema kwamba serikali yetu inavidhibiti na inaendelea vizuri katika usimamizi kutokana na juhudi ambazo zimepangwa, ili kuendeleza maisha ya viwanda vyetu na faida ya nchi yetu kwa mapato yake.

Mhe. Mwenyekiti, wazo langu katika mswada huu naiomba sana serikali mswada huu ni mzuri sana kwanza tunataka ajira kwa vijana wetu, pia tunataka ajira kwa jamii yetu mbalimbali. Kuna viwanda vidogo vidogo tunaanza milioni 11, lakini kuna viwanda vya kati vitafika mpaka milioni 600 na ngapi sijui huku chini. Hiyo yote ni dhana nzima tuhakikishe kwamba vijana wetu wanapata ajira katika kuendesha viwanda hivi.

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu kwa Mhe. Waziri pamoja na wataalam wake, la mwanzo kabla ya yote taaluma ni muhimu kuliko yote. Tujue madhumuni kwamba kiwanda maana yake ni kuzalisha na kuuza. Kwahivyo, mambo mawili haya yakenda vizuri ukizalisha utauza, basi viwanda vyetu vitasimama vizuri na vitaendesha biashara yake na faida kupatikana katika serikali na wao mpaka waajiriwa. Lakini uaminifu katika uendeshaji au waajiriwa naiomba sana wizara iwasimamie sana vijana wetu au wawekezaji wetu wenye viwanda vidogo vidogo na vya kati, juu ya kuhakikisha kwamba taaluma unaajiriwa pahala kwa maslahi

ya kiwanda, maslahi ya serikali na wewe unayefanya kazi pale. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, tutakuja hapa hakuna kitu.

Kwa hivyo, sheria hii nasema ni nzuri na sheria imelenga kuhakikisha kwamba viwanda umefika wakati wa ushindani wa viwanda katika nchi zetu za Afrika Mashariki. Mhe. Mwenyekiti, leo Tanzania Bara ukitaka chochote kipo tayari. Tumekwenda kutembelea juzi Tanga tumekuta ushindani wa biashara ya saruji. Mkoa wa Tanga peke yake pale tulipofika sisi kuna viwanda vitatu, *Tanga Cement* na vyenginevyo, ni ushindani mkubwa. Lakini pamoja na ushindani huo kila mmoja ana soko lake kutokana na ubora wake. Kwahivyo, bidhaa ikiwa nzuri utauza wala humuogopi mwenzako, lakini bidhaa ikiwa haina ubora huiyuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na kuleta sheria hii nzuri ya kuanzisha Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati, lakini kubwa kwanza kujua tu uzalishaji uwe bora upate kuuza soko la nje. Uzalishaji ukiwa sio bora hutouza biashara hiyo baada ya siku mbili tatu utaona kiwanda kinadidimia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, kuna uzalishaji wa viwanda vyetu vingi vya matofali, ni ajira, lakini ubora sasa. Unaweza kukuta mtu ana biwi lake la matofali hayana hesabu hayanunuliwi kutokana na ubora haupo. Mfuko mmoja wa saruji mtu anatoa matofali 80 au 100. Kuna mwengine anakwambia mimi natoa 40 au 38 haya yatanunuliwa yaondoke yule yanabakia pale pale. Kwahivyo, pawe na viwango, ufuatiliaji na wala tusiseme tu kwamba aah! Wapiga matofali wale wana hiari yao hapana, kwasababu wanatumia nguvu zao, yule anayenunua naye anataka aishi maisha marefu katika ujenzi wake. Kwahiyo, pawe na chombo cha kusimamia ili kuhakikisha kwamba ubora wa bidhaa uchukuliwe umuhimu, vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti hatufiki.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna viwanda vingi hata viwanda vya *furniture* hivi. Viwanda vya *Furniture* viko vingi na vijana wetu wanapata ajira. Hivyo ni vyema tuangalie kila siku nasema sina imani na wanaokata minazi katika nchi yetu na minazi imeangamia katika nchi yetu haipo, ndio maana zao la mafuta ya nazi limepotea. Leo tunategemea kununua nazi kutoka Tanga kuja hapa, ni aibu katika nchi yetu wakati Zanzibar ilikuwa inasafirisha Bara na kwengineko, inapeleka mbata zinasafirishwa zinakwenda nje, lakini leo hazipo. Watoto wetu wadogo ukiwaambia kuna tanuri ya mbata hawajui ni aibu. Kwahiyo, niiombe sana serikali pamoja na juhudi zetu za kuhakikisha kwamba viwanda vinaletwa lakini viwekewe sheria ngumu yaani, sheria ya kuleta manufaa kwa nchi yetu, pia na malighafi yetu isipotee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo nazi. Kuna wenzetu hapa lakini leo naona wale wenzetu wakike wengi hawapo, walikwenda kutafuta makapu ya kutafuta nazi kutoka Tanga kuja hapa, nikawaambia nyinyi vipi. Wakaniambia aah! Mheshimiwa, lakini najua kinamama wakienda lazima wapate zawadi waje nayo nyumbani. Wananunua nazi ndani ya makapu wanaleta Unguja, jambo la aibu.

Kwahiyo, niiombe sana serikali, naridhika na viwanda naiunga mkono sana serikali. Lakini tusimamie uwadilifu, uangalifu na tusimamie rasilimali yetu isipotee. Mhe. Mwenyekiti, leo niseme tu kwamba kwa mfano kama unataka kitu kizuri na unakisimamia vizuri basi kitakuwa, lakini ukisema tu kwamba aah! Mimi hii naiondoa njiani tu uta-*fail* njiani.

Kwakweli, niseme tu Mhe. Mwenyekiti, azma ya mswada huu ni mzuri na umekuja wakati unaofaa, hasa tukiangalia vijana wetu wengi hawana ajira na ajira yao ni ya kwenda hapa na pale, ili wapate maendeleo madogo madogo.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo nataka nilizungumze hapa, ni kwenda kujifunza kwa wenzetu, japo muda utakuwa haupo maana sheria inapitishwa lakini sio vibaya. Hao wataalamu, au wajumbe wa bodi sijui nani watakaochaguliwa, kuna wataalamu wetu wazuri tu anaokwenda nao Mhe. Waziri. Waende kwa wenzetu wakaangalie, je tukilifanya hili na nyinyi mnafanya hivi je, kiwango gani tukiweke ili tupate masoko ya Bara. Kwakweli, biashara ya Unguja na Pemba inategemea soko la Bara. Sasa pawe na ushindani mzuri na usimamizi mzuri, ili baada ya muda mfupi vijana wetu na wafanyabiashara wetu wasije kulalamika njiani wakasema aah! Sisi hivi sasa tumeshindwa bwana biashara haziendi kumbe ubora haupo.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti naunga mkono mswada huu na ninasema kwamba namuomba sana Mhe. Waziri aangalie vyema na awe mwangalifu na watendaji wake juu ya hivi viwanda vinavyotaka kuanzishwa, kwasababu viwanda hivi vinaitwa vidogo vidogo vitakuwa na watu 9, 60 au 100. Lakini nataka twende kwenye hivyo viwanda vya kati vifikie angalau watu 200, 250 na zaidi ili vijana wetu wapate ajira, kwasababu tunaamini kwamba, ili tuendelee tunahitaji viwanda, na viwanda hivyo vitupe manufaa kwa ajili ya mambo mazuri.

Jambo la mwisho Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba pamoja na yote niliyochangia. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ndio wizara mama na ndio wizara tunayoitegemea. Kwahivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, wenzetu Tanzania Bara wana maeneo wanapanda miti, na kila kitu. Lakini na sisi kwa hapa kwetu ardhi yetu inaturuhusu kupanda minazi na mikarafuu. Hivyo, atowe wito zaidi kwasababu ndio moja katika sekta ya biashara, tuhakikishe kwamba minazi inaongezwa kwenye maeneo mbalimbali na kila mwenye eneo aseme tu kwamba imefika wakati hivi sasa hivi

nataka kupanda minazi, kwa sababu tukifanya vyengine vyovyote ndio inapotea iliyokuwepo tunaharibikiwa.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, niseme naunga mkono na pia naipongeza kamati yetu inayohusika na wizara hii kwa kuleta marekebisho mazuri juu ya maendeleo ya shughuli zetu hizi. Baada ya hayo machache niseme tu Mhe. Mwenyekiti, nauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja sina tatizo ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Suleiman. Sasa namwita Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baadae akifuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo. Mhe. Dkt. Makame Ali karibu sana.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji wa mada hii adhimu ya maendeleo ya viwanda.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri Biashara, Viwanda na Masoko Balozi Amina Salum kwa kuvikumbuka hivi viwanda na kutaka kuviingiza katika utekelezaji ambao utaleta tija. Nathubutu kusema kwamba Mhe. Waziri ni kweli kwamba ni mtu wa kimataifa, ni mwanaharakati na ni mtu ambaye kwa kweli yuko *proactive* yaani anachangamkia kikazi. Kwa maana hiyo pia ni *aggressive* kwa kutafuta, sio kwa kupigana kufanya nini lakini *aggressive* katika kutafuta maendeleo, yuko *creative* mbunifu na anatafuta fursa mbalimbali yuko *opportunity*. Kwahiyo, nakupa hongera sana Mhe. Waziri kwa juhudi zako hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nina mambo yafuatayo ambayo nitayaongelea hapa na kwasababu ya muda Mhe. Mwenyekiti ukiona muda wako nimeula sana, basi wewe nikumbushe tu mimi nitajitahidi niishie hapo nitakapofikia.

Kwanza kabisa nitazungumzia historia ya viwanda, ingawa katika maelezo tuliyopata hapa imeanzia mwaka 1976 yaani miaka 40 iliyopita. Lakini kuna historia ile ya kutoka 1964 hadi hapo 1976 haipo. Sasa tukiangalia hapo miaka 40 hiyo tunaona kwamba uzalishaji au ile *contribution* katika pato la taifa umekuwa unakwenda *zigzag* haupandi, unapanda na kushuka lakini kwa kiwango kile kile kidogo.

Kwa mfano, mwaka 1976 *contribution* ya viwanda vyetu tulivyonavyo Zanzibar ilikuwa ni asilimia 2 ya pato la taifa. Lakini mwaka 1983 ilipanda ikafika asilimia 7.9 na hapo ilikuwa ni kama kiwango cha mwisho hatukupanda tena zaidi ya hapo. Mwaka 2012 kidogo tukapanda tukafikia 7.1 na huu mwaka uliopita wa 2016 tulifikia asilimia 6.9 ya pato la taifa, tuna kazi kubwa. Namwambia Mhe. Waziri kwamba tuna kazi kubwa ya kufanya kuvifufua viwanda na sio kuvifufua tu bali kuviendesha viweze kwenda na maendeleo ya wakati.

Mhe. Mwenyekiti, tuna viwanda kwa mujibu wa takwimu hizi, tuna viwanda vidogo vidogo havipungui 2,200 ambavyo vinaajiri watu kati ya 10 na 9 chini ya watu 9 bado ni viwanda vidogo. Halafu kuna viwanda vile vinavyoajiri watu wengi.

Sasa baada ya kusema hiyo historia, ningependa niyaeleze mambo haya yafuatayo na nitayataja kwanza kabla sijayaeleza moja moja ili kuangalia wakati, tutakapofika wakati mtu atafafanua mwenyewe, hili alikusudia nini ataliendeleza.

Kwanza kabisa nitazungumzia mambo ya wakala ambapo wenzangu waligusia kwa kirefu wakala ilikuwa nisichangie hili, lakini kidogo kuna kitu nimekikumbuka kwenye mambo ya uwakala kwa hivyo nitakigusia. Pili nitazungumzia mambo muhimu yaani *philosophical issues* za *industrialization* kwa maana hiyo hiyo ya viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati.

Tatu nitazungumzia *ZRID*, nimeita *ZRID* yaani *Zanzibar Rural Industrial Develop*, nitaizungumzia kwa ufupi jinsi ambavyo labda tunaweza tukaenda tukaikuta hii sekta ya viwanda vidogo vidogo.

Halafu tena nitazungumzia pia malengo yetu. Malengo yetu je, malengo yetu ni hapa kwenye viwanda vidogo vidogo na vya kati tu au tunalenga kwengine. Halafu nikitoka hapo nitazungumzia mambo ya *handling package* na *storage* mambo ya kuhifadhi kusafirisha na kuvi-*pack.* Halafu pia nitazungumzia mambo ya *standard*, viwanda lazima viwe na *standard*, tena *standard* hii ya kimataifa, kwa sababu utazalisha kitu hapa ukiuza hapa nchini kama hakiko kimataifa basi hata wananchi wa hapa hawatanunua bidhaa zinazotengenezwa viwandani. Vilevile nitazungumzia mambo ya *ZBS* kwa ufupi tu na *TBS*, halafu tena nitakuja maeneo sasa ya viwanda hivyo tunakolenga huko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nikianza na wakala. Wakala ni uwakilishi na uwakilishi umetajwa hapa jana mwenzangu alifafanua vizuri sina haja ya kurudia kule alikofafanua kule, lakini nasema wakala huyu yuko ndani ya wizara, anawakilisha wizara kwa mambo haya ambayo yanalengwa, bila shaka atahusika na mambo ya usajili na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua kwa sababu kutakuwa kuna *revenue collect* na ndio lengo kubwa na kutakuwa na mambo mengi tu yanayohusu fedha. Sasa nilitaka kujua tu kutakujakuwa na uhusiano gani kati ya *revenue collector* yule wa *ZRB* ambayo ni mamlaka iliyokabidhiwa mambo ya kukusanya *revenue*, na huyu wakala wa wizara.

Halafu pia natakakuuliza je, kutakuwa na *contact* baina ya wizara yenyewe na chombo chake hiki cha namna ya kuendesha hii, kwa sababu sijaona mahala pengine ipo sijaona zile *vision*, zijaona

mission, sijaona *objective and goals* na kadhalika za hii. Kwahiyo, pengine zingekuwepo ningeuliza swali hili kwa namna nyengine. Lakini cha muhimu ni kwamba kutakuwa na *contract* baina ya wizara na huyu wakala juu ya namna ya kuendesha hizi shughuli za viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nikitoka hapo, hapo nimemaliza kwenye wakala. Sasa naingia kwenye mambo muhimu ya kuzingatia yaani *philosophical issues* za *industrialization*, nitazungumza kwa kifupi na pale nitakapozungumza kwa Kingereza ni mazowea yangu tu kwamba ndio nalijua kwa hivyo pengine kwa Kiswahili silijui, maana yake sote ni Waswahili lakini kinatuchenga wengine, Kingereza pia sio Waingereza basi kwa hivyo pia kitatuchenga ni *automatic* kwamba inawezekana usielewe huku wala huku.

Sasa nasema kwenye philosophical issues ya kuzingatia, yaani mambo ya kuzingatia kwenye viwanda, ni mchango wangu huo ni kwamba kwanza kabisa tuangalie sana ile *what next* ya viwanda vyenyewe, yaani hapa nina maana kwamba mwananchi anakuwa ana-*concept* gani juu ya viwanda hivi vinavyokuja, maana akikubali kwamba kiwanda fulani kifanyike. Kwahivyo, hata kama kutakuwa na kitu kitachukuliwa ili kitengenezwe kiwanda, basi hatokuwa na malalamiko makubwa kuliko vile ambavyo atakuwa ana-*miss conception*, yaani hivyo viwanda vitakuwa ni *relative* na anavikubali mwananchi au vinapelekwa tu. Kwahiyo, tuzingatie hili kwamba viwanda lazima viwe vinakubalika kwa wananchi. Naeleza kwa ufupi hapo sitaki kwenda ndani sana.

Halafu kuna jambo jengine, ambalo kwa kweli linapaswa kuzingatiwa ni hili la nguvu za siasa *political power*, yaani viwanda vyovyote vinavyojengwa nchini ni lazima vi-*support* siasa ya kimaendeleo ya nchi na siasa ya kimaendeleo ya nchi ni siasa ya CCM, kwasababu ndio Chama Tawala na ndio

kilichoweka. Sasa kiwanda chochote kinachojengwa lazima kiwe kina-*support* mwelekeo wa Chama cha Mapinduzi ambao ni mwelekeo wa maendeleo ya wananchi. Kwahiyo, hizi *political powers* lazima tuziangalie sana huko wananchi nilisema mwanzo pale wawe na *interest* ya viwanda vyenyewe ndio siasa itakwenda vizuri. Wasijewakawekewa kiwanda ambacho pengine kitaharibu siasa, kikijakuharibu siasa hicho kiwanda kitakuwa hakina maana yoyote. *(Makofi)*

Halafu tena kuna jambo jengine la *Industrialization* ni *objectivity*. Hichi kiwanda tunachokusudia kujenga kina madhumuni gani, kita *achieve goal* gani, kitaweza kuzalisha yale ambayo tunayataka, kama mwanzo nilivyosema kwa viwango vile ambavyo tunavitaka na kwa wingi ule ambao tunautaka, au itakuwa ni vile vile viwanda ambavyo havitazalisha kwa viwango na wingi unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ningependa kusema kwamba kuna kitu kinaitwa *distortion*, yaani mtu anajaribu ku-*distort* ama kwa makusudi ama kwa lengo lake jengine, ili aweze kutekeleza azma yake ya kuharibu au kutengeneza hali ya siasa. Kwahivyo, na hii nayo tujaribu kuiangalia, na hii inakuja sana kama mwenye kiwanda atatoa matangazo kuwa atazalisha kitu fulani chenye sifa fulani, lakini matokeo yake anazalisha kitu ambacho hakina sifa ile ambayo inatakiwa, au pengine hazalishi yeye anachukua nje anapenyeza anasema anazalisha yeye, wananchi wakijakujua hilo inakuwa ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo pia ningependa kulizungumzia ni hili la elimu ya viwanda, elimu ya viwanda ni lazima iwepo, yaani watu wafundishwe namna ya kuendesha viwanda kwa taaluma mbali mbali ili uzalishaji uwende na wakati. Hayo ni mambo machache kwa upande wa *philosophical issues* za kuendesha viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye ile *ZRID* yaani *Zanzibar Rural Industrial Develop.* Kama tunakwenda kwenye viwanda vidogo vidogo maana yake tunakwenda kwa wananchi, kama tunakwenda kwa wananchi sasa hiyo ni sehemu ya *rural area*, tutakuwa kwenye *rural area.*

Mhe. Mwenyekiti, sasa napendekeza mambo yafuatayo yaweze kufanyika. Kwanza hivi viwanda vidogo vidogo vinavyoanzishwa, hivi vidogo kabisa ni lazima vifanyiwe majaribio makubwa sana, ili kuona kwamba vinaweza vikaenda *sustainable*, vikaenda kwa muendelezo na sio kimekuja leo na kesho hakipo tena. Halafu sio vibaya kama tutakuwa na *demostration*, yaani aina ya viwanda fulani tukavifanyia *demostration*, wananchi wakawa wanakwenda wanaona viwanda hivyo wanaviona vinazalisha hivi na kwa *technology*, *simple technology* ambayo hata wao wanaweza wakai-*adopt* wakaweza kuendeleza viwanda hivyo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwenye mambo haya ya *Rural Industrial Development*, ni utafiti wa kutosha sana. Kuna wananchi wengine hata ukiwapelekea *technology* ya aina gani wao wataipinga, lakini wako ambao wataikubali na wataiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda wako unakaribia kumaliza. Malizia.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Nimepata nusu. Haya, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Sasa lazima tufanye utafiti. Sasa mimi niende haraka nimeishia hapo kwa sababu ni mambo ambayo yanahitaji muda.

Mhe. Mwenyekiti, malengo ya viwanda vidogo vidogo hivi tunavipenda na vya kati ni kwamba ni kuendesha tukuze uchumi

wetu. Sasa tutakwenda na hivi viwanda vidogo vidogo tu au tutakwenda mpaka tutafikia kwenye *large scale production* yaani, viwanda vikubwa vikubwa, vikiwemo vile *basic factory* ambavyo vinachukua *rawmaterials* na kuweza kuitengeneza kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo kwa vile muda haupo sasa nieleze hapa kwenye mambo ya *standard*. *Standard* nilisema mwanzo kwamba lazima kinachozalishwa kiwe kwenye *standard* ya kimataifa, mwananchi anakikubali kitu ambacho kina ubora kwa nchini hapa. Sasa kama akikiona hakina ubora bila ya shaka kitakuwa hakina soko hapa hapa nchini hatotaka anunue. Kwahivyo, hawa *ZBS* na *TBS* kwa kushirikiana kama alivyosema Mhe. Waziri jana kwamba watashirikiana na *TBS*, ili kuendesha shughuli za viwango basi nashauri sana vyombo hivi viimarishwe, ili viweze kushirikiana zaidi kupata viwango. Maana tumeona hapa kwa mfano mdogo tu hapa mafuta haya ya *petrol* …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemaliza.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Umekwisha basi Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda ulioninpa na narudia kumpongeza sana Mhe. Waziri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia ahsante sana. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa nitamuita Mhe. Abdalla Ali Kombo, na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajitayarishe. Mhe. Abdalla Ali Kombo karibu.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumsifu Mhe. Waziri wa Wizara hii na Mwenyekiti wa Kamati hii, sina tatizo na mswada naunga mkono mia kwa mia lakini nina maoni yangu tu au pengine wasi wasi wangu juu ya uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kila mtu huwa anatia nia kwa kile anachokitaka chochote uwe ubaya uwe uzuri, sasa wasi wasi wangu wa uanzishwaji wa viwanda hivi ni sawa sawa na lile basi la Wamasai ni kwamba tunafuata watu ambao walikuwa na nia ya kufanya hivi, basi la Wamasai wakiingia likifika pahala kuna wenzao mama yooo, mama yoo wapi Sadalam hakuwa na safari lakini anaingia na yeye anakwenda Sadalam. Sadalam maana yake Dar-es-Salaam kwa Wamasai hakujipanga hakufanya chochote na yeye anaingia ndani ya basi.

Sasa wenzetu Bara walijipanga kwa viwanda Dkt. John Pombe Magufuli tokea anapiga kampeni anazungumzia viwanda, ile ni niya na alikuwa anafanya hayo akijuwa pesa iko wapi, madini yako wapi, watu wako wapi, mtaji uko wapi na wapi tuanze, wasi wasi wangu kwa Zanzibar hayo mambo yote hayapo, na sisi tumeingia kwenye lile basi yoyo wapi Sadalam paa tukaingia. Sadalam kwa Kimasai ni Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwasababu hapa juzi juzi nazungumzia viwanda tumeingia kwenye *Bulk* ya *Petroleum System* hatukujua tunakwenda wapi, tukajiingiza aje mtu mmoja tu wa mafuta, matokeo yake tukapiga wiki nzima hatuna mafuta una kiwanda kiko wapi hapa, tukapewa mambo mazuri tuliwauliza juu hapo kumbe ile *amount* ya mafuta yetu hiyo meli haiwezi kufika mbali, matokezeo yake mafuta yanakwenda kuchukuliwa Kigamboni. Kwa hivyo, nina wasi wasi na hili basi. *(Makofi)*

Lakini jengine, naamini sayansi sana na ushamba wangu lakini sayansi huwa naiamini sana. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri pamoja na kamati yake wangetusaidia tu katika haya jee, kwa kiasi gani ujuzi wetu ama utaalam wetu kuhusiana na haya tumeutizama tuko wapi, *demand* ya hivyo vitu viko wapi, haya gharama *capital* ya hesabu zetu angalau tumefanya chochote tukajuwa kama wizara au serikali tunahitaji pesa kiasi gani

kuanzisha haya. Vilevile, kuna kitu wanasema *competition* ushindanishwaji wetu tuliingia ndani angalau tukachunguza chunguza, je washindanaji wetu tunawajua wa nje, hapa Unguja na Pemba, Bara na wapi tuliyafanya hayo, au tunaingia tena tu.

Sasa hivyo ndio vitu ambavyo vinanitia wasi wasi *location* tunakijenga wapi hiki kiwanda Bambi, Matemwe, Mwambe, Micheweni. Jee, bidhaa hizo hata zikifika huku mjini zimeoza hazijaoza. Mhe. Mwenyekiti, sasa nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anaweza akanisaidia tuko wapi, je kuna *standard* tumefanya utafiti wowote hizo tunazozalisha isijekuwa unauza Chwaka tu, akija mjini hiyo *product* haifai ina *standard* yoyote tumeyafanya hayo.

Hapa kuna mambo ya sheria, mikataba na taratibu leo kuna *VAT* kuna *TAX* yamezingatiwa haya katika viwanda vyetu ambavyo tunavianzisha, hapa kucha kutwa tunagombana na Tanganyika *VAT* wengine wanalipa mara mbili *TAX* iko hivi, sijui Wazanzibari tunalipishwa mara ngapi tumekaa tukaya-*consider* haya. Lakini jee, bajeti yake Mhe. Waziri inasemaje kuhusiana na haya anazo fedha ya kutosha kuja kuwasaidia hawa wanaoanzisha viwanda vidogo vidogo, ama jee kuna kasma yoyote katika wizara yake ama serikali tumeyatizama haya. *(Makofi)*

Lakini jengine kuna aina ya viwanda hata vidogo vidogo. Kwa mfano, viwanda vidogo vidogo vya nguo tu sisi kusini kofia yetu lazima iwe na viuwa, Tumbatu shuka yake lazima ining'inie, kuna wale wa Kisarawe kofia yao tunaita mguu wa charahani haina viuwa, tumeyatizama haya katika kuanzishwaji wetu wa viwanda. Hivyo vyote vinatusaidia, kuna usafiri wa kutoka huko kwenye mali ikaja aidha Zanzibar *Town* au popote kwenye kiwanda, kutoka hapa kwenda Pemba au Pemba kuja hapa, kutoka hapa kwenda Dares-Salaam na kwenda Mombasa jee, tulikaa na

tukatizama gharama zake kuna *research* yoyote ambayo imefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hayo majengo ambayo tunaita *store* vitu vyetu yapo na kama yapo yanafaa, ili kuanzisha viwanda. Jengine ambalo ni kubwa kuna *new policy* kila rais anayeshinda anayekaa madarakani anakuja na lake, tumelitizama hili, kuna nchi zinaambizana yoyote rais atakayekaa hiki kibakie hivi hivi. Sasa haya yote hizi *policy* sasa hivi na muda tuliobakia mfupi wa miaka mitatu. Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwa uzoefu Tunguu ile ilikuwa Kituo cha Maonesho nakumbuka mpaka leo kwenye utawala fulani lakini sasa hivi *university*, je haya tunayoyapanga *new government* inayokuja itaya-*consider*. *(Makofi)*

Kwahivyo, wasi wasi wangu ni huwo, hizo biashara tunazozifanya hizo hizo *taste* kila mtu ana yake hapa, huyu anataka chungu huyu tamu yamepangwa hayo. Kwa mfano, kuna biashara nyengine zinataka umri mimi na wenzangu wengine si vibaya Mzee Yahaya umri wake na wangu kuwa tafauti, atakachokitaka yeye na mimi tafauti imepanga hivi na Shehe Hamza vijana wetu hawa, kuna *set of action* nani atafanya hii bei itakuwaje *promotion* itakuwaje *marketing* itakuwaje tume-*consider* haya.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri akija atatufahamisha mambo haya yote kuna *race* sio za mbio za kabila. Kwa mfano, leo Mmasai hapa hata ungemjengea viatu vya aina yoyote yeye anataka kiatu cha mpira ndicho atakachofukuzia ng'ombe, anataka shuka la buluu na jekundu kwake yeye umemtizama mtu huyu, sasa hivi ni vitu ambavyo vitatusaidia Mhe. Mwenyekiti, lakini je hawa watu hizi pesa wanazo.

Kwahivyo, ushauri wangu tusiingie kwenye basi la Mmasai kwamba eee Sadalam hiyo, hujui linakwenda wapi, tuke tulijue

basi linakwenda wapi tunafikia wapi. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo, sasa ninamuita Mhe. Rashid Makame Shamsi akifuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Rashid karibu sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu kuweza kutoa mchango wangu juu ya Mswada tulionao mbele yetu hapa unaohusiana na masuala ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, nitangulize vile vile kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuweza kufikiria kuweza kuleta mswada huu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na mustakabala mzima wa uchumi wa visiwa vyetu.

Lakini pia nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Bisahra na Kilimo kwa uwasilishaji wake mzuri pamoja na wajumbe wake wote ambao walishirikiana, nao katika kuweza kuandaa ripoti ile muhimu ambayo, nina imani kwamba imeweza kutoa mchango mkubwa sana katika kufanikisha upitishaji wa sheria hii. Vilevile, niwapongeze pia wajumbe wenzangu ambao wamenitangulia kwa michango yao mbalimbali ambayo baadhi yake itakuwa na mimi naiugusia.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kwa ufupi imekuja katika wakati ambao naweza kusema ni muafaka lakini kwa kiasi fulani vile vile tumechelewa kutokana na tunakotoka. Suala la viwanda lilionekana umuhimu wake tokea zamani sana katika nchi hii kwa mujibu wa historia na wenzangu wamezungumzia kwa ufupi, lakini kwa mustakabali mzima wa maendeleo ya nchi kama yetu suala la viwanda ni muhimu sana na hivi sasa viwanda hivi zaidi serikali imejivua katika uwekezaji katika masuala ya viwanda. Kwahivyo, kuwepo kwa wakala maana yake yeye atakuwa ni

msimamizi wa suala la viwanda ambavyo vitawekezwa au vimeshawekezwa na vyengine vitawekezwa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika huu waraka wa mswada wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, nikija katika jina fupi la Mswada inasomeka kwamba Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanzibar ya mwaka 2017.

Vilevile, tunapokuja katika sehemu ya pili ya kuanzishwa inasema kwamba kuanzishwa wakala inayojulikana kama Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar, kwa ufupi ikasemwa *SMIDA.* Mhe. Mwenyekiti nipo hapa kidogo hivi vitu nafikiri tuweke sawa ili tukimaliza kupitisha mswada huu basi hii nembo ya sheria hii na jina la mamlaka liwe limekaa sawa, unaposema ufupisho wa *SMIDA* maana yake umeweza kuondoa neno *micro*, ambalo *micro* kwa maana ya vile vidogo vidogo ina maana tayari ushalitema neno hilo.

Lakini hii sheria huyu wakala ni Wazanzibar sasa unakuta katika ufupisho hata hiyo Z haipo na kwa mujibu wa Mamlaka za namna hii nyingi basi neno *Z* lazima liwepo kwasababu hii Mamlaka ni ya Zanzibar. Kwahivyo, napendekeza kwamba katika ufupisho, katika jina iko vizuri, katika jina fupi iko vizuri, Wakala wa Maendeleo Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati Zanzibar basi neno *Z* liwepo. Kama tunataka *micro* ijitokeze kwa maana ya vidogo vidogo na vidogo, basi na ufupisho wetu tuutizame vizuri, hili napendekeza ili tutakapopitisha basi tusije tukawa na mageuzi mengine ambayo yatakuja kutuharimu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika maneno yaliyotolewa ufafanuzi nilikuwa napendekeza katika marekebisho tuje tuyaweke maneno haya katika *Alphabetical Order*, ili tusije tukasahau na yakaenda kama yalivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika ukurasa wa 218 Mhe. Mwenyekiti kwenye kifungu cha tano kifungu kidogo cha (c) napenda nikariri kidogo:

Ukurasa wa 218 kifungu cha 5(c) kinasema hivi:

"Kushirikiana na kuingia katika ubia au ushirika na mtu au ushirika wa watu wanaofanya na wanaojishughulisha na miradi ya kibiashara".

Inaendelea hiyo pana neno yanayoweza. Lakini tunaunda wakala, wakala ni chombo ambacho sio cha kibiashara ni chombo cha usimamizi. Kwahiyo, sasa hapa kidogo nashituka ninapoona kwamba kushirikiana na kuingia katika ubia au ushirika na mtu au ushirika na watu wanaofanya au wanaojishughulisha na miradi ya kibiashara. Sasa hapa naona tutakuwa tunaingiza wakala katika masuala ya kibiashara wakati tunaunda wakala, ili awe msimamizi wa hivi viwanda na tayari huko nyuma serikali imejivua katika masuala ya biashara na hususan vile vile katika masuala ya viwanda. Kwahivyo, ningependa sana Mhe. Waziri alitazame vizuri hili na hususan kwa mantiki ile ya wakala.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurasa wa 220 katika kifungu cha 10. Katika kifungu cha 10 Mhe. Mwenykiti, katika neno la pembeni linahusu wafanyakazi wa wakala tukitazama wafanyakazi wa wakala katika miswada mingi ya aina hii ya bodi basi haitangulii mwanzo. Kwahiyo, ningependa sana kipengele cha Namba 10 kiondoshwe kiende Namba 20, ili tuapoanza na masuala ya bodi tumalizie masuala ya bodi halafu masuala la wafanyakazi likae chini yake kuliko hapo lilipo. Tumezungumzia bodi lakini hapa ni wafanyakazi basi ni vyema ingeanza na Bodi ya Wakurugenzi kipengele cha 11 kika-*cover* hapo halafu hichi cha 10 kikaenda kwenye kipengele cha 20 nafikiri inaweza

tukakaa vizuri na hususan katika muundo mzima wa bodi za aina mbalimbali hapo kilipokaa naona kama sio sahihi sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu cha 11 ukurasa wa 221 imezungumzia Mwenyekiti wa Bodi ambaye atateuliwa na Rais. Kwanza niwapongeze wenzangu wa kamati kwa kuweza kuona kwamba suala la makamu lilikuwa halipo hapa, lakini nashukuru wameweza kuliona kwamba lazima kiwepo kifungu kinachozungumzia Makamu Mwenyekiti, na wenzangu walikijumuisha tu miongoni mwa wajumbe wa bodi. Lakini pia itapendeza yakizungumziwa majukumu ya Makamo Mwenyekiti wa Bodi na pale ambapo hususan Mwenyekiti anapokuwa hayupo, nafikiri katika taratibu nyingi za mabodi hiki kitu kinakuwa wazi kupatikana kwa Makamu Mwenyekiti lakini vile vile na majukumu yake ni vyema yaweze kuelezwa katika hiyo sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 222 katika kifungu cha 17 juu ya posho kwa wajumbe pamoja na maelezo mazuri yaliyopo au *statement* nzuri. Ningependa tuongeze maneno Waziri anayehusika na fedha atakapoidhinisha muda hadi muda hicho kipengele naomba kiingie hapo ili kuiweka hiyo *statement* katika mustakabala mzima kwamba hayo ni masuala ambayo muda hadi muda yanapaswa kuweza kuangaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurasa wa 225 katika kifugu cha 25 kifungu kidogo hapa nilikuwa napendekeza baada ya vifungu viwili vilivyopo napendekeza kuwe na kifungu cha tatu, ambacho kisomeke kama ifuatavyo."Waziri atapaswa kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi taarifa ya fedha ya mwaka ya wakala. Katika mtizamo mwingi wa bodi hichi kipengele kinakuwa kipo lakini hapa sikioni, lakini kitapendeza kuwapo kwasababu waziri anayehusika atapaswa kuwasilisha mbele ya Baraza taarifa zinazohusiana na bodi. Napendekeza kifungu cha 3

kiwepo hapo, nafikiri hakitoathiri mustakbali mzima wa muundo huu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 36 ukurasa 228. Mara nyingi sana huwa napiga kelele juu ya vifungu vya namna hii.

Kifungu cha 36 "Mjumbe wa Bodi, au Afisi wa Wakala hatowajibika yeye binafsi kutokana na jambo au kitu chochote kinachofanywa au kuwachwa kufanywa na ikiwa tendo au jambo hilo litafanywa au kuwachwa kufanywa kwa nia njema katika kutekeleza kazi zake chini ya sheria hii."

Mhe. Mwenyekiti, suala la nia njema hili kwa kweli linaleta utata kidogo kwasababu kuna watu hukusudia kwa makusudi halafu itakujakuwa kafanya au hakufanya kwa nia njema. Hivyo, ningependa Mwanasheria avitizame sana vipengele hivi, kwa mujibu wa uendeshaji wetu, wakati mwengine tunafanya vitu vya kukusudia halafu mtu anakuja kuepuka kupewa adhabu kwa sababu alifanya kwa nia njema au hakufanya kwa nia njema.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika kifungu cha 8 katika jaduweli ambacho kipo katika ukurasa wa 229. Katika kifungu hichi ambacho kipo chini ya jaduweli ya utaratibu wa vikao vya Bodi imezungumzia:

Ukurasa wa 229 kifungu cha 8 (1)

"Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji …"

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi nilikuwa napendekeza kiondoke kielekee katika masuala yanayohusiana na bodi ambayo tumeyataja nyuma yake. Kingeingizwa katika kifungu pengine

cha 20, kwa sababu kule tayari tumekwisha kuzungumza masuala ya kamati.

Mimi nafikiri hapa kama vile tunarudia rudia masuala ya Kamati ni bora kingeondoshwa kikaunganishwa na suala zima la kamati ambalo lipo katika masuala ya bodi katika kurasa ambazo …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia muda wako iko ukingoni.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nimalizie sasa katika ukurasa wa 230. Katika ukurasa huu kwenye madhumuni ukiangalia hii *version* ya Kingereza katika *objects and reasons* kuna vifungu vinne lakini katika huu wa Kiswahili tuna vifungu 3 na kifungu ambacho kimekosekana ni kile kifungu ambacho kinasema *"Empower in Small and Medium Industries in Zanzibar."* Sasa hichi katika Kiswahili kifungu hicho kimekosekana, kwa hivyo kitizamwe tafsiri yake itakuwa vipi kiweze kuingizwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana na niupongeze sana mswada huu kwa kweli katika masuala haya ya viwanda tujitahidi sana katika masuala ya soko, tuone kwamba serikali hii sasa kama tunataka kushajihisha na kuweza kupata soko vizuri kwanza sera yetu lazima hiyo ambayo tunayoiyunda pengine hivi sasa inahitaji kuwekwa sawa, lazima iwe inaendana na *policy* zile ambazo zinazungumziwa masuala ya viwanda na biashara kwa nchi za Jumuia za Afrika Mashariki na zile Jumuia za Kikanda. Lakini vyenginevyo sera zetu zikiendana kinyume au hazihusiani na yale, basi tutakuja kukuta hatuna soko la bidhaa zetu katika viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile serikali hii ingekuwa vizuri ikawa na Maonesho ya Kudumu ya Biashara na Viwanda kama zilivyo

katika nchi yengine. Waanzilishi wetu, maraisi wetu waliopita walilifikiria hili wakaweka maonesho ya kudumu lakini kila anayekuja anakuwa na mabadiliko yake. Ni vizuri sasa umefika wakati tuwe na maonesho ya kudumu ya biashara na viwanda, ili tuwe na soko la ndani na hatimaye ndiyo tutapata wengine wa kuja kuangalia maonesho yale, basi tutaweza kujitangaza vizuri katika bidhaa zetu ambazo tunazozalisha katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi niwaombe sana wenzangu waichangie hii na kupitisha na mimi naipitisha au kuunga mkono sheria hii au mswada huu wa sheria kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid Makame kwa mchango. Sasa namwita Mhe. Hamza Hassan Juma na akifuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia mswada huu muhimu kwa wananchi wetu kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar. Mimi nataka niseme kwamba nia ya Mhe. Waziri ya kuleta Mswada huu wa sheria ni nia nzuri sana, kwa sababu yeye Mwenyewe ni mchumi lakini sasa mswada huu tutakuwa bado tuna-*face* changamoto nyingi sana hasa baada ya kuanza ukuwaji wa hivi viwanda vidogo vidogo ambavyo Mhe. Waziri amevitengenezea utaratibu wa kuboreshwa au kuhuishwa.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wametangulia kusema kwamba hakuna jambo unalotaka kulifanya ili liweze kufanikiwa bila ya kuwangalia historia. Ni kweli Zanzibar hapa katika miaka mingi ya nyuma tulikuwa tuna viwanda vingi sana vilikuwa vinafanya kazi vizuri, vinatoa bidhaa ambazo zina ubora unaohitajika. Kutokana na changamoto mbalimbali viwanda vile vingi vilipoteza uhai na kufariki moja kwa moja, kuna baadhi ya

vichache vinaendelea kubakia, lakini bado vinakumbana na changamoto nyingi. Ili kuweka *record* sawa basi nadhani Mhe. Mwenyekiti ningetumia kama dakika mbili au dakika moja kutaja baadhi ya viwanda ambavyo Zanzibar tulikuwa navyo na vingine bado mpaka sasa hivi vipo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tulikuwa na viwanda vifuatavyo. Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Siagi, Kiwanda cha Maziwa, Kiwanda cha Nyaya za Umeme, Kiwanda cha Masufuria, Kiwanda cha Nguo *Cotex*, Kiwanda cha Magodoro, Kiwanda cha *Cocacola*, Kiwanda cha Sigara. Kiwanda cha Sabuni za kuogea na sababuni za michi, maarufu tukiziita sabuni za chokaa.

Lakini tulikuwa tuna Kiwanda cha mwanzo kabisa kwa Tanzania cha kutengeneza Madirisha na Milango ya *Alluminiam* kikiitwa *Window 2000*, Kiwanda cha Sukari mpaka sasa hivi kipo kinakufa na kufufuka Kiwanda cha Makonyo, Kiwanda cha mafuta ya Nazi, Kiwanda cha kutengenezea *Tissue*, vile vile tuna viwanda vyengine ambavyo havihesabiki kama viwanda lakini vitu ambavyo vinatoa ajira. Viwanda vya Kokoto, Viwanda vya Maseredani, Viwanda vya Matofali kama alivyozungumza Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Ali Kombo alitoa tahadhari ingawa lugha yake inakuwa nyepesi nyepesi, lakini nadhani sisi kama Zanzibar na sisi ndiyo watunga sheria uko umuhimu mkubwa wa kuweza kuweka mikakati maalum, ili mambo tunayoyafanya yawe endelevu yasiwe yanakwenda yanazimika yanakwenda yanazimika.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi suala la viwanda lazima tujiulize kwamba kwa nini tunaanzisha viwanda halafu vinakufa. Mimi nafikiri moja katika changamoto kubwa na hii lazima Mhe. Waziri huu wakala ambao utakauunda sasa hivi katika moja ya

changamoto wakiweza kuisaidia changamoto hiyo basi tunaamini viwanda vyetu vitaweza kufufuka na vilivyokuwepo vitaimarika na vitaendelea, suala zima la kusimamia *access of marketing*.

Mhe. Mwenyekiti, biashara yoyote ni soko, unapofanya biashara unaambiwa kwanza uangalie soko lakini vile vile kuangalia *capital* na kuangalia *rawmaterials* wapi utaweza kupata. Bado soko la Tanzania Bara ni soko ambalo linatutesa sana. Hii inatokana na fikra tu za baadhi ya watu wasiotaka maendeleo hasa kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuna kiwanda cha Sukari Mahonda, hivi karibuni wafanyabiashara wetu kutokana na ukwasi wa upatikanaji wa sukari soko la Tanzania Bara, kuna baadhi ya wafanyabiashara walinunua sukari wakaipeleka Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, hiyo seke seke waliyoipata bandarini walikaribia sukari ile kuitosa baharini kutokana na kitu ambacho kinachotoka Zanzibar kuna kikwazo gani kuingia Tanzania Bara. Wakati kuna sukari inatoka nje ya nchi inaingia Tanzania Bara, leo sukari inayozalishwa Zanzibar inazuiwa kuingia Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Wazanzibar wenzetu wanatengeneza *tissue*, *tissue* zile wanapofika nazo Bara wanaambiwa kwamba *tissue* zile hazikutengenezwa Zanzibar. Kwakweli, hii Zanzibar yaani, wenzetu wanaiyona kama ni tatizo kwao wao. Nadhani Mhe. Mwenyekiti huu wakala utakaoundwa moja katika jambo ambalo wajitahidi sana kusaidia *access* ya soko la kuingia Tanzania Bara. Tatizo linalowakuta wafanyabiashara wetu kwanza mitaji yao wanaipata katika mazingira magumu.

Nimejaribu kuangalia hii Sera yetu ya Viwanda moja katika kitu ambacho ni changamoto iliyoelezwa humu ni suala zima la *access of finance* yaani, upatikanaji wa fedha. Benki moja kubwa

ambayo inayotegemewa ni Benki ya Watu wa Zanzibar, lakini hata hii Benki ya Watu wa Zanzibar, lakini bado mikopo yao haiko rafiki kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo na wakati, kwasababu ni mikopo ambayo inariba kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, masuala haya kama hatukuyachukuliwa tahadhari basi watu watahamasika, wataanzisha viwanda, wataingiza mitaji yao, lakini matokezeo yake wanapoingia katika soko kwa kweli watakuwa wanarudi nyuma pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kama walivyozungumza wenzangu suala la maonesho ya biashara. Zanzibar ni nchi ambayo tunategemea uchumi wetu ni biashara na huduma. Tuliwahi kuanzisha maonyesho Mwanakwerekwe pale yalikwenda vizuri matokezeo yake tukaigeuza skuli. Tumeondoka pale tukaanzisha maonesho mengine Tunguu matokeo yake baada ya kuwa skuli sasa hivi imekuwa Chuo Kikuu.

Sasa hivi labda Mhe. Waziri aje atuambie maonesho mengine yataanzishwa wapi, ili yawe *permanent* yaweze kuwasaidia kuwakutanisha wajasiriamali wetu pamoja na wengine kutoka nje kuja kuonesha bidhaa zao, lakini vile vile kupata ubia na kuingia katika soko kubwa la kimataifa lakini vile la nchi za Afrika ya Mashariki. Kwakweli, kutegemea maonyesho ya pale Michenzani Wajasiri wetu amali wetu pale bado tutakuwa tunaendelea kuwapotezea muda vijana wetu, lakini hatima yao ya kuendelea mbele itakuwa ngumu kuweza kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine bado hatujakuwa na mpango maalum wa kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Mimi mwenyewe nimeshafanya jitihada kuna baadhi ya wawekezaji wametaka kuja kuwekeza kiwanda cha nondo hapa Zanzibar na wana historia nzuri tu wana viwanda karibu vitano katika nchi mbalimbali za Afrika Mashariki pamoja na Tanzania

Bara, lakini wamehangaika kutafuta eneo la kuwekeza kiwanda hicho mpaka wamepiga mkono chini wamekosa kupata hilo eneo. Kwahiyo, nategemea labda huu Wakala utaweza kuja kusaidia kufanikisha kazi kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tukiangalia sasa hivi kuna soko lila la Marekani wanaliita soko la *AGOA*. Mimi nadhani kama huu wakala wetu utaweza kukaa na wafanyabiashara na *Chamber of Commerce* kuangalia na kushajihisha ni bidhaa gani ambazo tunaweza tukaingia katika soko la *AGOA*, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti tunaweza tukawaidia wafanyabiashara wetu. Lakini sasa hivi tukiangalia hata *Chamber of Commerce* tuliokuwa nao wengi wao ni wafanyabiashara wa kununua na kuuza, lakini sio wengi wafanyabiashara wanao *invest* katika viwanda, na sio kama hawataki katika kui *invest* wanakimbia tatizo la upatikanaji wa soko na usumbufu ambao utakaokuwa sio wa lazima.

Mhe. Mwenyekiti, kwakweli masuala haya nafikiri ni muhimu sana kuweza kuboresha au kuanzisha upya uhamasishaji wa viwanda kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia katika mswada nimekuja moja kwa moja katika kifungu cha 4 ambacho kinasema kuanzishwa kwa wakala itakaojulikana kama wakala wa maendeleo ya viwanda vidogo vidogo na vya kati Zanzibar ambavyo kwa ufupisho vitakuwa ni *SMIDA*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani na mimi bado napendekeza jina hili napendekeza jina hili aidha itakuwa *SMIDAZ* au Z mtaitafutia pahala pa kuiweka kwa sababu neno Zanzibar lazima lionekane katika sheria hii. Lakini kuna kitu hapa hata baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wamekuwa wana wasi wasi na hiki kifungu kidogo cha 2 kinachosema “Wakala itakuwa ni chombo cha serikali kisichojitegemea kikamilifu na kwa idhini ya

Waziri na kwa kutumia jina lake litakuwa na uwezo wa ……" Haya mambo ambayo yamewekwa hapa chini kama kupokea kama dhamana, kununua au kwa namna gani.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe, muda wako umemaliza, nakuomba malizia neno lako la mwisho.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hee! Haya.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa wale ambao kuwa hawajapata muda wa kuchangia na wameleta majina yao hapa, nawaomba wafanye michangio yao kwa maandishi kulingana na muda na muda wetu ulivyo, ili tuweze kumpa nafasi waziri anayejibu na tuweze kupitisha mswada huu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nikimuandikia kwa maandishi ghafla Mhe. Waziri nitamchanganya lakini naomba nigaiye kama dakika mbili niweze kumalizia, ili apate kuja kunisaidia kunipa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hichi chombo kama nilivyosema kifungu cha kidogo cha 4. Naomba kushauri kama ilivyo Wakala wengine wa serikali au mamlaka hichi chombo kiwe kinajitegemea moja kwa moja, ili waweze kuwa na uwezo au upana mkubwa wa kuweza kutoa michango yao.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 26 huu Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kifungu hichi ilikuwa huku mbele tuongeze katika kifungu kidogo cha 3 tuongeze (d) katika hivi vyanzo vya fedha. Kwakuwa hapa kuna vyanzo vya fedha kinasema fedha zinazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, misaada na bakaa, fedha zozote halali.

Lakini, naomba tungeongeza kifungu ambacho kitaihakikishia hii taasisi kuweza kupata fedha za uhakika kila wakati, kifungu chenyewe nilikuwa naomba kuwe asilimia moja ya ushuru wa bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nje, asilimia moja ya ushuru basi fedha hizi ziingie moja kwa moja katika huu mfuko maalum wa viwanda kwasababu itasaidia kwamba zile bidhaa zinazotoka nje kuzipunguzia nguvu baada ya kuanzisha mfuko huu bidhaa zile zitaweza kuongezwa hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 24 hapa nitataka maelezo kwa nini hichi kifungu cha 24(a) kimeweka fedha za Wakala zitatumika ufuatavyo, mishahara maposho na mikopo ya wafanyakazi. Kwanini iwepo na mikopo ya wafanyakazi, sijawahi kuona sheria tuliyoipitisha hapa ikaanza kuzungumzia mikopo ya wafanyakazi sasa hii labda nije nipewe sababu lakini mimi nilikuwa napendekeza hili suala la mikopo ya wafanyakazi wa wakala liondolewe, kwasababu tunajua utaratibu wa watumishi wa umma wote mikopo yao inapitia kupitia *guarantee* ya mishahara yao kupitia mabenki mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache vilevile nilikuwa naomba kuna suala hicho hicho kifungu cha 26 suala la *BOT*.

Mhe. Mwenyekiti, *BOT* katika Sera ya *BOT*. Katika Sera ya *BOT* kuhakikisha kuwezesha wawekezaji na wafanyabiashara wa Tanzania kuweza kuwawezesha kufanya biashara. Sasa kuna fedha za *SME* ambazo zinatoka kutoka *BOT* na fedha hizo Mhe. Mwenyekiti kiwango chake kinafika mpaka bilioni nne (4,000,000,000/=), lakini Zanzibar hapa hakuna hata mfanyabiashara mmoja au taasisi yoyote iliyoweza kufaidika na fedha hizo, wakati fedha hizo kuna makapuni na taasisi za Tanzania Bara zinaweza kufaidika.

Kwahiyo, miongoni mwa hizo fedha ambazo au vyanzo vya fedha vya kusaidia Mfuko huu wa Maendeleo wa Viwanda Vidogo Vidogo, basi moja kwa moja zitoke *BOT* katika kifungu kusaidia *Small and Medium Enterprise.*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru. Lakini kuna kitu kimoja nilikisaahau naomba maelezo ya Mhe. Waziri, hii taasisi tunayoianzia haimo katika bajeti, jee fedha zake baada ya kupitishwa hii sheria zitapatikana wapi, kwasababu hapa kutakuwa kuna wakala kuna wafanyakazi kuna bodi fedha zao za kuanzia kazi mpaka Julai itakapofika fedha hizi zitapatika wapi.

Baada ya hayo machache kwa kuwa Mhe. Mwanasheria Mkuu ananitizama, naamini ataweza kunipatia jawabu za kutosha, nakushukru sana naunga mkono hoja na vile vile nitasikiliza jawabu kwa waziri. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma. Waheshimiwa Wajumbe, hapa itakuwa mwisho wa mjadala wetu kwa leo, na kwa wale ambao kuwa hawajapata kuchangia basi walete kwa maandishi kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri karibu kujibu hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia mswada huu kwa michango yao ambayo iliongeza ubora wa huu mswada, na wale ambao walitaka ufafauzi Mhe. Mwenyekiti tutajitahidi kutowa ufafanuzi, kwa ajili kwamba tukitoka tukisha upitisha mswada huu mimi nategemea wao ndio watakuwa wadau wakubwa wa kuweze kuishajihisha chombo hiki, ili kuweze kufanya kazi vizuri.

Kwakweli, walengwa wakubwa wa mswada huu wamo katika majimbo yao kwasababu hawa wajasiriamali wengi wao wako katika majimbo yao wana wahudumia na wengine wanauliza naomba misaada mbalimbali. Kwahiyo, ndio wadau wakubwa watakaoweza kufanya kazi na hao wajasiriamali ambao tayari wamo katika viwanda hivi ili waweze kujiendeleza na nchi iende mbele zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umechangiwa na wajumbe mpaka sasa hivi wajumbe saba akiwemo

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara);
Mhe. Ali Suleiman Ali;
Mhe. Makame Ali Ussi;
Mhe. Abdalla Ali Kombo;
Mhe. Rashid Makame Shamsi; na
Mhe. Hamza Hassan Juma.

Nategemea wengine wataleta michango yao kwa maandishi basi tutawajumlisha na wao wote naanza kuwashukuru japokuwa sijapata michango yao, lakini najuwa kwamba muda mfupi lakini na wao wangechangia kujenga hoja, ili shirika hili yaani wakala ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukuwe nafasi hii kuwashukuru kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu na wajumbe wake wote kwa kufanya kazi na sisi wizara yetu vizuri sana na katika kutushauri na maelezo wanayotupa siku zote tunapokea kabisa kabisa na kwa hii mswada huu naomba nichukuwe pongezi na shukrani za kipekee, kwasababu kamati hii haikufanya kazi hii wao peke yao.

Kamati, imechukuwa wataalamu wakiwemo wataalamu wa *Chamber of Commerce* na wataalamu mbalimbali ambao wanauzoefu katika sekta hii ya viwanda, ndio ambao walikaa nao wakawapa ushauri na maelezo ndio maana maoni yao yakawa mazuri ambayo sisi kama wizara tunayaunga mkono na imeongeza ubora wa hii mswaada. Kama milivyoona kiambatanisho cha marekebisho ambayo kamati imefanya imetokana na busara na kazi nzuri waliyoifanya wajumbe wa kamati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kujibu wa mchango wa Mhe. Hamza Hassan Juma kwasababu watu kidogo nitajibu kwa haraka haraka lakini nitaunganisha baada ya michango kwasababu mengine imejirejea ningenza kuanza na mchango wa Mhe. Ali Suleiman Ali almashuhuri Shihata. Mchango wake kwanza alizungumzia historia ya viwanda, historia ya sisi kama Zanzibar tulivyokuwa tumekwenda na viwanda miaka yote hii na mchango wake kuhusu historia ningeomba niunganishe na mchango wa Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na mchango na Mhe. Makame Ali Ussi kuhusu historia.

Niseme tuu kwamba Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwamba miaka mingi tuliyokuwa nayo ya viwanda Zanzibar viwanda vyetu vingi vinategemea mali asili tuliyokuwa nayo yaani malighafi tuliyokuwa nayo. Kwa mfano, sekta ya kilimo ndio iliyokuwa inachangia viwanda vingi hapa Zanzibar nitowe mfano tu kwamba ukiangalia viwanda vya mafuta ya nazi vilikuwa viwanda vinategemea mafuta ya nazi ni sekta aya kilimo hapa Zanzibar.

Miaka ya nyuma kiwanda hiki cha mafuta ya nazi kilikuwa inatoa bidhaa mbalimbali kuanzia mafuta yenyewe, nazi watengeneza mashudu, wakitengeneza sabuni na kadhalika hiyo ilikuwa ni sekta moja. Lakini pia msisahau kwamba katika sekta hii ya nazi

kuliwa vile vile makapeti na dometi mambo mengi yakitokana na sekta hii ya nazi, bahati mbaya sekta ya nazi kwasababu tumeitumia vibaya matokeo yake sasa hivi hatuwezi kusema tunataka ku-*promote* sekta ya nazi kwasababu minazi yenyewe haipo.

Jukumu tulilonalo sisi na Wizara ya Kilimo waangalie utaratibu mwengine mpya tutakaoweza kushajihisha zao la nazi, vile vile kuangalia utafiti tafauti na nchi mbali mbali kwa mfano *Sri Lanka* wamewezaji na wao kuhuwisha zao na nazi mpaka sasa hivi nazi *Sri Lanka* inachangia sehemu kubwa katika sekta yao ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, pia ukiangalia katika hii sekta huko nyuma viwanda vyengine vikitengea kilimo tunavyo viwanda wa viungo na karafuu, ndio maana tunavyo viwanda sasa hivi vingi viwanda vyetu kama cha makongo ni moja wa kiwanda, ambacho kimekaa muda mrefu kinatakiwa kifanyiwe ukarabati sasa hivi, lakini ni kiwanda ambacho kinachangia pato la taifa. Huko nyuma viwanda vya ngozi na viatu vimekufa kwasababu malighafi tulikuwa hatuna sisi hatuna ngozi hapa ya kutosha kwahiyo viwanda hivi kama hiki hapo kimekufa.

Viwanda vya soda na vyengine vyengine kwa hiyo soda iliyokuweko kule ya potelo navyo vile vile havikuweza kuhimili ushindani wa soda ya *Cocacola* za nje pia viwanda hivi vimekufa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tuangalie pato la viwanda wakati ule kama alivyosema Mhe. Makame Ali Ussi pato la viwanda ilikuwa inapata ikishuka kuanzia kulikuwa kuna kipindi asilimia mbili, kuna kipindi cha asilimia sita, kipindi chengine asilimia saba. Lakini katika miaka hii ya awamu hii pato la viwanda kwasababu *category* ya viwanda inajumlisha pia viwanda vya kokoto na kadhalika.

Pato la viwanda kwa mfano mwaka 2015/2016 imeongezeka kuchangia kutoka asilimia 18.1 mpaka asilimia 18.6. Vilevile, tukizungumzia *manufacture* yaani, viwanda vinavyozalisha hasa kwa mfano hayo mambo mbalimbali mafuta ya makonyo na kadhalika, viwanda hivi vimechangia kwa mfano mwaka 2015 asilimia 6.7 na mwaka 2016/2017 zimechangia asilimia 6.9. Tunategemea mwaka 2017/2018 sekta hii itachangia zaidi kwasababu viwanda kama vya vyakula na viwanda vya sukari imeongeza vile vile uzalishaji kwa hiyo mchangio wake utakuwa mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie sasa baada ya mapinduzi kulikuwa na nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya mapinduzi ilianzisha wakati ule Shirika la Jitegemee Viwanda Vidogo Vidogo. Shirika, hili nalo halikufanya vizuri baadhi ya shughuli zake zikafa kwasababu gani ya kwanza tatizo la kuwa na fedha za kigeni zilikuwa hazipo kwasababu viwanda hivi vilikuwa vinagemea zaidi malighafi ya kutoka nje, kwa mfano hayo masufuria na kadhalika sehemu kubwa ya viwanda hivi ilikuwa malighafi inatoka nchi za nje.

Kwahiyo, ikitumia sana fedha za kigeni kwasababu tulikuwa tunasema kwamba tuna viwanda vya kupunguza pesa za kigeni lakini viwanda hivi navyo vikawa vinategemea vile fedha za kigeni, iyo malighafi kutoka nje na matumizi ya fedha zile yakawa yameongezeka lakini na *competition* vilevile ya bidhaa za nje ikasabisha viwanda hivi navyo vipate matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumzia sera ya soko huria katika miaka thamanini tulikuwa na soko hurua ndio vikaja viwanda vingi binafsi kama *COTEX*, *BANCO* na vyengine lakini pia viwanda hivi navyo ikawa inategemea mali ghafi kutoka nje. Kwasababu *COTEX* ikitegemea zile nyuzi kutoka nje zikiagizwa

na viwanda vya *BANCO* madawa na sehemu kubwa vilevile yakitokea kutoka nje.

Sasa hiyo ndiyo tafauti Mhe. Mwenyekiti ya wakati ule. Sasa hivi nini serikali inataka ifanye serikali baada ya kupitia na kuangalia hali halisi ilivyokuwa kule nyuma ikaona kuna haja kutizama tulikosea wapi na changamoto zile vipi na tufanye nini.

Kwahiyo, naomba nimjibu swali la Mhe. Abdalla Ali Kombo kuhusu taaluma na kama tumejiandaa na kama kuna matayarisho yaliofanywa na kama tumeangalia hali halisi yaliulizwa maswali mengi na wengine waliuliza maswali mengi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwajibu Waheshimiwa Wajumbe kwanza kwamba tafiti nyingi zimefanywa Mhe. Mwenyekiti tafiti ya kwanza ilifanywa mwaka 1998 hawa watu wa *UNIDO* walitufanyia utafiti unaitwa Sera za Viwanda, utafiti mwengine Mhe. Mwenyekiti ukafanywa mwaka 2006 wakati ilipokuwa inaundwa Sera hii ya Ujasiriamali na hiyo waliifanya *UNIDO* hawa ni wataalamu wanoshughulikia masuala ya viwanda.

Utafiti mwengine Mhe. Mwenyekiti ukafanywa mwaka 2015 wakati wa kuandaa Mkakati wa Viwanda umefanaya ya *JAICA* na halafu mwaka 2016 hivi karibuni tukafanya *review* ya kupitia Sera hii ya Ujasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, na tafiti zengine nyingi ambazo zimefanywa kwa kuangalia viwanda kimoja kimoja kwa mfano kama kiwanda masuala ya mwani kwa kuangalia masuala mengine kwa mfano ya chumvi na kadhalika. Tafiti Mhe. Mwenyekiti nyingi zinafanywa na sisi Wizara yetu tuna utaalamu wa kutosha kwa sababu wataalamu tunawagemea wa nje na wa ndani wanatusaidia sio tuu peke yetu wizara yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, likaja suala la taaluma ya kuendesha viwanda lazima nitowe ufafanuzi kuhusu taaluma ambayo nadhani muhimu kuna taaluma mbili lazima kama serikali au wizara lazima tuzisisitize. Taaluma ya kwanza ni kwa mjasiriamali huyo mwenye kuonesha viwanda kwasababu Mhe. Mwenyekiti viwanda hivi ambavyo wakala huu utasisimia ni viwanda ambavyo vidogo kwasababu wengi hawana wajasiriamali, viwanda vidogo na vidogo vidogo zaidi ni wajasiriamali ambao sasa hivi wapo wanaendesha biashara hii, tusisahau kwamba sasa hivi katika viwanda elfu mbili na idadi yetu sehemu kubwa ya viwanda hivi wajasiriamali ambao wapo sasa hivi wanafanya biashara zao.

Tunatakiwa wajasiriamali hawa tuwape taatuma ya kutosha ya kuweza kuendesha biashara zao, taaluma za aina gani kwanza taaluma ya kuendesha biashara taaluma hiyo wanayo muda mrefu tumewapa taaluma hiyo hivi juzi tumeanzia *Incubation Centre* ambayo iko Mbweni inasimamiwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, ili kuwapa taalauma ya kuendesha biashara taaluma vilevile ya kujua jinsi ya uzalishaji wa biashara zao, taaluma pia ya kujua ubora wa bidhaa zao, taaluma vile vile ya kuwafahamisha utaratibu gani wa kuweza kupata ule ubora na vyombo vinosimamia ubora, ili waweze kuwasaidia.

Vilevile, taaluma tunatakiwa tuwape ya kujua soko liko wapi na niunganishe na hoja zilizounganisha na Mhe. Abdalla Ali Kombo, kuhusu kujua wale watumiaji wa bidhaa zile hiyo nayo ni taaluma muhimu ambayo wakala anatakiwa aijuwe na tumesema ukiangalia katika sheria yetu haya ni majibu ambayo wakala atafanya kuwaendeleza wajasiria mali na kuwapa elimu zaidi.

Ni kweli hatuwezi kuanzisha viwanda bila kujua viwanda vile tulivyovianzisha vinahitajika au havihitajiki, viwanda vile

tunavyovianzisha jee mteja wetu yuko wapi na anahitaji kitu gani na kujuwa kwamba kuna tafauti kubwa sana baina ya wateja wanatumia bidhaa zetu, tuwajuwe kutegemea na makabila yao, tuwajue kutegemea na mambo yao wanayoyapenda, tuwajue kutegemea na mila na silka na taratibu na tamaduni zao.

Mhe. Mwenyekiti, huwezi kuchukuwa biashara ukaweka kule ambapo hakutakiwi. Kwa mfano, kama tunajua kwamba Wamasai hawatumii kitu fulani, kwa hiyo hatuwezi kufanya biashara tukawa tunawalenga Wamasai, tutafanya biashara za viwanda kutegemea na kuwalenga watu ambao tunawajua utaratibu mzima mahitaji yao, uwezo wao na kadhalika. Kwahiyo, yote hayo Mhe. Mwenyekiti, wizara yetu imejiandaa na katika moja kazi ya wakala hii kufanya mambo yote ambayo nimeyaorodhesha.

Vilevile, kutakiwa taaluma kwa ajili ya wafanyakazi bahati mbaya mara nyingi nchi za Kiafrika tulipokuwa tunanzia shughuli kama hizi tunasahau kuwatayarisha wafanyakazi kufanya kazi katika viwanda kama hivi, na ndiyo maana mara nyingi viwanda kama hivi vinakwama kwasababu kunakuwa hakuna wafanyakazi wa kuweza kufanya kazi hii. Kwakweli, tunakuwa mara nyingi tunashikilia kuwafundisha wataalamu, lakini wataalamu wana-*role* yao lakini na wafanyakazi wadogo wadogo ambao ni mafundi, washoni, wasimamizi wanajuwa wanaosimaiya masuala ya ubora wote hawa wanatakiwa watayarishwe.

Kwahiyo, kuna haja kabisa na serikali imejiandaa kupitia Wizara yetu hii ya Elimu na Mamlaka inayoshughulikia elimu hii ya *Vocational Training*, ili kuwa-*train* vijana wetu ambao watakuwa wanahitajiwa kwa sekta maalum kwa viwanda maalum kwa wakati maalum. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kama hivi sasa tunazungumzia masuala ya viwanda kwa ajili ya uvuvi, ni vizuri sasa hivi kuanza kuwafundisha vijana wetu masuala yanayohusu

mambo ya uvuvi huko nyuma kulikuwa na mchepua wa mambo ya uvuvi lakini ukaondoshwa. Kwahiyo, kurudia utaratibu wa mchepuo ambao umeanza sasa hivi kuna mchepuo katika shule zetu, basi nadhani ni utaratibu mzuri tuendeleze watoto wetu, ili waweze kuja kujaza nafasi hizi zinazohitajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali pia alizungumzia masuala ya soko hili nitakuja kulijibu nitaliunganisha na upande wa pili. Lakini jengine ambalo Mhe. Ali Suleiman Ali alilizungumza kwa ujumla wake, kwamba hii wakala itakuwa ina kazi kubwa kusimamia na naomba nimuhakikishe kwamba wakala huu utakuwa na kazi kusimamia kwasabau unashirikiana sasa hivi na vyombo ambavyo vina uzoefu wa kutosha kwa mfano kama *SIDO*. Vilevile, chombo cha kusimamia viwanda vidogo vidogo cha India, pia tunazungumza na Serikali ya China na baadhi ya vyombo kama hivi vilioko China. Kwahiyo, sisi tumejiandaa na ningeomba wenzangu Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasiwasi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kujubu hoja ya Mhe. Makame Ali Ussi pia yeye alikuwa mchangiaji wa pili Mhe. Makame Ali Ussi alizungumzia zaidi mambo mengi yanayohusu *philosophy* na kadhalika na mambo mengine yanayohusu nani ambao tutawaajengea hivi viwanda na kadhalika, nataka kujua muelekeo sisi malengo ya viwanda hivi na vile vile ile *philosophy* hasa iliyokuwa nyuma yetu na kuna mipango gani.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii nieleze *philosophy* ya hii leo tunazungumzia mswaada kwa ajili ya kuangalia sekta ndogo ya viwanda, kwasababu ulivyokuwa unafanya unatizama viwanda katika *spectrum* yote katika upeo wote mkubwa viwanda viko vya aina mbili au tatu kubwa.

Kuna hivi vidogo vidogo ambavyo tumeshaviorodhesha lakini pia tukiamaliza viwanda vya kati tuna viwanda ambavyo ni vikubwa zaidi ya mtaji ambao umewekwa kwa mujibu wa sheria hii, viwanda vile navyo kwa mujibu wa sheria za Zanzibar, kuna sehemu mbili kuna viwanda ambavyo vinasimamiwa na *ZIPA* na kuna viwanda ambavyo sasa hivi viko nje ya *ZIPA*. Vile vya *ZIPA* ni vile ambavyo vinasimamiwa na masuala ya wawekezaji kutoka nje, na vilevile kwa mtaji ambao unatakiwa mwenye kiwanda aweke na vile ambavyo viko nje ya *ZIPA* ni hivi ambavyo tunavizungumzia lakini, mkakati wetu tumeorodhesha viwanda kwasababu sekta yaani, viwanda ambavyo kwa ujumla wake vyote hivyo ndio viwanda ambavyo tunavisimamia katika *priority* ambayo au kipaumbele ambacho tumekiweka.

Viwanda vya kwanza ni viwanda kwa ajili ya *agro-industry* yaani, *processing* vikiwemo viwanda vya kusarifu matunda, mboga mboga na vitu vyengine ambavyo vinahusiana na hapo vikiwemo asali na vitu vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile baada ya kuangalia sekta ya kilimo tunaangalia sekta nyengine ya uvuvi kwa humo katika sekta ya uvuvi kuna samaki na kuna vitu vyengine vinavyozalishwa katika bahari ikiwemo mazao mbalimbali yanayotokana na bahari kama chumvi na kadhalika.

Lakini pia tunangalia sekta nyengine upande wa kutengeneza nguo, kutengeneza *bedsheets* vitu ambavyo vinahusiana na utalii na vitu ambavyo tunatumia utamaduni wa Zanzibar, tunatumia silka ya ujuzi ulioko Zanzibar vikiwemo tunatengeneza *jewelries* na kadhalika, pia tunaangalia viwanda vya madawa na vitu vinavyohusiana na hospitali, tunaangalia viwanda vya teknolojia na vitu vinavyohusiana na teknolojia na viwanda vinavyohusiana na mambo ya sekta ya utalii ikiwemo mfano viwanda vya mafuta ya *spices* na mambo mengine. Mwisho tunaangalia viwanda kwa

kutumia utaratibu wa kisayansi na kiteknolojia ikiwemo viwanda vile vya kutengeneza data na kufanya teknolojia na kutengeneza vitu vya *electronic*.

Mhe. Mwenyekiti, katika filosopia, *philosophy* iliyopo sasa hivi na tunayotaka tuifate sisi Zanzibar ni *philosophy* ya kutumia *value chain* ndio maana tukaanza na sera yetu na mswada huu kwasababu tunataka viwanda vya kuweza kulishia viwanda vikubwa. Tunapozungumzia mnyororo wa thamani kwamba kutakuwa na viwanda kama hivi vidogo vidogo mazao yao au vitu vyote vinavyozalishwa vitakuwa vinakwenda kurudishia viwanda vikubwa vilivyopo Zanzibar au vilivyopo nje ya Zanzibar. Huo ndio utamaduni ambao tunaotaka tuufanya juu ya *philosophy* ambayo iko nyuma yetu na tumeona uwezo huo tunao.

Mhe. Mwenyekiti, uwezo huo tunao kwasababu viwanda vyetu sasa vilivyopo bado vingali vidogo lakini vikiwezeshwa kupewa utaalamu, kupewa rasilimali. Mfano, kama mitaji, kuangalia wafanyakazi wote wanafundishwa vya kutoshwa na ubora wa bidhaa zao ni nzuri kama ilivyotakiwa katika masoko. Mhe. Mwenyekiti, tutaweza kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano tu kule Bara ilikuwa wanazungumzia kuanzisha *assembly* ya magari, sisi tukasema kwamba kama wao wataanzisha kiwanda cha *assembly* ya magari sisi Zanzibar kuna uwezekano wa kufanya vitu ambavyo tunaweza tukafidia katika kile kiwanda cha *assembly* ya magari. Kama kutengeneza sehemu za makochi kwa kutumia usumba na vitu vyengine vyengine. Kwahivyo, hiyo ndio dhana tunayokwenda nayo kwamba viwanda hivi ndio viwe viwanda vya kuweza kulishia na ndio maana wanafanya nchi kama Malaysia, nchi kama Indonesia na nchi nyengine. Kutokana na hali hiyo, hivi sasa sio lazima viwanda viweko Zanzibar ili tuweze

kuvitumia, viwanda vinaweza kuwa nje ya Zanzibar tukaweza kuvitumia.

Kwahiyo, msingi wetu mkubwa ni *value chain* na viwanda hivi ambavyo tunataka kuvishajihisha ndio vitakavyoweza kutusaidia kuweza kufika huko tunakotaka kwenda. Nafikiri hiyo pia nimejibu *objectivity* aliyoizungumza mheshiwa. Pia alizungumza habari ya siasa kwamba viwanda hivi viende sawa sawa na siasa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napingana kidogo hapa kwasababu hatutaki viwanda hivi viwe vinafanya siasa. Tunachotaka kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaongozwa na sera za vyama, kwa sasa hivi Chama cha Mapinduzi ndio kinachoongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa hiyo Sera za Chama cha Mapinduzi ndizo zitakazokuwa zinaongoza katika suala zima la uendelezaji wa viwanda.

Kama mnavyojua ilani ya uchaguzi ya 2015 na 2020 tumeipitisha wenyewe na ndio ilikuwa *platform* inatufikisha hapa leo tukawa tunaongoza serikali. Kwahiyo, katika utaratibu mzima wa wakala jambo ambalo wakala tutakuwa tunasimamia ni kuwashajihisha na kuwasaidia, pamoja na kuwaelekeza wajasiriamali waweke viwanda vinavyoendana sawa sawa na Sera ya Chama chetu cha Mapinduzi ambayo ndio inayoongoza nchi yetu.

Wakala huo hauanzishi viwanda. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitowe ufafanuzi zaidi inaonekana kama wakala huu utaanzisha viwanda, hapana. Wakala huu utakuwa unawashauri wajasiriamali watapokuwa wanafikiria kuanzisha viwanda, viwanda hivyo viendane na mkakati ambao tumeuweka wa viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma ndio maana viwanda vikawa vime-*fail*, mtu anaweza akaamka asubuhi akasema analeta kiwanda fulani akaweka bila ya kufata utaratibu, bila ya kujua

umuhimu wa kile kiwanda, bila ya kujua soko liko wapi, bila ya kujua mkopo atapata wapi? Maana ya wakala huu ni kuwasaidia wajasiriamali na kuwawezesha kufanya mambo ambayo yatawapa tija. Kwahiyo, sisi kazi yetu itakuwa ni kuwaelekeza na kuwafahamisha na kuwaelekeza kule ambako tunataka wafuate, ili uchumi wa nchi ukuwe na pato la wananchi liweze kuja juu.

Mhe. Mwenyekiti, kwahiyo utaratibu wa *value chain* ndio tutakaotumia lakini tutawashauri, tutafanya utafiti, tutawasaidia kufanya ubunifu. Suala la ubunifu ni muhimu sana kwasababu fursa zipo hivyo tunataka wananchi wetu watumie fursa zao zilizopo, ili waweze kujiendeleza. Wakala huu utakuwa unawasaidia kuchanganyisha fursa zao walizoziona na kuwawezesha, na kuwapatia mambo ambayo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. Hiyo ndio kazi kubwa ya wakala huo ambao tunataka tuuwanzishe.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ubora alilolizungumza Mhe. Makame Ali Kombo pia ni muhimu, kwasababu kitu ambacho kinatufelisha sisi viwanda hapa vinavyotengeneza vitu lakini bidhaa zetu hazifiki mbali kwasababu ubora wao haujakuwa ule unaotakiwa. Kwahiyo, vyombo vyetu vya ubora tuna *Zanzibar Bureau of Standard* na tuna Bodi ya Vyakula. Bodi hizi mbili zitaimarishwa, ili kuwasaidia na wao na kuwapa elimu na kuwaelekeza katika ubora unaotakiwa, ili waweze kufanyabiashara zao na waweze kupata soko linalohitajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama ikiwa tunaona kwamba uzoefu unakuwa hautoshi mara nyingi *TBS* kwa kushirikiana na *ZBS* wana utaratibu maalum waliopanga wa kuwasaidia hasa wajasiriamali wetu wanakwenda wengi kule wanasaidiwa kule Bara. Pia *FIDO* vile vile inawasaidia wajasiriamali wetu, ili kuweza kufika katika ule ubora ambao unatakiwa. Mhe. Mwenyekiti, hili nalo tunalitilia uzito ambao unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Ali Kombo yeye alisema kwamba ana wasiwasi kama tunaanzisha hatujajiandaa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimtoe wasi wasi huo kwa nini sisi hatujaanza kupiga makelele kama wanavyofanya wenzetu kule Bara. Kwasababu ukilinganisha sisi na Serikali ya Muungano, wenzetu wa Serikali ya Muungano wako vizuri kiviwanda, ingawa nao hawako vizuri zaidi kwa mujibu wa taratibu zao walivyojiwekea, lakini wako vizuri kiviwanda. Sisi tuko katika hatua sasa hivi ya kufanya *review* kuangalia kwanza kupitia zile sera zetu, tushapitia Sera ya Wajasiriamali, tunapitia Sera ya Viwanda Waheshimiwa Wajumbe.

Sera ya Viwanda Zanzibar imepitishwa mwaka 1998 na imeeleza mambo chungu nzima ya kutekeleza kwa bahati mbaya mengi hayajatekelezwa. Kwahiyo tunapitia sera zile na tunajipanga vizuri zaidi lazima tufanye *review* ya sekta nzima ya viwanda, kujua ni viwanda vya aina gani. Hapa vipi tufanye, imefikia wapi ukiacha viwanda vidogo vidogo ambavyo vipo sasa hivi huu ni utaratibu wa kipindi cha muda mfupi wa miaka mitatu hii.

Lakini tunajiandaa kwa utaratibu wa kipindi cha muda mrefu kulingana na kama tunavyojuwa MKUZA unamalizika tunaingia katika MKUZA mwengine na tunaingia katika dira nyengine. Maana yake 2020 dira nyengine inabidi inatayarishwa sasa hivi na mipango imeshaanza. Kwahiyo, itabidi tufanye mapitio ya Sera ya Viwanda, lakini tupange mkakati au mpango wa viwanda, mpaka sasa hivi mpango wa viwanda hatuna.

Hivyo, tunatakiwa tutayarishe mpango wa viwanda ama unaweza kuwa miaka mitano au miaka mitatu inategemea Tume ya Mipango tulivyokubaliana, na Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi ya kuja kuzungumza mpango wa viwanda na hayo

wanayosema yote tutaweza kuyatia na kuyajumuisha. Mhe. Mwenyekiti, si kweli kama hatujajiandaa, tumejiandaa na tunajua tunakokwenda tunaanza na wakala huu kwa ajili ya hawa walioko tayari wanafanya kazi, lakini tunajiandaa kwenda mbele kwa kuwa na mpango ambao utakuwa unaangalia masuala yote.

Tunaangalia *EPZ* kwa nini tumefeli kwenye *EPZ* hatukwenda vizuri zaidi, na kwa nini maeneo yote mpaka sasa hivi hayajakuwa *develop*, kwasababu ya mambo mbalimbali tunayaangalia. Kuna eneo la Micheweni, kuna eneo la Fumba, Fumba tumeanza kwa kupewa Said Salim Bakhresa eneo na kujenga nyumba, kuna eneo jengine la *EPZ* na *ZIPA* wana eneo la *EPZ*. Kwahiyo, hayo yote inatubidi tuyatizame na tuweze kuyafanyia mpango. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaangalia vilevile utaratibu wa kuangalia *special economic zones* zaidi katika sekta ya kilimo. Tunataka sekta ya kilimo kwa mfano viungo kwasababu *ZSTC* Kiwanda cha Makonyo kimeshapata fedha kwa ajili ya kuweza kufanyiwa upanuzi na kuweza kuendelezwa zaidi, lakini tunatakiwa tuwe na mashamba makubwa ya viungo na mambo mengine, ili viweze kulisha Kiwanda hiki cha *ZSTC* ambacho kitakuwa kikubwa, kitakuwa na sehemu tatu kubwa zaidi kwa ajili kuhudumia wananchi wetu lakini kuwa kama ni soko la kununua bidhaa zetu na kuweza kuuza nje. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwamba *EPZ* ya kilimo Ethiopia ipo tunataka tuiangalie nayo je tunaweza kuanzisha hii na tutafaidika vipi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuangalia maeneo mengine kama ya *logistic park* kuna utaratibu *logistic park*, hayo nayo ni maeneo mapya tunatakiwa tuyatizame. Kwahiyo, kama nilivyosema hii sheria tunayoipitisha leo ni ya kipindi cha muda mfupi tunajiandaa kipindi cha muda mrefu kutaka kwenda sambamba na dira ya baada ya mwaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine alilouliza Mhe. Abdalla Ali Kombo, mengi ameyauliza mambo yote yanayohusu mambo ya *demand*, mambo ya *competition,* tunajua *competition* zetu zikoje kwa bidhaa zetu ni zipi, tunaangalia utaratibu wa masoko nitalieleza la masoko peke yake, tunaangalia utaratibu wa je bajeti kwa mfano hili aliuliza Mhe. Hamza Hassan Juma tukipitisha huu wakala je bajeti ipo?

Mhe. Mwenyekiti, huu wakala tumewekewa *special provision* katika sekta ya viwanda, tumepangiwa kama milioni mita tano kwa ajili ya kuanza mara tu ikipitishwa hii sheria tutaanza kuanza kazi hii, na hivi tunaangalia tumeoneshwa eneo ambalo tunaweza kuanzisha tutalifatilia lile eneo kwa sababu lipo kuweza kulijenga. Nadhani mimi kipindi cha mwaka 2018 tutaweza kuwa pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya wakala ilikuwa ni bilioni tano lakini imegaiwa katika miaka minne, mwaka huu kuanzia tunaanza na milioni mia tano. Itakuwa katika kipindi cha mwisho cha bajeti yetu kwasababu imetiwa kama nilivyosema *provision* katika bajeti ya serikali.

Kwahiyo, mengi aliyozungumza Mhe. Abdalla Ali Kombo haya wakala watayazingatia. Kwa mfano, suala la usafiri tunaangalia sasa hivi bidha hizi zinazokuja usafiri wake unakuwaje? Kuna hofu kwamba wengi wajasiriamali wetu natoa mfano hawawezi kusafirisha kwasababu biashara zao ni ndogo ndogo.

Tutazungumza na watu wa *freight forwarders* kuona kwamba unaweza ku-*share* makontena kwasababu wanafanya nchi nyingi tu ku-*share* makontena yanasafirishwa kama yanakwenda sehemu moja yanapelekwa. Kwahiyo, kuna mbinu nyingi ambazo ni za kibiashara wajasiriamali wetu hawazijui ambazo sisi tunazijua na taaluma hiyo tutawapa wajasiriamali wetu. Sasa mambo yote aliyozungumza Mhe. Abdalla Ali Kombo ni muhimu na nayaunga

mkono na kwa kweli tumejiandaa kuyafanyia kazi kama inavyobidi.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho alilozungumza Mhe. Abdalla Ali Kombo hili naona niliseme kwamba sera mpya zinakwenda na rais mpya.

Mhe. Mwenyekiti, sio kweli sera hazifanywi na rais peke yake, kama nilivyosema pale mwanzo sera zinafanywa kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama chetu. Na ukiona kwamba nilisema mimi hapa sera hii ya viwanda ilifanywa 1998 ndio hiyo ambayo tunaendelea nayo kwasababu ni Sera iliyosimamiwa na Chama cha Mapinduzi na ilikuwemo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa hivi tunaitizama na ndio maana hatua hizi moja moja tunazozichukua kama mfano kuanzisha chombo kama hiki kimetajwa mle katika sera ya viwanda ya 1998, kwamba kuanzishwa Kituo cha Kuendeleza Biashara na Viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Makame Shamsi aligusia kuhusu sheria akasema imechelewa sana. Mimi nakubaliana naye kwamba hiki chombo kilitakiwa kianzishwe muda mrefu lakini ndio bahati mbaya kilikuwa hakijaanzishwa mazingira yalikuwa hayakuwa yakuweza kuanzisha chombo hiki, lakini wakati huu ni wakati muafaka wa kuanzisha chombo hiki. Alizungumza yeye na Mhe. Hamza Hassan Juma nafikiri kuhusu jina.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na serikali hatuoni tatizo na hili jina, lakini tumetoa mapendekezo kwamba katika huu mswada kuna sehemu tulitaja Zanzibar, kwasababu mwanzo katika huu mswada tumesema hapa kuanzishwa wakala huu ukiangalia Nam. 4 wakala huu kuhusu Zanzibar ambayo itaitwa *the SMEDA*. Kwahiyo, tutaiondosha

Zanzibar huku inakotajwa kwasababu Zanzibar tayari imeshatajwa hapa mwanzo katika hii sheria yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba nchi zote zinazoanzisha wakala kama huu ama mamlaka ama *agency* hawajataja nchi zao. Kwahiyo, sio lazima sana kutaja nchi zetu. Kwa mfano, kuangalia *FIDO, FIDO Small Industrial Organization* haikusema Tanzania, ukiangalia *SMEDA* ya Mauritius (*Small and Medium Enterprises Development Agency*) ya Mauritius haikusema Mauritius, ukiangalia ya India *National Small Industrial Organization* haikusema India, na *SMEDA* vile vile hata ya Japan haikusema.

Kwakweli, hili jina kwasababu lazima utie Zanzibar, kwakweli sio lazima sana. Kwahiyo, tuliona kwamba muda wenyewe unatosheleza hata kwamba hawa *micro* hatukuwataja lakini *micro* ni sehemu vile vile ya *small,* kwa hiyo ingawa ni *smaller than small*. Hiyo, ni vizuri kama tulivyoitia mapendekezo yetu sisi wizarani na serikali tuyaache kama ilivyo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Makame Shamsi aligusa kifungu baada ya kifungu, nimekubaliana na baadhi ya mapendekezo yake mengine yamo katika marekebisho waliofanya kamati. Vilevile, kuhusu kifungu cha 25 alisema kwamba waziri atapaswa kuwasilishwa kwenye Baraza kuhusu maendeleo ya ufanyaji kazi wa wakala huu. Kwa mujibu wa sheria iliyofanywa marekebisho ya utumishi wa umma hili limeshafanyiwa marekebisho kwa hiyo mawaziri sisi wote wenye mashirika yetu ama wakala tutakiwa kuleta taarifa katika Baraza. Sheria imeshachukuliwa hiyo imo katika sheria kubwa ya utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusu uwajibikaji wa wajumbe. Huu ni utaratibu ambao upo kwasababu hawatoweza kukwepa uwajibikaji wao, kwani lilipotokea jambo kunakuwa na utaratibu

wa kisheria ambao unafatwa. Kwahiyo, kifungu hiki nacho inatakiwa kiachwe vilevile.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8 kuhusu bodi, hayo mheshimiwa kama nilivyosema tumeyakubali na yatafanyiwa kwa mujibu na wenzetu wa sheria wakiona wataichukulia hatua.

Mhe. Mwenyekiti, labda niseme moja ambalo ni la muhimu katika hili ni kifungu kinachohusu maonesho ya kudumu, na haya naunganisha na maoni ya Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia na yeye kuhusu maonesho ya kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, maonesho ya kudumu serikali imekwisha kuamua na tumeshapewa eneo sisi kama Wizara ya Biashara kujenga maonesho ya kudumu. Tumepewa eneo la eka 88 Nyamanzi hili eneo tunatakiwa tujenge kituo cha kufanyia mikutano, lakini pia tunatakiwa tujenge vile vile eneo la maonesho na kujenga maofisi na kujenga hoteli kwa wanaokuja, na kujenga nyumba za kuwapangisha wale wanaokuja kwenye maonesho wanatakiwa wengine watoke nje basi wanaweza kukaa katika nyumba kwa sababu ni kama *apartment*. *(Makofi)*

Kwahiyo, kazi hii tumeshapewa na wizara yangu tumeshaanza kutafuta wawekezaji tumeshapata kama wawekezaji tumeshapata kama wawekezaji watano ndio tunaendelea sisi na Wizara ya Fedha na Mipango kuweza kuona wapi wanaweza kutujengea hilo eneo. Kama nilivyosema gharama za kujenga eneo hili ilikisiwa milioni mia moja mpaka mia moja na ishirini dola. Hivyo, hii kazi Mhe. Mwenyekiti ningewaomba tuendelee nayo na nadhani katika miaka miwili hii tutaweza kuwa na maelezo ya kutosha kuhusu eneo la kudumu la kufanyia maonesho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niseme kwamba kwasababu ya hali hiyo tunalo eneo ambalo tunatumia sasa hivi, nalo ni Maisara

tumepewa fedha mwaka jana kama mnakumbuka tulipewa bajeti ya milioni mia sita kununua magazebo ambayo yatakuwa ya kudumu mpaka hapo tutakapokuwa na eneo letu. Kwahiyo, vyombo hivi vinategemea kuwasili mwishoni mwa mwezi huu na kwa taarifa yenu tu kwamba maonesho tunaendelea nayo ya pale Maisara wakati wa sherehe za Mapinduzi kwa sababu tumeanza kama ni onesho la kudumu kila mwaka tutafanya na tutakapokuwa na eneo letu tutakuwa tunahamia katika eneo letu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu wajasiriamali hatukuishia hapo tunaangalia sasa hivi kwanza tunataka kupitia utaratibu mzima wa suala zima la masoko. Kama mnavyoona wizara yetu bado kitengo cha masoko hatujakuwa nacho lakini tunaangalia sasa katika masoko Mhe. Mwenyekiti kuna mambo mawili muhimu yanatakiwa tuyatizame.

Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumzia masoko kwanza unatakiwa ufanye utafiti, ikiwa unataka kutafuta soko lazima ufanye utafiti. Vilevile, ukishakuwa na soko bila ya kufanya *promotion* bidhaa zako hata kama una soko lazima ufanye *promotion*, ili uwafahamishe wateja wako kwamba biashara zako zipo na za aina gani na kila kitu. Kwahivyo, haya ndio mambo ambayo tunayotaka tuyafanyie utafiti. Pia kuangalia fursa zilizopo kwa mfano Bara, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza kwa masikitiko sana kwamba Soko la Bara linasumbua sana Wazanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwasababu wafanyabiashara wetu wanapokuwa na bidhaa zao wanapata tabu kwasababu kule kunakuwa na mambo mbalimbali yayowafanya wasiweze kuuza. Lakini niseme tu mazungumzo yanaendelea kutaka kujua sisi mipata yetu ni nini katika soko la Bara. Kwakweli mnapokuwa na soko *market access* ni jambo la Kikatiba kwa hivyo hatuwezi kukubali kuona sababu ambazo sio za msingi, tulikuwa tunataka

tuzungumze na tutakuwa na mazungumzo haya mwisho wa mwezi huu, na tutaweza kujuwa hasa nini utaratibu tufanye nini kitakachotokea kwa ajili ya kuondosha vikwazo kama hivyo tunavyoviita vikwazo ambavyo sio vya kukodi. Kwahivyo, hili nalo linafanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine kwa mfano ya sukari na mambo ya *tissue,* mengine haya ni wenyewe. Kuna mambo ambayo tunayafanya sisi wenyewe kwa mfano tatizo kama la sukari, kiwanda chetu kinachouza sukari kina–*compete* na wafanyabiashara wengine. Tumelizungumza hili na linafanyiwa kazi. Lakini kama tutaweza kuwapa nguvu Kiwanda cha Sukari tukawa tunawaachia wao watengeneze sukari na wanao uwezo huo, kwa tafiti tulizofanya mwaka wa 2020-2023 wataweza kutengeneza sukari za kututosheleza Zanzibar nzima na kuweza kuuza nje. Sasa mpaka hapo hao wanaouza biashara za sukari ndio wanaosababisha kule Bara wasione kwamba hii sukari inatoka kiwandani kwetu. Tunazungumza nao na tutaweza kufikia mahali kuweza kupata muwafaka.

Mhe. Mwenyekiti, niunganishe na Soko la *AGOA,* soko hili lipo lakini kwa bahati mbaya Waafrika wengi hatukuweza kutumia Soko la *AGOA*, kwa sababu hatujaweza kuweka miundombinu, kuweka utaratibu mzuri wa kuimarisha bidhaa zetu. Naomba niseme tu kwa upande wa Zanzibar kwa utaratibu wa Soko la *AGOA* hivi sasa hivi tuna wataalamu watakuja karibuni kuona kwa kiasi gani kwa bidhaa hizi tulizonazo sasa tutaweza kuingia Soko la *AGOA.* Soko la *AGOA* tumepewa bidhaa 6666, lakini hatujaweza kutumia hata thuluthi ya Soko la *AGOA.*

Lakini kama tutafanya na wakala huu tumechukua jukumu lake tutaweza kuingia soko la *AGOA.* Kwa hiyo, inategemea ujumbe utakapokuja tutaangalia bidhaa za mwanzo, wao wametwambia kuwa bidhaa za mwanzo wanazoziona zinaweza kuingia ni bidhaa

za viungo, mafuta ya viungo na vyengine vingi vinavyotokana na mambo ya kilimo. Kwahivyo, Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na tutafanya kazi hiyo kuangalia lile soko la *East Africa*, au *South Africa*. Hivyo, hivi sasa kuna mambo ambayo tunaaza sasa hivi Afrika ya Kusini wanachukua bidhaa zetu wanauza wao. Kwa mfano viungo sisi hatujaweza kuvitengeneza. Kwahiyo, soko si tatizo kubwa, soko lipo inabidi na sisi tuliimarishe.

Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza kuhusu suala zima la *SMIDA* na nimeshajibu kuhusu hili na *AGOA* nimeshajibu. Maeneo maalum hili nadhani la mwisho nitakalojibu kwasababu nimeulizwa.

Maeneo maalumu kwa ajili ya bidhaa ya viwanda. Sisi tukishirikiana na Wizara ya Ardhi kupitia na mradi wao ule wa *Special Development* wametupangia maeneo maalum ya viwanda. Kuna maeneo kila sehemu wamepanga, lakini sisi kwa utaratibu huu wa wakala tumesema kila wilaya wanatakiwa nao watutengee eneo maalum la kuweza kufanya kazi za viwanda.

Kwahiyo, hii changamoto nawarushia wenzangu wajumbe kwasababu wote wao ndio wanawakilisha wilaya, wakakae na Halmashauri zao watuambie kila wilaya wataweza kuzalisha bidhaa gani kuanzia kilimo mpaka kwenye viwanda, tumeshapata wilaya mbili Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kati. Wilaya ya Kati wao wamesema wako kwenye asali, Wilaya ya Kusini nao wamesema asali na vitu vyengine wameshatwambia, lakini Wilaya ya Kaskazini Unguja hatujapata taarifa wala Pemba. Kwahiyo, tutafanya kikao ningeomba kupitia wawakilishi wao ndio wadau wakubwa wakakae na wezetu wa wilaya tujue, kwasababu tunataka kuweka *industrial park* katika kila wilaya kuanzia kunako kilimo mpaka katika kutoa *product* ambayo

tutaweza kuiuza kama wanavyotufanyia sasa hivi bidhaa hii ya mwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwahiyo maeneo haya maalum yapo na utaratibu wa bajeti tumejiwekea sisi. Kwa mfano, kwa kujenga tu *SMIDA* peke yake ukichukua pamoja na hizo *industrial park* zilizoko wilayani na mikoani tumepata bajeti ya shilingi milioni 17,691 Dola za Kimarekani. Hizi ndio bajeti ambazo tumepata kwa ajili ya kutengeneza utaratibu mzima kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo ya hii *SMIDA* na *industrial park* za maeneo ya wilayani.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba tumejiandaa na nashukuru kwa michango yote iliyokuwa imechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe, niseme kwamba hii ndio nafasi nzuri sana ya kuweza kuimarisha viwanda vyetu, tuanze kuwasaidia wajasiriamali wetu na tuweze kuwafanya ili waweze kuwa wadau wakubwa. Kitu ambacho nataka kwamba tuwa-*graduate* hawa tuwaweke juu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba nimuite Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutengua kanuni ya muda ili tuweze kupata muda wa kumalizia shughuli yetu hii. Ahsante Mhe. Waziri karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda uliobakia hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu, kwa hiyo niliombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tupate muda wa kutosha kumalizia shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu na marekebisho yake.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogona vya Kati Zanzibar ya Mwaka 2017

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Awali

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 2 Matumizi
Kifungu cha 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Kuanzishwa kwa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mengi ambayo yalikuwa yanatia matumaini, tumuombee Mwenyezi Mungu aweze kufanikisha hayo ambayo ameyalenga, isipokuwa nina suala moja tu katika hiki kifungu cha 4(2) ambacho kilikuwa kinasema, uwakala kuwa ni chombo cha serikali kisichojitegemea.

Sasa, uzoefu ukisema chombo ambacho kisichojitegemea kwa hiyo ina maana kila kitu itakuwa lazima wapate ushauri kwa waziri, na masuala haya ya ujasiriamali ni masuala mengi sana ambayo na wao wakala wanatakiwa wapate nafasi kubwa ya kuweza kufanya maamuzi. Sasa hili nilikuwa naomba kwamba waziri anikubalie kuwa baada ya kusema hiki chombo kisichojitegemea kwamba kiwe ni chombo kinachojitegemea kikamilifu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Hamza Hassan Juma akatizama katika ile ya Kingereza kwasababu wakati mwengine Kiswahili huwa kina mazonge yake. Hii maana yake ni *semi-autonomous*, yaani ina mamlaka ya kutosha lakini haijapewa mamlaka yote. Kwasababu chombo hiki sio cha kibiashara kwamba kina *full mandate* kufanya biashara, hakifanyi biashara. Lakini ukiangalia kazi zake (a), (b) na (c) ni sawa sawa na chombo chengine chochote ambacho kipo katika serikali.

Kwahiyo, kwa hapa ilivyo kina uwezo kabisa na vyombo vyengine vyote kama vina bodi lazima vikashauriane na waziri kama itakavyokuwa vyombo hivyo. Kwahiyo, kwa hali hii ilivyo kwasababu nilisema kitaweza kufanya kazi zake vizuri bila ya kuwa na tatizo na wana uwezo wa kufanya yote haya bila ya kubanwa, ila kuna mambo mengine kwa sababu wana bodi lazima ipite bodi na bodi lazima imshauri waziri, ili kuweza kuendelea na mambo. Hivyo, ni taratibu hata katika sheria ya utumishi wa umma imewekwa hiyo. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi hofu yangu imekuwa moja, unajua sasa hivi sisi ambao kamati zetu tuna mashirika ya serikali pamoja na hizi mamlaka sasa hivi imekuwa hata zile sheria ambazo tumezitunga, mamlaka ya bodi na mengine na vile vyombo vimewekwa kabisa kwamba ni mamlaka ambazo zinajitegemea moja kwa moja. Lakini leo katika maamuzi mengi hasa utakuta katika masuala ya maslahi na mambo mengine inafika pahala vyombo vile au taasisi zile zinakuwa zinalalamika, kwasababu mambo mengi inabidi yanakwamba mpaka yatoke maamuzi mengine kutoka juu, sasa yanakwaza katika shughuli.

Sasa leo zile mamlaka nyengine tayari zinajitegemea moja kwa moja na tayari kuna vikwazo vingi katika utendaji. Jee, hiki ambacho moja kwa moja kwenye sheria kimeshaelezwa kwamba

chombo kisichojitegemea, kwa hiyo ina maana hawa watakuwa sasa hawana uhuru wa kufanya maamuzi kila kitu waende wakaulize? Sasa hiyo ndio hofu yangu. Mimi hofu yangu ni moja tu, kwamba itakuwa kama tunatengeneza urasimu uliokuwa hauna sababu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwasababu hii sasa hivi itakuwa tunarudi kule kule kama Idara ya Maendeleo ya Viwanda sio uwakala. Sasa nadhani hili neno ndio tunaona kidogo litaleta ukakasi, lakini kimsingi kuweko kwa mamlaka ndio pale sasa watakapofunguka wataweza kufanya shughuli zao kwa utulivu zaidi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimemfahamu na nimemsikia Mhe. Hamza Hassan Juma hoja ambayo anaijenga. Ukisoma ile ya Kingereza neno ambalo limetumika ni *semi-autonomous* na ya Kiswahili ili usome vizuri usome neno 'Chombo cha serikali kisichojitegemea kikamilifu', maana yake usome haya maneno yote mawili sambamba usisome neno moja ukaliacha moja.

Mhe. Mwenyekiti, maana yake nini, imekuja hivyo. Kwasababu kwenye utaratibu wa kuunda mashirika au makampuni ambayo ndio yanajitegemea wao kisheria ndio huwa wanakuwa wana *full autonomy*, wanakuwa na hadhi kamili ya kujitegemea. Hizi wakala ukisoma kifungu cha 55 cha Sheria ya Utumishi wa Umma wao wanakuwa hawana sifa za moja kwa moja kamili za kujitegemea ndio maana tunasema hawa wanakuwa ni *semi-autonomy*, wanakuwa hawajitegemei kikamilifu. Lakini Sheria ya Utumishi wa Umma inasema aa! Wana uwezo wa kuwa na bodi zao, wana uwezo wa kuwa na Mkurugenzi Mkuu wao, wana uwezo wa kufanya mambo na kuamua wao wenyewe, lakini zile sifa nyengine za kimashirika wao wanakuwa hawana ndio maana

tunasema wanakuwa wana *semi-autonomy* katika kufanya mambo yao.

Kwahiyo, hili neno lisoke yote mawili ni wakala wa serikali isiyojitegemea kikamilifu. Mara nyengine naweza kukubaliana inawezekana ni tafasiri kutoka kwenye neno *'semi-autonomous'* kuligeuza sasa kuja Kiswahili na ndio maana unaona yamekuja maneno mawili tofauti, kisichojitegemea lakini kuna na kikamilifu; lakini yanatakiwa uyasome maneno yote kwa pamoja. Nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua sitaki tupoteze muda lakini nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu iko haja ya kuiangalia upya Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwasababu ukiangalia hivi sasa hiki kifungu ambacho nakisema kuwa kisichojitegemea kikamilifu, basi nadhani kifungu hiki sasa kingeliwekwa mpaka katika yale mashirika. Kwakweli ile *full autonomy* yenyewe hata kule katika mashirika sasa hivi haipo. Bodi sasa hivi zipo tu, lakini mamlaka ya bodi tayari zimeshachukuliwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshanijua ninakokwenda Sheria ya Utumishi wa Umma kwa kweli imeteka mamlaka zote ikiwemo ya Baraza la Wawakilishi. Naomba tuendelee.

Kifungu cha 4	Kuanzishwa kwa Wakala pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 5	Uwezo wa Wakala pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 6	Muhuri wa Wakala
Kifungu cha 7	Kazi za Wakala pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Uongozi na Utawala wa Wakala

Kifungu cha 8	Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 9	Majukumu ya Mkurugenzi Mkuu pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 10	Wafanyakazi wa wakala pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 11	Bodi ya Wakurugenzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 12	Muda wa Wajumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 13	Utaratibu wa Vikao vya bodi
Kifungu cha 14	Kujiuzulu kwa Mjumbe wa Bodi
Kifungu cha 15	Nafasi ya Mjumbe kuwa wazi
Kifungu cha 16	Katibu wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 17	Posho kwa Wajumbe pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 18	Uwezo wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 19	Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 20	Kamati za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 21	Marufuku ya Kutangaza au kutoa taarifa kwa mtu asiye na mamlaka
Kifungu cha 22	Fedha za Wakala pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 23	Makadirio pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 24	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru tena kunipa nafasi hii nilikuwa naomba ufafanuzi katika kifungu hiki cha 24(a) kinachosema "Fedha za Wakala zitatumika kama hivi ifuatavyo: Mishahara, maposho na mikopo ya wafanyakazi wa wakala".

Sasa kwa uzoefu wangu tunapopitisha hizi sheria haya masuala ya kusema kwamba mikopo ya wafanyakazi ya wakala inakuwa hatuja-*experience* suala hilo sasa lakini hapa naona limejiingiza. Nilijenga hoja kwamba hapa fedha za wakala ibakie tu kwamba mishahara na maposho hii mikopo ya wafanyakazi wa wakala iondolewe. Kwasababu tunajua watumishi wa umma wote kuna utaratibu maalum wa upewaji wa mikopo kupitia kwenye mishahara yao. Sasa kuongeza neno kama hili hapa kidogo linaweza likahamasisha mtu kuona kwamba mimi sasa hivi niende nikakope lakini atakopa nini bila ya kupitia katika mshahara wake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba haya maneno na mikopo ya wafanyakazi wa wakala yaondolewe ibakie suala la mishahara na maposho. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye tunaweza kukiondosha hicho hakina dhara yoyote, kwasababu tayari imo katika taratibu za serikali kinaweza kikaondoshwa tu hamna neno.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mwalimu wangu Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Balozi Amina Salum Ali kwa kunikubalia.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sipingani na yale ambayo ameyasema Mhe. Waziri ambayo tayari ameshakubali. Mawazo yangu ambayo ninayo ni kwamba hiki kifungu cha 24

chote ndio tukaweza tukakiondoa. Kwasababu sheria nyingi ambazo tunatunga matumizi ya fedha tayari yanajulikana namna gani ya utaratibu wake. Ukiyaweka hapa kisheria halafu ukaja ukatumia baadae watakuja kutuhoji hawa waheshimiwa.

Kwahiyo, sio sheria nyingi tunazotunga tunaweka utaratibu huu. Hivyo, nilidhani hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma ilikuwa zaidi ya kuki-*broke* kifungu cha 24 chote. Kwakweli, ukikisoma kifungu cha 24 kinachosomwa ni mishahara na maposho, utaratibu wa kulipa mishahara kwa wafanyakazi unajulikana. Lakini ya pili, fedha nyengine zinazokubaliwa kwa usafiri utaratibu unajulikana, na kulipa maposho ya bodi utaratibu wake unajulikana, na gharama nyengine zote zinazostahiki kulipwa na wakala. Kwahiyo, ushauri wangu hichi kifungu cha 24 chote tukiondoe. *(Makofi)*

Kifungu cha 24 Matumizi ya Fedha pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kifungu kimekubaliwa pamoja na marekebisho yake. Marekebisho yenyewe ni kufutwa, kuondolewa kabisa chote hicho. Tumekubaliana?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Haya.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika kuweka *hansard* yetu sawa itolewe kauli safi haya mapendekezo aliyotoa Mhe. Mwanasheria Mkuu, ili tuyakubali.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Mwanasheria Mkuu alisimama kwa marekebisho kwamba yafanywe kufutwa

kabisa. Sasa ndio tunahoji hapa hayo marekebisho yenyewe kwamba kiondolewe kabisa. Tumekubaliana hivyo?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mwongozo wako kidogo. Mhe. Mwenyekiti, tukubaliane lugha marekebisho na kufutwa. Vilevile tukubaliane na kwenye *numbering*, ina maana kama tutakuwa kifungu hichi tumekifuta moja kwa moja, kwa hiyo ina maana vifungu vitakavyobakia sasa visomeke kwamba kifungu cha 25 itabidi kisomeke kifungu cha 24 na vyengine kitu kama hicho. Maana yake kama itakuwa marekebisho ina maana kifungu kitabakia kutakuwa kuna marekebisho tu, lakini kama kufutwa mpaka *numbering* itabidi zibadilike huko tunakokwenda. Mhe. Mwenyekiti, mwongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaposema kwamba kiondoke hichi ina maana ndio miongoni mwa marekebisho.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, sawa sawa anavyosema Mhe. Mjumbe namba zitabadilika. Kifungu kizima hichi kitolewe chenye (a), (b) n (c) na namba zitabadilika.

Kifungu cha 25 Hesabu za Ukaguzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati

Kifungu cha 26

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa naomba msaada wa Mhe. Mwanasheria Mkuu moja kwa moja kwasababu nilipendekeza katika kifungu hichi cha 26 (3) vyanzo vya fedha vya mfuko ni vikijumuisha, sina haja ya kupoteza muda kuvitaja (a), (b) na (c). Lakini nilipendekeza tuongeze (d) kwamba asilimia moja ya ushuru wa bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi. Kwasababu ina maana hapa tutakuwa tuna kianzio cha uhakika ambacho kila siku fedha zinaingia kama tulivyotengeneza Sheria ya *ZURA* katika zile fedha za kuendeshea Mamlaka ya *ZURA* kwamba fedha zile kutakuwa kuna kianzio na tumeona manufaa yake. Hata Mfuko wa Barabara.

Sasa hili ndio maana nikasema naomba ushauri au maelekezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu tutafanya vipi. Aidha, kusubiri tutakapopitisha Bajeti Kuu ya Serikali. Nadhani kama ni vyanzo vya fedha lakini kwa bahati mbaya tulipokuwa tunapitisha ule mswada wa fedha hatukuingiza au hazikutajwa fedha hizo. Lakini hiki chombo kwa umuhimu wake na kwasababu wakala wanakuja kuimarisha Viwanda Vidogo Vidogo. Kwahiyo, kubana zile bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi asilimia fulani ya fedha ikaingia katika mfuko wa viwanda itasaidia kukuza hivi viwanda vyetu vidogo vidogo vya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa nataka tu maelekezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu hili wazo kama linaweza likakubalika. Jee, hapa ni pahala pake au itabidi sasa tuje tusubiri kwenye Bajeti Kuu ya Serikali kuja kuangalia katika zile tozo mbalimbali. Kwasababu hata hizo kodi za *TRA* ambazo ndio unazosema

kwamba kupitia ushuru utakaoingizwa bidhaa sasa hivi tayari imeshakuwa *budgeted* na haikulengwa katika kusaidia hivi viwanda. Sasa nilikuwa nataka tu ushauri wa kisheria sijui tunaweza tukafanya vipi. Lakini lengo ni kubana bidhaa zinazoingia nchini ili zile fedha ziingie katika kuimarisha viwanda vyetu vya ndani. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, wazo la Mhe. Hamza Hassan Juma ni zuri kwa sababu kwanza ukilitizama kwa kuendesha hii mifuko ambayo tunaianzisha, basi kila mfuko unaoanzishwa lazima uwe na aina ya fedha ambao utaufanya ule mfuko nao uendelee kuwepo na kutumika. Kwahiyo, kwa wazo nasema ni zuri, lakini kwa pendekezo lake kama tuiweke hapa sasa hivi kwa hilo halitowezekana kwasababu kwanza tayari tumeshapitisha Bajeti yetu ile ya Serikali na utaratibu wake mzima umeelezwa.

Lakini la pili, tayari tuna mfuko wetu ule wa *Infrastructure Fund* ambao ndani yake imewekwa asilimia ya kugawa kwenye mifuko yote ambayo inaanzishwa. Sasa ipo mingi hii, upo wa UKIMWI, upo wa Mazingira, mifuko mingi tunaanzisha na *fund* zake zote zinakwenda kwenye ule mfuko wa *Infrastructure Fund.*

Sasa kwa wazo la Mhe. Hamza Hassan Juma ambalo amelitoa kwa kufanya mifuko hii iendelee na tutafute chanzo cha fedha nasema ni zuri. Lakini kwa kuliweka hapa sasa hivi hilo halitowezekana. Ndio maana hata na sisi tukaamua kuja na vyanzo hivi vya kuanzia navyo ili labda baadae tutakapokuja sasa mwakani kwenye Bajeti yetu ya Serikali kama kutakuwa na uwezekano wa kuzidisha, au serikali kuamua kuweka utaratibu mwengine wa kuwezesha hii mifuko tunayoanzisha basi tuje kufanya hivyo. Lakini kwa sasa hivi mimi ningemuomba haya yaliyokuwepo ndio yatosheleze ili tuendelee. Lakini wazo lake ni zuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ndio maana nikasema nipate maelezo wapi pa kuweka. Lakini kutokana na umuhimu wa hii sekta na huu mfuko ili uwe endelevu, basi mimi nafikiri kuanzia sasa hivi mimi pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu na huo uwakala tuanze kuangalia. Jee, ile fedha niliyoisema ya bidhaa zinazoingia nchini tunaweza tukafanya nini? Mimi nilipendekeza asilimia moja, lakini wao wajaribu kuangalia kibajeti itaweza kuathiri vipi ili tuje kupata fedha hizo.

Kwa mfano, ukiangalia kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu hata suala zima la mazingira katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji kuna fedha maalum inatozwa kwa ajili ya kusaidia masuala ya uhifadhi wa mazingira. Sasa sisi tunataka kujenga au kulinda kuimarisha viwanda vyetu vya ndani. Kwahiyo, hili nafikiri tupeane kazi kwa sote na nitakuja nalo kwenye bajeti, ili kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapatikana mfuko wetu huu uweze kutuna Mhe. Waziri aweze kufanya kazi zake vizuri. Ahsante.

Kifungu cha 26	Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 27	Usimamizi wa Mfuko
Kifungu cha 28	Matumizi ya Fedha za Mfuko pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 29	Ripoti za Hesabu

Sehemu ya Tano

Vifungu vya Fedha

Kifungu cha 30	Bajeti ya Mwaka na Bajeti ya Ziada

Kifungu cha 31 Ukaguzi wa Hesabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 32 Taarifa ya Mwaka ya Mkurugenzi Mkuu

Sehemu ya Sita

Masharti Mengineyo

Kifungu cha 33 Waziri kutoa Maelekezo ya Kisera kwa Bodi
Kifungu cha 34 Usajili wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 35 Makosa na Adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 36 Kinga
Kifungu cha 37 Kanuni

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, sasa naomba Baraza lako tukufu liyakubali. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Uwakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar ya mwaka 2017

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Uwakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar pamoja na Kuwezesha Ushajihishaji na Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo,Vidogo na vya Kati Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya tatu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya MakamU wa Pili wa Rais kutengua kanuni ya muda tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya MakamU wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa shughuli za leo zimemalizika, na kwa kuwa kwa sasa tutakuwa na shughuli nyengine muhimu mbele yetu hapo. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako tukufu liahirishe kikao hichi mpaka Jumatatu tarehe 11 Disemba, 2017 sasa tatu za asubuhi barabara. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji kwanza wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaliahirisha Baraza naomba nitoe tangazo maalum. Waheshimiwa Wajumbe, wote baada ya kutoka hapa ifikapo saa nane tunatakiwa tuhudhurie katika semina. Baada ya kutoka hapa tunapumzika kwa muda saa nane tunarudi tena ukumbi wa juu kwenye semina mpaka tutakapomaliza shughuli yenyewe. Kwahivyo, Waheshimiwa Wajumbe, wote wabaki katika ukumbi huo, sasa hivi ni muda wa mapumziko na kusali na baadaye saa nane tuwe katika ukumbi, kwa ajili ya semina hiyo. Tumeelewana?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, baada ya hayo naomba niakhirishe Baraza hili hadi hapo siku ya Jumatatu mnamo saa tatu za asubuhi.

(Saa 7:17 mchana Baraza liliakhirishwa hadi

tarehe 11/12/2017 saa 3:00 asubuhi)